ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1. Mhe. Ali Abdalla Ali	Naibu Spika/Jimbo la Mfenesini.
2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Mwenyekiti wa Baraza Jimbo la Kikwajuni.
3. Mhe. Mgeni Hassan Juma	Mwenyekiti wa Baraza/ Nafasi za Wanawake.
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamu wa Pili wa Rais/Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Kuteuliwa na Rais.
5. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora/ Jimbo la Dimani.
6. Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Fedha/ Kuteuliwa na Rais.
7. Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/JimbolaTumbatu
8. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais.
9. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais/ Kuteuliwa na Rais.
10.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
11. Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/ Waziri wa Afya/Jimbo la Ziwani.
12.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati/ Kuteuliwa na Rais.

13.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Kuteuliwa na Rais.
14.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais.
15.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni.
16.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge.
17.Mhe Dr. Sira Ubwa Mamboya	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Kuteuliwa na Rais.
18.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara,Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni.
19.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo/Jimbo la Gando.
20.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma/Jimbo la Makunduchi.
21.Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni.
22.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
23. Mhe. Shawana Bukheit Hassan	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Dole.
24. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka.

25. Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake.
26.Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
27.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake.
28.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/ Jimbo la Nungwi.
29.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni.
30.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Mpendae.
31.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake
32.Mhe. Said Hassan Said	Mwanasheria Mkuu.
33.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
34.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
35.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
36.Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais
37.Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
38.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
40.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake

43.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
44.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
45.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
46.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
47.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
48.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
49.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
50.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
51.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
52.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
53.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
54.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
55.Mhe. Marina Joel Thomas	Kuteuliwa na Rais
56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando)	Jimbo la Mkwajuni
57.Mhe. Mlinde Mabrouk Juma	Jimbo la Bumbwini
58.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
59.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali	Jimbo la Uzini
60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi	Jimbo la Chambani
61.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
62.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
63.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
64.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo

65.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
66.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
67.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
68.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
69.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
70.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
71.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
72.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
73.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
74.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
75.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
76.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
77.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	Jimbo la Jang'ombe
78.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Tisa - Tarehe 27 Mei, 2015

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Mwenyekiti (Mahmoud Mohammed Mussa) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Ikulu na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora kwa mwaka 2015/2016.

Mhe. Hamza Hassan Juma (Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa): Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa naomba kuwasilisha hati mezani kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora. Ahsante.

Mhe. Fatma Mbarouk Said (Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika (*PAC*): Mhe. Mwenyekiti, naomba kuweka hati mezani ya Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika (*PAC*) kuhusiana na Bajeti ya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka 2015/2016.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 74

Idadi ya Maswali yaliyoulizwa Barazani

Mhe. Saleh Nassor Juma (Kny. Mhe. Jaku Hashim Ayoub) - Aliuliza:-

Maswali ni njia moja inayotumiwa na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi katika kuhoji utekelezaji wa shughuli za serikali. Na kwa kuwa Wajumbe huwa wanauliza maswali hayo kwa serikali katika kila kikao ili kupata majibu ya serikali. Na kwa kuwa Mkutano unaofuata utakuwa ndio wa mwisho katika Baraza hili.

(a) Je, ni maswali mangapi yameulizwa katika Baraza hili la Nane lililoanzia mwaka 2010 hadi 2015.

(b) Katika maswali yaliyoulizwa ni mangapi yamejibiwa na mangapi hayakujibiwa.

(c) Ni wizara gani mpaka sasa iliyowahi kuulizwa maswali mengi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako kabla ya kujibu swali naomba kwanza nimpongeze Mhe. Saleh Nassor Juma kwa kumuwakilisha vizuri Mhe. Jaku Hashim katika maswali yake.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 74 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Mwenyekiti, katika Baraza la Nane la Wawakilishi lililodumu katika kipindi cha miaka mitano (2010 – 2015) maswali yaliyoulizwa ni 4,897, kati ya haya maswali 1,721 yalikuwa ya msingi na maswali 3,250 yalikuwa ya nyongeza.

b) Mhe. Mwenyekiti, kati ya maswali ya msingi 1,721 yaliyoulizwa, maswali 1,647 yamejibiwa na maswali 74 hayajapata muda wa kujibiwa.

c) Wizara ya Afya ndio iliyoulizwa maswali mengi zaidi ikifuatiwa na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano na Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri mdogo wangu hapa Mhe. Muhammed Aboud Muhammed naomba niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa kazi ya kutunga maswali Mhe. Waziri na kuyawasilisha hapa ni kazi kubwa sana ambayo inahitaji *thorough feasibility study*, na kwa kuwa ameniambia kuwa kuna maswali 74 bado hayajapata majibu.

Je, maswali haya yaliyobaki yatamaliziwa kupata majibu katika hili Baraza la mwisho la 20 kwa kipindi hiki.

Pili, kwa kuwa Wawakilishi wanafanya kazi hiyo ya kutunga maswali inakuwa wanafanya kazi kubwa sana kutunga maswali 1,721 ya msingi ni kazi kubwa sana. Je, Mhe. Waziri kwa kuwa sisi hapa tukimaliza kazi za Baraza za kila mwaka tunakwenda Arusha kupumzika na kucheza mpira kule.

Je, kwa hawa watu waliojitahidi kutunga maswali 1,721 unaweza angalau wale watu wawili walioiouliza maswali mara nyingi humu ukawapatia nafasi ya kwenda kupumzika kidogo angalau Rushdie, Dubai au pale Muscat. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kujibu maswali ya Mhe. Saleh Nassor naomba nitoe maelezo mafupi yafuatavyo.

Mheshimiwa nataka nikubaliane kabisa na Mhe. Saleh Nassor kwamba kazi ya kuuliza maswali ni kazi ngumu na inapaswa kuwapongeza sana Waheshimiwa wa Baraza hili tukufu, kwa namna ya umahiri na uwezo wao mkubwa wanavyouliza maswali. Ingewezekana sana kama uwezo upo basi hawa wanaoliza maswali mazuri namna hii wakapata nafasi ya kupongezwa na kwenda kupumzika mahali. Lakini kwa bahati mbaya sana uwezo wa hali yetu ya uchumi bado hauruhusu kutoa zawadi za namna hiyo za kwenda kupumzika nje ya nchi. Lakini nawaomba wenyewe kwa kujifurahisha kwa kazi kubwa waliyoifanya basi wangefanya kuchangishana ndani ya Baraza hili wakafanya tafrija ndogo ama kuwachangia wale walioiouliza maswali mengi kwa nia ya kwenda kupumzika huko Dubai na kwengineko.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo sasa naomba kujibu swali la Mhe. Saleh Nassor Juma lenye (a) na (b). Maswali ambayo bado hayajapata majibu, Baraza letu tukufu linafanya kila jitihada ili serikali iweze kutoa majibu ya maswali hayo. Pale ambapo hayatoweza kumalizwa kujibiwa katika Baraza hili naamini Mhe. Mwenyekiti, maswali hayo yatakwenda kwenye Baraza lijalo, kwa sababu naamini Waheshimiwa Wawakilishi hawa wote watarudi tena katika Baraza hili. Kwa hivyo, hamna haja ya kuwa na wasiwasi wapate kuyasikiliza majibu yao.

Kuhusu safari ya Dubai ni kama nilivyoeleza katika maelezo yangu ya awali kwamba haiwezekani, hakuna uwezo huo wa kuwapa zawadi hiyo. Mhe. Mwenyekiti, nashukuru sana.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Mhe. Mwenyekiti, ahsante na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza dogo tu, kwa kuwa Mhe. Waziri katika swali lake mama alisema maswali elfu moja na zaidi yaliyojibiwa. Katika maswali hayo yaliyojibiwa na kwa kuwa humu wengi wao huuliza maswali.

Je, ni nani wa mwanzo ambaye aliuliza maswali mengi na nani wa mwisho ambaye alikosa kuuliza maswali. Mhe. Mwenyekiti, ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, nafikiri homa ya uchaguzi imeanza kwa hiyo si vizuri kwa sababu sote tuko hapa

wale waliokuwa wameuliza, waliokuwa hawakupata nafasi ya kuuliza lengo letu ni moja. Waheshimiwa nia na madhumuni makubwa ni kwamba tunafanya kazi kwa pamoja.

Kwa hiyo, mimi ningependa niwapongeze Wawakilishi wote kwa kazi nzuri waliyoifanya wakati wote na wale walioweza kuuliza maswali mengi tunawapongeza na wale wasiopata nafasi ya kuuliza nao tunawapongeza, kwa sababu kila mmoja ana haki yake katika Baraza hili tukufu.

Mhe. Mwenyekiti, maswali yaliyoulizwa ya msingi yalikuwa 1,721, maswali ya msingi yaliyojibiwa ni 1,647, yaliyokuwa bado hayajajibiwa kwa sababu ya muda na yatajibiwa ni maswali 74. Maswali ya nyongeza kama nilivyosema ni 3,250. Kwa hivyo, serikali nayo tuipongeze sana imefanya kazi kubwa ya kujibu, mawaziri na manaibu waziri wamekuwa mahiri kwa kujibu maswali ya Waheshimiwa kwa hivyo na wao wangepaswa sana kupongezwa na wao ndio wa kupewa zawadi kwa wakati huu, lakini kama nilivyosema kutokana na hali ilivyo hakuna nafasi hiyo tuwapongeze kwa kila mmoja kutekeleza majukumu yake.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa utaalamu wake wa kujibu maswali mazito kama haya. Mimi swali langu ni kwamba, kwa maelezo ya Mhe. Waziri ni kuwa maswali yote yalikuwa 4,867; kati ya hayo 1,721 yalikuwa ni maswali ya msingi, 1,747 kama nilisikia vizuri yalikuwa ni maswali ya nyongeza lakini kuna maswali 74 mpaka leo hayajajibiwa wala hayamo katika kujibiwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu Mhe. Mwakilishi anapouliza swali huwa anahitaji jibu na mara nyingi maswali huwa yanahusu majimbo yao na shughuli za serikali. Lakini uzoefu nilionao ni kuwa wakati mwengine Mheshimiwa anapeleka swali linakaa mpaka kipindi chengine kinachofuata ndio linajibiwa, lakini kuna wengine hupeleka hivi karibuni tu na wakapata majibu. Mimi swali langu liko hapa.

Haya maswali 74 yaliyobakia ni kwa sababu yalikuwa hayana uzito kama mengine, na kama yalikuwa yana uzito kama mengine ilikuwaje tukaingia katika vikao siku nyengine ikawa kuna swali moja tu, siku nyengine mawili tu, kama leo matatu tu ya kuuliza na haya yakaachwa mpaka hivi leo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, serikali siku zote iko tayari kujibu maswali yote, lakini kutokana na shughuli zetu za ndani ya Baraza wakati mwengine huwa tunafupisha kipindi cha maswali na majibu kwa nia ya kufanya majukumu mengine. Lakini pia nataka nilipongeze sana Baraza hili la serikali kwa sababu ukichukulia Mabunge mengine duniani na idadi ya maswali yalivyojibiwa na hiyo idadi iliyobakia ni ndogo sana na bado tumo

katika kipindi hiki cha Baraza hili la bajeti, naamini mengine mengi ambayo bado yamebaki yatapatiwa majibu.

Kwa hiyo, kwanza hatuna budi tujipongeze wenyewe kwa kazi kubwa ya maswali hayo. Kama nilivyosema maswali ya msingi yalikuwa 1,721 lakini maswali ya nyongeza 3,250. Kwa hiyo muone kwamba Waheshimiwa Mawaziri na Manaibu Waziri wako mahiri na wako tayari kujibu maswali hata yale ya nyongeza ambayo yanaibuka hapa hapa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hiyo jibu langu kwa Mhe. Salim Abdalla Hamad ni kwamba tuendelee kuvuta subira kwa yale yote ambayo yamewahi kujibiwa na si kwa sababu swali moja lilikuwa na uzito zaidi kuliko swali jengine, lakini inajitokeza kutokana na ratiba na ufinyu wa muda wakati mwengine ndio maana swali lile ambalo leo lilikosa nafasi linapelekwa mbele ndio tatizo linapojitokeza. Wakati mwengine pengine waziri mhusika pia amedharurika kwa siku hiyo akaomba swali lake lipelekwe mbele.

Kwa hiyo, jambo la msingi ni kwamba muda na dharura mbali mbali zinazojitokeza ndio sababu zinazosababisha maswali mengine yasipate majibu kwa siku iliyotarajiwa. Haya ni mambo ya kibinadamu ni nje ya uwezo wa binadamu, inaweza kutokea dharura yoyote ile au ya jambo lolote. Kwa hivyo, ni vyema tukavumiliana lakini tujipongeze kwa kazi kubwa na nzuri iliyofanyika ya maswali na majibu yake.

Nam. 9

Msaada wa Serikali Katika Ujenzi wa Kituo cha Afya Vikunguni

Mhe. Saleh Nassor Juma - Aliuliza:-

Kwa kuwa lengo la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kuhakikisha kuwa wanajenga Vituo vya Afya vya kutosha ili kutoa huduma ya afya kwa wananchi pamoja na kuweza kuimarisha afya ya mama na mtoto. Na kwa kuwa wananchi wa kijiji cha Vikunguni kupitia juhudi zao wenyewe wameamua kujenga kituo cha afya ambacho kimebakia kumalizia (*finishing*) pamoja na kuweka samani ili kianze kazi. Na kwa kuwa wananchi wanaonekana kukaribia kushindwa kumalizia hatua hizo kutokana na hali ya umasikini na uchache wa kipato.

Je, ni lini serikali itaelekeza nguvu zake yenyewe au kupitia ufadhili, kumalizia kazi hizo ili wananchi wa Vikunguni waweze kupata huduma ya afya sambamba na kuimarisha afya ya mama na mtoto katika kijiji hicho.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti ahsante sana, kwanza naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia sote tukiwa hapa wenye afya njema na wazima. Pili naomba kwa ruhusa yako Mhe. Mwenyekiti, kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 9 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Afya imeweza kuchukua hatua mbali mbali zikiwemo hatua zifuatazo:-

Kwanza kabisa Wizara ya Afya ilifanikiwa kuchangia vifaa vya ujenzi katika ujenzi huo kama vile saruji na hard board.

Pili, baada ya hapo wizara imehangaika sana kutafuta mfadhili wa kuweza kumalizia jengo hilo na kwa bahati nzuri wizara imebahatika kumpata mfadhili ambaye anaitwa *MILELE Foundation* kutoka Dubai, *United Arab Evidence* Umoja wa Nchi za Falme za Kiarabu ambaye yeye amekubali kujenga nyumba ya kuishi wafanyakazi pamoja na kituo cha afya eneo hilo hilo.

Mhe. Mwenyekiti, jengo lililokuweko ambalo sasa hivi wananchi wamekusudia kulijenga kama kituo cha afya sasa kitafanyiwa marekebisho na Milele Foundation na kuwa nyumba ya wafanyakazi.

Pia kujenga kituo cha afya cha kisasa tumekubaliana nao kwamba watajenga kituo cha kisasa cha afya ambacho kitaweza kukidhi mahitaji ya utoaji huduma mbali mbali katika eneo hilo, zikiwemo huduma za kina mama na watoto kwa wananchi wa Vikunguni na maeneo yaliokuwa karibu na hapo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa muda huu tunawaomba na tunawataka wana jamii kujitayarisha kwa ujenzi huo na bahati hatimiliki ya eneo hilo tayari wameshatukabidhi wizara pamoja na *Site Plan* ya eneo hilo na ujenzi unatarajiwa kuanza mwezi ujao yaani mwezi wa Juni 2015 panapo majaalia, *inshaallah*.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na maelezo ya mfadhili huyo *Milele Foundation* ambaye ameshatupatia tayari na mikata ambayo yeye *Milele Foundation* ameingia pamoja na mkandarasi. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza napenda kuipongeza serikali kwa kuweza kutupatia mfadhili wa kuweza kutujengea au kutumalizia kile kituo cha Afya pamoja na nyumba ya Madaktari. Kwa hivyo, nachukuwa fursa hii kuipongeza serikali kwa kufanya kazi hiyo.

Sasa swali ni kwamba kwa kuwa wananchi wa kijiji cha Vikunguni wanategema sana Hospitali ya Vitongoni *Cottage Hospital* sambamba na Hospitali ya Chake Chale pamoja na ya Gombani, ambazo zote ziko karibu kilo mita tano kutoka Vikunguni na kwa kuwa mpango wa serikali yetu ni kupunguza vifo vya mama na mtoto, na kwa kuwa wajawazito kutembea kilo mita tano kufuata huduma ya mama na mtoto ni kazi kubwa kwa kipindi cha karibu miaka miwili na nusu pengine mpaka ipatikane *finishing* ya majengo hayo.

Je, isingekuwa vyema serikali kwa kutumia lile lile jengo liliopo huku majenzi yanendelea wakaweza kutoa pale Vikunguni angalau huduma ya afya ya mama na mtoto kabla ya *Milele Foundation* kutukabidhi hayo majengo, si vyema angalau wangeweka *temporary* huduma ya dharura pale Vikunguni kwa huduma ya afya ya mama na mtoto huku majengo haya yakiendelea, ili kuwapunguzia budhuza wamama wajawazito na wazazi kutoka Vikunguni pale hadi Vitongoji *Cottage* au Gombani.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Wazo hilo tumelipokea na tutalifikisha kwa kile kitengo cha kwenda kuwafata mama na watoto kwa ajili ya huduma zao. Kwa hivyo, wazo hilo tumelipokea na tutaliwasilisha kulifanyia kazi. Ahsante sana.

Mhe. Raya Suleiman Hamad: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, namshukuru Mhe. Waziri kwa majibu mazuri na niishukuru serikali ya Zanzibar kwa kujenga vituo kila pahala kuwaondolea usumbufu wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, kujenga ni jambo jengine na huduma ni kitu chengine, kwa vile vijijini tuna matatizo sana ya madaktari kuhudumia wanawake na watoto. Ni lini serikali itajipanga kuweza kutuletea madaktari kutuondolea usumbufu wa kuweza kwenda Gombani au Chake Chake katika vituo vilivyomo vijijini kupata huduma za mama na mtoto katika chanjo na mambo mengine.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Naomba kwanza nikubaliane nae asilimia mia moja kwamba kuwa na jengo tafauti na kuwa na huduma ni vitu viwili tafauti. Kule wenzetu nchini India sehemu nyengine wao hawana majengo lakini wanatoa huduma katika yale mahema au sehemu nyengine wamejenga baraza chini ya mti inatolewa huduma za vipimo mbali mbali, kwa sababu hawakuweza kufikia hatua ambazo sisi tumeweza kufikia kutokana idadi ya watu waliokuwa nayo wao.

Kwa hiyo, kwa upande wa huduma naomba nimshukuru Mheshimiwa kutoa mawazo haya sisi tunaendelea bado kufanya mawasiliano na wenzetu wa Utumishi kwa sababu tunahitaji kuchukuwa uajiri vijana zaidi.

Kwa bahati nzuri Chuo chetu cha Afya kinazalisha watoto wengi kila mwaka takribani watoto 250 vijana ambao wanamaliza masomo yao pale mbali mbali, kuna fani nane pale ambazo zinatolewa na fani hizo pia zinahusiana na hizi huduma ambazo umezitaja Mheshimiwa.

Kwa hiyo, tutaendelea kujitahidi kadri uwezo utakaporuhusu Bajeti ya Serikali itakaporuhusu kuongeza idadi ya wafanyakazi, ili waweze kutoa huduma hata pale panapokuwa hapana vituo vya afya vilivyojengwa, lakini kwa kupitia huduma zao za kuwafikia walengwa moja kwa moja kwa kuunda zile kambi za muda basi tutajitahidi kufanya hivyo kadri tutakapopata vibali vya kuwaajairi watoto wengine, ili tuweze kufikia malengo hayo. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nashukuru na mimi kunipa nafasi kuuliza kwa Mhe. Naibu Waziri. Lakini kabla ya kumuuliza Mhe. Waziri Mhe. Mwenyekiti, napenda sana niwapongeze Jeshi la Polisi Mkoa wa Kaskazini hasa katika Wilaya ya Micheweni kwa kufanikiwa kutuliza ghasia iliyojitokeza juzi usiku baada ya mwananchi mmoja aliepachika bendera ya CUF kuvamiwa na wana CCM kijiji kizima kwa mashoka na mapanga wakataka kumuhasiri, lakini Jeshi la Polisi likafanikiwa kumnusuru mwananchi yule na bila ya kuumia mwananchi mwengine yeyote.

Kwa hiyo, nawapongeza sana nawaomba waendelee kufanya kazi zao vizuri na pia nawaomba watumie ustarabu wa sheria, ili wote wale waliotaka kuhatarisha amani iliopo katika nchi yetu waendelee kudhibitiwa.

Mhe. Mwenyekiti, swali langu namuuliza Mhe. Waziri kwanza naipongeza serikali, nawapongeza wafadhili waliojitokeza kujenga kituo hichi cha Vikunguni lakini kwa sababu pale wananchi wanashida hasa wanawake na wazazi. Je, haioni serikali kujitokeza ikaongeza fedha kidogo ikanza kujenga kabla ya mfadhili kuja yeye akamalizia tu.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, naamini pongezi wameshazipokea na wameshazisikia wao wenyewe. Ila ninachotaka kusema kwamba kwa baadhi ya vituo ambavyo wananchi wanajitolea kufikia *stage* fulani Wizara ya Afya uwezo ukiruhusu huwa tunaingia moja kwa moja kuwasaidia. Lakini sasa hivi kwa bahati nzuri sana tunamshukuru Mwenyezi Mungu tumepata wafadhili wawili wakuu ambao wanakwenda moja kwa moja kwenye vituo hivi vidogo vidogo.

Mhe. Mwenyekiti, wa kwanza huyu *Milele Foundation* yeye takribani amekubali kuvitengeneza vituo takribani 38 vyote jumla yake na wa pili ni *ORIO* kutoka

Serikali ya Uholanzi ambalo ni shirika lao la misaada la kimataifa wao pia wamekubali kutengeneza vituo kama 22.

Hiyo ni mbali na ule msaada tulioupokea kutoka kwa *ADB* walioshughulikia nao takribani vituo 38 pamoja na ile nyumba nzuri ya daktari ambayo Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji aliifungua katika Sherehe za Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar.

Kwa hiyo, naomba nikubaliane nae Mheshimiwa kwamba hivi sasa hatutaki tena kuongeza vituo kwa sababu vituo vimeshatoleza. Hivi sasa tuna upungufu wa nyumba za wale wafanyakazi kukaa. Wafanyakazi wetu wengi walalamika wanatoka maeneo ya mbali kwenda kutoa huduma na wakati wa kurudi wakati mwengine huwa wanakosa usafiri.

Kwa hiyo, nakuombeni Waheshimiwa sasa hivi tusielekee kwenye vituo tena tuelekee kwenye nyumba za wafanyakazi. Kwa sababu ukiwa umejenga nyumba ya wafanyakazi pia umewatumikia wananchi wako waliokupigia kura, kwa sababu kwa kuweka nyumba ya wafanyakazi umekiimarisha kile kituo zaidi kwa kuweza kuleta wafanyakazi wakaweko pale pale na huduma zile zikapatikana masaa 24. Kwa hivyo, muhimu sana tunakuombeni vituo vya afya sasa basi kwa muda huu kwa sababu vimetosheleza.

Mapungufu yetu makubwa yaliokuwepo ni nyumba za wafanyakazi ambao vituo vile vipo, ili waweze kukaa pale. Wafanyakazi wengine huwa wanakaa kabisa kwa sababu huwa wanakosa usafiri na maeneo mengine niliyotembea hasa katika Jimbo lako kuna kituo kimefunguliwa kipya kizuri tu, lakini hakijatumika mpaka leo pale pembeni ya tulipofanya Baraza la Idd jina limenitoka kidogo.

Ni kituo kizuri cha kisasa lakini mpaka leo hatujui tatizo ni nini wafanyakazi wanafika pale kwa muda lakini watu wamezoea ile Hospitali kubwa wanakwenda kule ndio imani yao.

Sasa tunasema hivi sasa vituo sasa basi kama kuna Wawakilishi, pamoja na wananchi, pamoja na fedha za jimbo labda *CDF* tunataka kufanya basi tuelekezeni kwenye nyumba za wafanyakazi vituo vile vitaimarika kwa kuwapata wale wafanyakazi wa Wizara ya Afya ama watoa huduma ama madaktari ama *CO* au *Nursing* watakuwepo pale kwa masaa 24. Kwa hiyo, huduma pia zitapatikana masaa 24 vituo vile. Ahsante sana. (*Makofi*)

TAARIFA

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Micheweni alipokuwa akiuliza swali lake ya nyongeza ameeleza kuwa Mkoa wa Kaskazini Pemba na kuweza kuwapongeza Jeshi la Polisi kwa kutuliza amani na utulivu kwenye Mkoa wa Kaskazini Pemba Jimbo la Micheni.
Mhe. Mwenyekiti, taarifa aliyotoa Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Micheweni kama kanununi zinavyoeleza kuwa taarifa yoyote ile itolewayo iwe na uthibitisho, namuomba Mhe. Mwakilishi atupe uthibitisho ili tuweze kujua kama kweli taarifa hizo ni za kweli. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe nafikiri hili suala tutafuata zile taratibu zetu baadae, ndipo tutakapokuja kushughulika nalo kama vile sheria na taratibu za humu katika Baraza zinavyoturuhusu.

Kwanza Mheshimiwa Mjumbe ametoa maelezo ambapo Mheshimiwa Mjumbe mwengine amehisi, kama kuna tatizo basi tuna taratibu zetu tutazifuata hizo na baadae tutakuja kuthibitisha haya kama ambavyo utaratibu wa Baraza unavyoturuhusu.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa na ombi kidogo kuhusu utaratibu labda Mhe. Mwanasheria Mkuu angetusaidia kwa sababu lile jambo lililozingumzwa na Mhe. Subeit Khamis Faki lilitolewa wakati wa Wizara ya Afya inajibu swali. Sasa na Mheshimiwa mwengine amesimama pia nae ni Naibu Waziri kwa kumpa heshima yake vile vile.

Sasa mimi nilikuwa najibu, swala liliulizwa wakati mimi najibu. Lakini sikujua masuala ya Bendera kupandishwa kushushwa na la pili pia sikujua kwa nini lilikuja kwenye swala la msingi la wizara ya Afya.

Sasa naomba muongozo wako Mhe. Mwenyekiti, ili Mheshimiwa nae isiwe amekatishwa kwa sababu yule mwengine alipewa haki ya kulizungumza na kulipongeza kuzungumza masuala ya kisiasa kwenye Wizara ya Afya.
Sasa na hili ningeomba sana Mheshimiwa nae apewe fursa ya kupatiwa nafasi lile ombi lake. Lakini naomba muongozo wako juu ya jambo hili kwa sababu akikatishwa tu bila ya kupewa fursa ya kujibiwa, mimi nitahisi unyonge kwa sababu Mjumbe mmoja atakuwa kapewa fursa, Mjumbe wa pili amenyimwa fursa hiyo. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, naomba muongozo wako.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe muongozo wangu nilikwisha kutoa kwamba tuangalie zile taratibu zetu na baadae tuone basi hili jambo lina ukweli

kiasi gani au lina utata kiasi gani. Baadae vyombo vya kiserikali vitakuja kutoa taarifa kwa mujibu wa taratibu zetu zilivyo. Ninachelea kutoa fursa kwa sababu hili suala ndio kwanza limekuja hapa sijui uhakika wake ukoje.

Sasa ni vizuri likafatiliwa ili taarifa itakayokuja hapa katika suala hili iwe ni taarifa ambayo ina umakini na ya uhakika kama ambavyo kanuni zetu za 59 zinavyotuongoza katika Baraza hili. Kwa sababu Kanuni inatutaka tusizungumze kitu ambacho hatuna uhakika nacho au hakuna umakini nacho katika Baraza hili.

Sasa ningeliomba Serikali kufatilia hili na baadae tuweze kupata taarifa kama zilivyo taratibu zetu nyengine. Naomba tuendelee na taratibu zetu baade taarifa kamili itakuja na wala ghofu isikuwepo, naomba tuendelee.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Hichi ni chomba cha wananchi kama alivyosema Mhe. Rais, ni ngome na taarifa zimetolewa nakuomba sana Mwenyekiti kabla serikali hajashughulikia suala hili Mheshimiwa aliyewasilisha taarifa hii angewasilisha kwa maandishi kwa sababu sasa hivi tunaelekea kwenye uchaguzi na viongozi wote wanahubiri amani na utulivu katika nchi yetu, na taarifa hii inaweza ikaleta kidogo machafuko.

Kwa hiyo, nakuomba sana Mhe. Mwenyekiti, kwamba ungeomba kabla serikali haijatoa taarifa yake kiongozi Mhe. Subeit Khamis Faki kwa kumtaja jina aliyewasilisha taarifa hii angewasilisha taarifa rasmi mezani kwako, ili tukaijadili na serikali ikaweza kutolea tamko kwa sababu hichi chombo kinasikilizwa na wengi na sasa hivi sauti hii imeshafika kwa wananchi, na inawezekana ikaonekana kwamba kuna tatizo hapo.

Kwa hiyo, nakuomba sana taarifa hii iwasilishwe mezani kwako ili tuweze kujadili na waliokuwa na ushahidi watatoa waliokuwa wanataka kuijadili, kuichangia wataichangia nakuomba sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Haya kama serikali kuna lolote tunaomba tupate, Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Nafikiri ulikwisha kutoa ufafanuzi mzuri ulieleza kwamba kwa sababu jambo hili liko kwenye kipindi cha masuala na majibu tumalizie masuala na majibu na kama kuna taarifa zozote basi ni baada ya masuala na majibu.

Alichokisema Mhe. Subeit Khamis Faki hata mimi asubuhi aliweza kunielezea na nikamwambia kwamba nitafatilia niweze kujua hali halisi ya yaliyotokea. Kwa hiyo, ni mambo yanaweza yakatokea katika nchi yetu jambo lolote lile jema na

zuri. Kwa hivyo, ni vizuri bado tupewe nafasi tuwasiliane na wahusika baadae tukipata taarifa yoyote tutaleta hapa ya zaida. Lakini wote wawili walikuwa na haki Mhe. Subeit Khamis Faki alieleza tuna utamaduni hapa unaponyanyuka na ukasema kabla hujauliza swali mara nyengine japo ni nje ya utaratibu wetu wa kikanuni, lakini mara nyingi tuna utamaduni wa kusema sema maneno kabla ya kuanza kuuliza maswali.

Ni vizuri niungane na Mhe. Mahmoud Thabit Kombo kwamba wakati huu tulikielekea uchaguzini ni vizuri lugha zetu zote ziwe inaelekea kwenye suala la kuhimiza amani na salama ya nchi yetu. Kwa vile Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo ana haki naye wa kutaka ufafanuzi huo kwa hiyo tusubiri mpaka hapo baadae kama kuna ufafanuzi tutaweza kutoa kwa sasa Mhe. Mwenyekiti, naomba tuendelee masuala na majibu.

Na. 71

Tatizo la Kilimo cha Umwagiliaji Maji

Mhe. Saleh Nassor Juma (Kny: Mhe. Jaku Hashim Ayoub) - Aliuliza:

Kilimo cha umwagiliaji maji katika bonde la Muyuni kimekwama kwa muda mrefu kutokana na tatizo la maji ya kisima kilihochimbwa kuonekana kuwa na maji chumvi. Na kwa kuwa viongozi wa jimbo wamechukua hatua ya kuondoa tatizo hilo;

a) Je, Serikali imechukua hatua gani kutafuta njia nyengine mbadala ya kupatikana maji kuendeleza kilimo hicho na inatoa kauli gani kwa wananchi ambao ndiyo waathirika wakubwa wa tatizo hilo.

b) Serikali inayowajibika ni ile inayofuatilia matatizo ya wananchi wake popote walipo iwe Mjini au Vijijini, kwa nini watendaji wa Wizara ya Kilimo wanaendelea kubaki maofisini huku wananchi wakikabiliwa na matatizo na hawajui kinachoendelea kama vile wakulima wa bonde la Muyuni.

c) Wizara inawaambia nini Mbunge na Mwakilishi wa jimbo hilo pamoja na wananchi wanaolitumia bonde hilo.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili - Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub swali lake kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Kilimo na Maliasili inaelewa matatizo ya wakulima wa bonde la Muyuni na mengineyo hasa ukitilia maanani masuala ya mabadiliko ya tabia ya nchi. Katika juhudi ya kutafuta tatizo hizo Wizara yangu ilibuni na kuandika miradi mitano ya ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji ukiwemo mradi wa Muyuni na kuwasilisha Ofisi ya Uratibu wa Miradi ya Fedha zinazotokana na msaada wa chakula *(Food Aid Counterpart Fund)* ya Dar es Salaam na kwa bahati nzuri kati ya miradi mitano mradi wa Muyuni ndiyo uliopata ufadhili.

Mhe. Mwenyekiti, katika kutekeleza mradi huu maji ya kutosha yanahitajika ili tupate maji ya kutosha ilibidi kichimbwe kisima kirefu. Kisima kirefu kilichochimbwa lakini kwa bahati mbaya maji yaliyopatikana ni ya chumvi ambayo hayafai kwa umwagiliaji.

Idara ya Umwagiliaji Maji ikishirikiana na wahandisi wa Mamlaka ya Maji (*ZAWA*) wamepima wingi wa maji katika visima vifupi viliopo karibu na eneo la mradi na kuona kiwango cha maji yaliyomo ni kidogo hayawezi kutosha kumwagilia.

Utafiti umeonesha kwamba kwa maumbile ya Muyuni kisima chochote cha kina kirefu kinachochimbwa kitakuwa na maji ya chumvi. Kwa mantiki hiyo umwagiliaji kwa kupitia maji ya kisima haiwezekani. Kwa hivyo, wajumbe wa Kamati Tendaji wa mradi Zanzibar walifika Muyuni kukiona kisima hicho na kuonana na wanajamii mnamo tarehe 29/04/2015, pia kikao cha pamoja na wataalamu kimefanyika huko Muyuni mnamo tarehe 4/05/2015, kwa kuelezea wakulima hatua iliyofikia pamoja na mawasiliano na Mhe. Mbunge wa jimbo hilo.

Mhe. Mwenyekiti, kilichofahamika kwenye suala hili uongozi wa jimbo umechukua hatua kuondoa tatizo hilo. Hatujui hatua gani iliyochukuliwa. Wizara tayari imewasilisha kwa Kamati ya Uongozi ripoti hii ambayo imeainisha pendekezo la uvunaji wa maji ya mvua ili kufanikisha mradi huu. Wizara inasubiri maamuzi ya Kamati kwa ajili ya utekelezaji.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana.

Kwa kuwa wananchi wa Jimbo la Muyuni katika vijiji vya Kitogani, Muungoni, Paje, Bwejuu, Jambiani na Pete wameekeza maisha yao pamoja na kujiongezea kipato katika sekta hii ya kilimo cha mpunga. Na kwa kuwa maeneo niliyoyataja haya ardhi kinakubali sana kilimo cha mpunga tatizo ni maji.

Na kwa kuwa Naibu Waziri amekiri pale kwamba visima vifupi maji yanayopatikana kwenye maeneo ya Pete na Jambiani hayatoshi, lakini

yanapatikana. Na kwa kuwa hivi karibuni mvua imenyesha nyingi na kusababisha mafuriko na maji kupotea baharini bila ya kutumika na baadae maji yakapotea ovyo ovyo katika bahari.

Je, Mhe. Mwenyekiti, ni lini Serikali itakamilisha huo mpango wake wa kuvuna maji ya mvua ambao maji hayo ya mvua yatahifadhiwa pamoja na kushirikiana na maji ya visima vidogo vilivyopo katika maeneo ya Pete na Kitogani pale, ili yaweze kuwasaidia wananchi hawa kuzalisha mpunga ambao unawasaidia wao kwa chakula pamoja na kujiongezea kipato kwa kuweza kuuza.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Saleh Nassor Juma swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi kwamba Mradi wa Kukusanya Maji ya Mvua katika eneo la Muyuni ambapo tulitegemea sana kwamba kuna mradi wa kuchimba kisima, ili tupate mradi huo wa umwagiliaji maji, lakini kutokana na hali kama nilivyosema maji yake ni ya chumvi.

Kwa hivyo, Kamati ambayo inahusika kwa sababu ule ni mradi ambao ulioletwa umeshirikishwa na hii Kamati. Hivyo hatuwezi kubadilisha mradi mpaka tupate maoni ya Kamati hii ili tuje tuweze kupata maoni yake ndipo tutakapoweza kubadilisha mradi.

Lakini watakaporudi na ripoti ambayo iliyopelekwa kuhusu taarifa ya pale ya Muyuni, hapo tutakapojua nini tufanye kuhusu kukusanya maji kukubalika mradi wetu huu wa kukusanya maji kutegemea kilimo cha uvunaji wa maji.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, na mimi ninashukuru sana asubuhi ya leo kuweza kunipa nikapata kuuliza swali la nyongeza kwa Mhe. Naibu Waziri pamoja na majibu yake mazuri.

Mhe. Mwenyekiti, mtoa hoja ameeleza ametaja Jambiani na wapi, lakini niseme kuwa Jambiani mpunga haulimwi, kuna bonde amelisahau ambalo la Pangeni, Kilombero. Mhe. Naibu Waziri unakumbuka kuna mradi *special* kati ya huko Cheju pamoja na Kilombero na Pangeni.

Je, Mhe. Mwenyekiti, mradi ule umefikia wapi hivi sasa na umekwama wapi, ili kuweza kupatikana maji haya ambayo yanayotakiwa sasa hivi kuendeleza kuvuna mpunga.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Makame Mshimba Mbarouk swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kuna mradi mkubwa; mradi wa Exim Bank. Mradi huu ndiyo uliokuwa upo maeneo ya Cheju na Kilombero na kwengine. (*Makofi*)

Mradi wa Cheju ni huu mradi ambao tayari upo katika sehemu ya kuchimbwa visima katika kutekeleza mradi huu, hivyo tupo katika hatua za uchimbaji wa visima.

Mradi wa Kilombero, nao mradi huu katika sehemu ambayo kwenye hiyo miradi mikubwa katika sehemu ya miradi ya kukusanya maji ya mvua ndiyo uliokuwepo huku Kilombero nao upo katika taratibu zake. Kwa hivyo, bado mradi huu upo katika taratibu na ukifikia wakati mradi huu utamalizika.

Mhe. Shadya Mohamed Suleiman: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwa kuwa wananchi wanakuwa na hamu ya maendeleo. Je, Mhe. Naibu Waziri ni lini Kamati itarejesha majibu hayo na hiyo Kamati Wajumbe wake wanatokea Wizara ya Kilimo au wanatokea wapi.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Naibu Spika, ahsante kwa ruhusa naomba kumjibu Mhe. Shadya Mohamed Suleiman kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, suala la kurejesha majibu kwa wajumbe hawa, siwezi kukwambia watarejesha lini. Hivi sasa ndiyo wamekwenda kupeleka hiyo taarifa. Kwa hivyo wakishamaliza shughuli zao bila shaka wakati wowote watarejesha majibu hayo.

Lakini kuhusu wajumbe wa Kamati hawatoki Wizara ya Kilimo. Wajumbe hawa ni wajumbe wawili wanatokea Wizara ya Fedha.

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe jana tulimaliza michango yetu na leo ilikuwa ni nafasi ya Mhe. Waziri ili aweze kuanza kujibu baadhi ya hoja, masuala pamoja na kutoa ufafanuzi wa mambo ambayo yaliyokuwa na Waheshimiwa Wajumbe na baadae tuweze kupitisha bajeti yake.

Kwa hivyo, nachukua fursa hii basi kumkaribisha Mhe. Waziri ili aendelee na utaratibu huo. (*Makofi*).

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Kazi na Utumishi wa Umma: Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote ninachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu Subuhana Wataalla kwa kutuamsha salama tukiwa na hali nzuri *alhamdulillahi*.

La pili, nichukue nafasi hii kuwashukuru sana Waheshimiwa wote waliopata nafasi ya kuchangia na wale ambao walipata nafasi ya kusikiliza, kwa michango yao, maelekezo yao na ninawaahidi kabisa kwamba nitayafanyia kazi vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, kabla sijaendelea naomba nichukue nafasi hii kutoa kama nasaha ndogo tu kwa Waheshimiwa wote waliokuwemo ndani. Kiumri wengi wamenishinda pengine inawezekana lakini kikazi *experience* ninasema kidogo *alhamdulillahi* ninayo; humu ndani Mawaziri ambao wazoefu ni Mhe. Abubakar Khamis Bakary, Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini na baadhi ya Mawaziri, Mhe. Ramadhan Abdalla Shabaan, Mhe. Ali Juma Shamuhuna, hao ni wazoefu na ni *very senior* kwangu mimi. (*Makofi*)

Sasa kidogo haya majukumu tuliyopewa hatukupendelewa ni Mwenyezi Mungu katupa. Sasa michango ilielekezwe katika kujenga zaidi kuliko kubomoa. Hapa si mahali pa kutengeneza siasa, hapa ni mahali pa kutengeneza maendeleo ya wananchi na jamii kwa jumla. Na ninashukuru sana asilimia ya wachangiaji wengi jana kwenye hotuba hii ambayo niliyoitoa ilikuwa na lengo la kuchangia zaidi. (*Makofi*)

Ninasema hata wale kwa bahati mbaya, mimi ninasema kwa bahati mbaya kwa sababu hawajapatapo kuchangia katika lugha ile hata siku moja. Mimi upande wangu nimewasamehe. Ninajua kwamba hawakuwa na nia mbaya, walikuwa na malengo yao wote na ninawatakia kheri *inshaallah* waendelee kuendelea na

shughuli za uongozi na Mwenyezi Mungu atawajaalia *inshaallah* tutakutana hapa baada ya Oktoba tukijaaliwa. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, majumuisho yangu haya sina nia ya kujibu hoja moja moja, nitajitahidi nijibu kwa ujumla na wale ambao walisema wataweka buti na mmoja ni Makamu Mwenyekiti wa ile Kamati ya Katiba na Sheria. (*Makofi*)

Sasa kilichonishangaza Mhe. Mwenyekiti, kwamba kwa niaba ya mwenyekiti mwalimu wetu ambaye ninamuheshimu sana Sheikh Suleiman Hemed Khamis aliwasilisha ripoti ile kwa niaba ya mwenyekiti. Mwenyekiti ana dharura tunajua, makamu mwenyekiti alikuwa na dharura zake, akasema bora nikae pembeni kwa sababu anatayarisha buti. Na ile buti kwa kule Makunduchi inaitwa mchonga, naye anatoka Jimbo la Chonga. Sasa nikaona haya mambo sasa kutoka Chonga na anataka kuizuia buti ile, ninasema mimi buti ile aah! haina haja kuzuiliwa kwa sasa hivi. Sheikh Abdalla Juma Abdalla wa Chonga tupo salama, sina wasi wasi. (*Makofi*)

Ninachosema ni kwamba Kamati ile tulipokaa nayo iliipongeza sana Wizara yetu *alhamdulillahi* na ninamshukuru sana Sheikh Suleiman alizungumza maneno mazuri kwenye Kamati na yeye ni mjumbe wa Kamati, makamu mwenyekiti ni mjumbe wa Kamati. Nilikuja kushangaa kidogo kwamba anakataa katika mambo yale ambayo tulikubaliana.

Sasa hata hivyo hakuwa na lengo baya ninaamini, alikuwa anachonga ukali tu. Lakini *alhamdulillahi* mimi sasa hivi nishapevuka, *experience* ninayo. Wale wazee wa Makunduchi waliokuja jana, kuna mtu kanitania kanimbia walipokuwepo asubuhi michango ilikuwa mizuri, walipoondoka tu michango ikaanza kutawanyika.

Sasa ninawaambia walikuja na mambo maalum wale, tulipoondoka mchana wakaniambia tunakuomba ujibu masuala uwe umetulia, usiwe na wasi wasi. Sisi zawadi yako ya kukupa mwezi wa Oktoba tunayo usiwe na wasi wasi. Kwa hivyo, walinipa moyo sana, *inshaallah* wameniombea Mungu mimi, lakini na mimi ninakuombeeni na nyinyi vile vile Mwenyezi Mungu atawajaalieni salama na amani *inshaallah*. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo, naomba kidogo nitumie fursa hii vile vile kulizungumza suala la ubaguzi ambalo limezungumzwa hapa. Hakuna jambo ambalo linanikera mimi rohoni mwangu tukichangia hotuba za bajeti hizi, tukisema jambo la ubaguzi kati ya Unguja na Pemba. Hivyo, tumbague nani na kwa madhumuni gani na kwa nini.

Mimi sina historia hiyo na nikianza kubagua na mimi mwenyewe nitajibagua, si munaniona nilivyo hivi. Lakini chama changu mimi hakijanibagua, Wazanzibari hawajanibagua mpaka leo, wala sijajengewa hoja kwa sababu huyu ni nani. Ninapata fursa zangu kwa mujibu wa taratibu za kisheria kwa mujibu wa Mwenyezi Mungu alivyojaalia. Hakuna suala la ubaguzi la Unguja na Pemba. Jamani wengine mashahidi hapa. (*Makofi*)

Sheikhe Suleiman Hemed simtolei mfano ni ushahidi kule Msuka Wingwi, kule kuna skuli inaitwa *Haroun Primary School*. Sasa kama kuna skuli inaitwa jina Haroun na ile kamati ina mchanganyiko wa vyama mbali mbali, wakanipa heshima ile na ukitaka ugomvi ukaseme lile jina libadilishwe, watakuja juu. (*Makofi*)

Pale ambapo Mhe. Mwenyekiti, Mwenyezi Mungu alinipa mtihani, *wallahi* waliondoka wazee wa Wingwi gari nzima kutoka Msuka wakenda Mkoani wakaingia kwenye meli, wakaingia kwenye boti wakafika mpaka Unguja na kufika nyumbani kwangu, ni gari nzima, wamekuja kunipa mkono wa pole na *alhamdulillah*, sisemi walichoniletea lakini kwa mwezi mzima sikununua chakula. (*Makofi*)

Sasa kama ingekuwa tuna itikadi za kibaguzi wananchi wale wangekuja? Mhe. Mwenyekiti, wakati ninakabidhiwa Wizara ya Elimu, mimi ninatoa historia kidogo tu tulielewe hili; wakati ninakabidhiwa Wizara ya Elimu kuna walimu walipata mitihani kabla ya hapo, walisimamishwa kazi, walifukuzwa kazi lakini nikasema kwamba sasa hivi uchaguzi umemalizika na mimi Mwenyezi Mungu kanijaalia nimekuwa ni Waziri sasa hivi. Tukatoa msamaha tukawarejesha kazini watu wote wale, kwa sababu mbali mbali, wala tena hatukutaka kujua sababu zile. (*Makofi*)

Kwa hivyo, ninakuombeni sana ndugu zangu Waheshimiwa suala hili la ubaguzi halijengi, ilifika hatua mpaka leo watu wanahoji bajeti zinatolewa kwa ubaguzi Unguja na Pemba. Mimi hapa nina takwimu Afisa Mdhamini wa Kazi, Utumishi; nimekaa Wizara ya Elimu miaka mingi, kwa hivyo ulimi hauna mfupa. Imepewa asilimia 79 ya bajeti na nyengine mpaka asilimia 53, asilimia 50 Idara nyengine. Sasa ni *number three*, ninadhani ni *number three* nyengine zimepata kwa sababu ya uzito wa majukumu yake. Lakini inapofika hatua tukasema tunaanza kubaguabagua si kweli na Pemba wanapata bahati kubwa sana. Kwa sababu kwenye kasma zao wanatiliwa moja kwa moja.

Kwa hivyo naomba sana tuepushe lugha hizi, tunadhalilishwa, tunabaguliwa, tunafanywa nini, hakuna jambo hilo jamani. Serikali hii ya Mapinduzi ya Zanzibar tokea wakati huo na hata sasa hivi na sasa hivi ndiyo zaidi chini ya uongozi wa Dkt. Ali Mohammed Shein suala hili jamani analikemea siku zote.

Tupendane, tushirikiane na tujenge nchi yetu. Baraza la Wawakilishi kiwe ni chombo ambacho kitatusaidia.

Mhe. Mwenyekiti, nisionekane natoa mhadhara leo sina nia hiyo, na kutaka pengine kuyafunika yale masuala ambayo nimeulizwa, nitayajibu yote *Inshaallah*. Suala la ubaguzi nimelizungumza.

Nataka nizungumze kwa ujumla suala la nyaraka. Waheshimiwa Wajumbe mmeuliza suala la nyaraka, nyaraka umuhimu wake serikali inajua. Kuna Mhe. Mjumbe alizungumza hapa kwamba serikali bado haijatambua umuhimu wa nyaraka. Hivi jamani, juhudi zote hizo zilizochukuliwa na serikali, bado leo watokezee watu waseme serikali haijatambua umuhimu wa nyaraka haiwezekani. Serikali hii ni yetu sote, hii ni serikali yenye mfumo wa Umoja wa Kitaifa unamlaumu nani na sote tumo ndani, tukifanikiwa tunafanikiwa sote na tukiharibikiwa tunaharibikiwa sote.

Mhe. Mwenyekiti, serikali imefanya juhudi kubwa, waziri mwenzangu aliyetangulia alifanya kazi kubwa na mimi nilipokwenda pale, wala sikwenda kuomba kwamba niletewe wizarani kwangu, kwa sababu watu wanafikiria kwamba hii nyaraka inakokwenda na mimi nakwenda huko huko. Mimi siifuati nyaraka, nyaraka inanifuata mimi baada ya maelekezo ya Mhe. Rais, wala sina *interest* yoyote kwenye nyaraka.

Tumeweka pale kamera 64 za *CCTV*, baada ya maelekezo na baada ya michango ya Waheshimiwa Wajumbe, Mhe. Abdalla Juma tuliweka kamera pale kwa kujenga hoja, zile ambazo mlizileta sisi tukaona zina umuhimu tuzitekeleze. Yule anayekaa pale sio malaika, mimi nilimwita ofisini kwangu Mhe. Mwenyekiti, nikamwambia na bahati nzuri ni mwanafunzi wangu, nikamwambia ndugu yangu wewe unakaa ndani eneo letu ni hatari pale, yanafanyika mambo na wewe utakuja kuhusishwa, akaniambia maalim mimi hata kesho niko tayari.

Hivi sasa taratibu za kumuhamisha zinafanywa, ili tuhakikishe nyumba ile haikaliwi tena na raia wote na tutafanya utaratibu eneo letu la Idara ya Nyaraka moja kwa moja liwe mikononi mwetu.

Kwa hivyo, nishamwita muhusika, tunafanyakazi lakini nyengine kimya kimya tu. Nitowe hadithi kidogo Mhe. Mwenyekiti. Kuna ndugu wawili walipotea walitoka Makunduchi, unajua zamani ukitoka Makunduchi kuja mjini unaaga siku mbili kabla au wiki nzima kabla, kwamba nakwenda mjini na kila unayemuona njiani unamsalimia *asalaam alaykum* kesho nakwenda mjini, hata kama humjui, kwa sababu ilikuwa tunu zamani kutoka Makunduchi kuja mjini.

Usiku kucha hulali unataka uamke upesi uwahi gari na gari za zamani zikitoka saa 10 au 11 na ikirudi saa 9, hiyo ndio ya mwisho tena.

Sasa ndugu wale walipokuja mjini wakazunguka zunguka maeneo ya Mji Mkongwe. *It is a true story,* na wako hai hao watu mpaka leo. Juzi nilimkumbusha mmoja, akaniambia wacha wewe tena umeshakuwa mtu mzima usinipe mifano hiyo.

Basi walipotea, kupotea kwa kule kwetu Makunduchi tunasema *kwaga*. Akamwambia mwenziwe unajua bwana... Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kidogo nizungumze kinyumbani na jana wazee walinipa baraka zote hapa, kwa hivyo nazungumza kidogo. Akamwambia bwana *twaga*, yaani tumepotea. Sasa yule mmoja akawa analia kwa makelele kweli kweli, eee! anapiga makelele mpaka watu wakawauliza mnalilia nini? Wakasema *twaga.*

Sasa watu wa mjini unawaambia *twaga* watafahamu wapi. Lakini yule ndugu yake ana busara sana, akamwambia kaka sikiliza, wewe unalia kwa sauti na mimi nalia lakini ndani kwa ndani, na kulia ndani kwa ndani kunauma zaidi. Tazama mtoto unayempenda sana ukimgomba hatoi sauti, analia ndani kwa ndani inavyomuuma ile.

Hata wewe nyumbani siku mambo yanapokuharibikia ukitolewa ukali kidogo, ile hamaki yako ya ndani kwa ndani inauma zaidi bora ungekuwa unamjibiza, akinyamaza kimya mtu kama amehamaki hakujibu basi anakera zaidi. Basi kwa bahati nzuri michango yenu sikuhamaki nitaijibu yote leo *Inshaallah*.

Kwa hivyo, tunafanya mambo mengi, *CCTV* kamera tayari tumeshaweka, hivi sasa nyaraka zote zinakuwa *digitalised* zinafanyiwa utaratibu katika *electronic* zinatengenezwa vizuri na kazi hii imeshafanyika vizuri sana.

Pia waheshimiwa wakalalamika kwamba hatuangalii maslahi. Serikali imepitisha posho maalum kwa wafanyakazi wa nyaraka kwa sababu ya kukithi shida wanazozipata pale, watalipwa posho maalum au wanalipwa posho maalum. Kuanzia Julai mwaka huu wa fedha wataanza kulipwa pesa zao zile zile, lakini wafanyakazi waliokuwa sio waaminifu hatuwaweki pale, kama tulivyofanya kwa wale ambao walihusika na kadhia hii tumewaondosha pale.

Mhe. Mwenyekiti, kuna tume iliundwa, serikali imechukua hatua gani. Kuna ujumbe maalum ulipelekwa Oman, humu ndani bahati nzuri wajumbe wawili walikuwemo na mjumbe mmoja kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania walikwenda mpaka Oman. Sasa subirini, serikali itaandaa ripoti maalum itawasilisha serikalini tutajua, baadae tutawapeni taarifa.

Ningependa mujuwe kwamba serikali imefanya juhudi imefuatilia mpaka Oman, tunalia lakini ndani kwa ndani sauti hamzisikii. Waheshimiwa Wajumbe, nawaombeni sana kwa suala hili la nyaraka tumelifanyia kazi kweli kweli na tutaendelea kulifanyia kazi hatuwezi kurudia makosa haya haya.

Mhe. Mwenyekiti, hivi karibuni nililetewa nakala kutoka taasisi moja ya *Commonwealth*, inasema; 1960 *to* 1961 kuna nyaraka zaidi ya 500 ziliibiwa duniani, miaka hiyo ya 60 na tumetakiwa tufuate taratibu za kisheria kwenda kuziomba zirejeshwe, kwa sababu ziko kwenye taasisi fulani kule zimewekwa miaka 60. Unakuja kumkamata Maalim Haroun kwa nyakara za yaliyotokea juzi. Kwa hivyo, ninachosema Mhe. Mwenyekiti, tuendeleeni na utaratibu wa kufikiri na kufahamu kwamba juhudi ya serikali inafanyika. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, migogoro ya wafanyakazi katika Hoteli ya Chavda waheshimiwa wamezungumzia kwa ukali sana. Jamani migogoro imetatuliwa, pesa wamelipwa watu wale pamoja na Hoteli ya *Resident.* Hapa Mhe. Mwenyekiti, nina orodha ya wafanyakazi wote wale wenye kazi hii wako 31 hawa, jumla ya milioni 42 wamelipwa na kama wapo ambao bado hawajaridhika hakuna matatizo, na wale waliokuwa hawakuridhika basi taarifa zao ziko kwenye kitengo chetu cha *DHU* na kesi yao itasikilizwa tarehe 4 Juni, wapo wamekuja na tunalifanyia kazi hilo.

Mhe. Mwenyekiti, ninachosema kwamba Hoteli ya Chavda, Hoteli ya *Resident* na hoteli nyengine zote. Hebu tutizame katika kile kitabu changu kuna eneo lile la migogoro iliyotatuliwa ni mingapi na mingapi iliyosawazishwa iliyopatiwa jawabu na iko mingine ambayo bado inaendelea. Naomba nisome kidogo taarifa ifuatayo Mhe. Mwenyekiti, ili tuweze kuelewa kidogo.

Mhe. Mwenyekiti, suala la... Samahani hapa kuna mchanganyiko kidogo wa hizi taarifa. Kuna suala zima la... Samahani hili nitalisema mwisho bora, maana yake linaungana na mambo mengine nitalisema mwisho, nimalize hili la migogoro ya wafanyakazi.

Mhe. Mwenyekiti, inapotokea migogoro kwenye mahoteli wafanyakazi wanadhalilishwa na kunyanyaswa. Nawaombeni Waheshimiwa Wajumbe washaurini waje pale wizarani. Mnakaa nayo mnamngoja mpaka waziri alete hotuba yake, halafu ndio tumkamate waziri. Kwa nini hatuwasiliani mapema, mbona mnapokuwa na matatizo mengine mnakuja tunakaa pamoja tunayasawazisha mapema. Hawa wafanyakazi na wananchi ni wetu sote.

Mhe. Mwenyekiti, suala la *E-Government*, limezungumzwa kwa ukali sana na wamefika watu kusema kwamba ni usanii, ni azma nzuri ya serikali. Naomba kwa ruhusa yako Mhe. Mwenyekiti, ninukuu hapa taarifa iliyowasilishwa na

Mwenyekiti, Mhe. Suleiman Hemed kwa niaba ya kamati, ambayo ndio inayosimamia wizara yetu. Sasa baadhi ya waheshimiwa wamelaumu sana kwamba ni usanii, hakuna kinachofanyika, udanganyifu mtupu. Hebu niisome hii ripoti kwa ruhusa yako ninukuu kidogo.

"Mhe. Spika, utekelezaji wa sera ya *E-Government* umefanikiwa kwa kiasi kikubwa, ambapo kamati ilielezwa kuwa taasisi za serikali 53 kwa upande wa Unguja zimeunganishwa na mradi wa *E-Government* na kwa upande wa Pemba matayarisho ya kuziunganisha taasisi za serikali yanaendelea, ambapo Kampuni ya *ZTE* kwa kushirikiana na Kampuni ya Zantel, wanafanya juhudi ya kukamilisha mipango hiyo ili zoezi hilo liweze kukamilika.

Mhe. Spika, nanukuu. Lengo kuu la huduma za serikali mtandao ni kumsaidia mwananchi kupunguza gharama za upatikanaji wa huduma na kuleta unafuu wa maisha ya mwananchi huyo. Hivyo, kama yangu inatarajia kuwa kuunganishwa huduma hiyo kwa baadhi ya taasisi za serikali kuna maanisha kuwa wananchi watanufaika kwa kiasi kikubwa na kurahisisha huduma za msingi wanazozihitaji".

Mhe. Mwenyekiti, nimetakiwa nithibitishe hizo taasisi 53 ni zipi. Mhe. Mwenyekiti, siwezi kuzisoma zote ni nyingi, hizi hapa 53 ninazo na kwa wale waheshimiwa ambao wanaotaka waipate nakala hii, basi *Inshaallah* nitawapatia tukijaaliwa nikimaliza majumuisho haya, ninayo taasisi 53. Sio kwamba tumeota tu tukasema, haiwezekani hatufanyi kazi kwa kubahatisha, tunafanya kwa kujiamini. Sasa mimi naiamini zaidi kamati yangu kuliko kitu chengine chochote, kwa sababu wao ndio waliokwenda wakaona ile hali.

Sasa tunapokuja hapa tukasema kwamba ni usanii mtupu, ni kuvunjana moyo, serikali *Inshaallah* hatutorudi nyuma tutaendelea kukamilisha zoezi letu.

Sasa kama alivyosema Mhe. Mahmoud jana, namshukuru sana kwa maelekezo yake, bahati mbaya sana Mhe. Hija Hassan uliondoka jana, lakini Mhe. Mahmoud alifungua darasa hapa la *E-Government* jana, umesikia ee! basi nimefurahi sana kama umesikia na ulipendekeza tufunguwe darasa la itikadi, lakini tutafungua na darasa *la E-Government* ili kuwafahamisha zaidi watu. Kwa hivyo, ninachosema kwamba tusivunjane moyo kipindi hiki, tujitahidi kutiana moyo *Phase II* ndio itakayoamua maendeleo yote hayo *Inshaallah*.

Baada ya hayo kwa upande wa *E-Government* sina cha kuongeza, na ukinitaka zaidi mheshimiwa mimi nipo *available*.

Mhe. Mwenyekiti, naomba radhi kidogo, unajua hamu ni kitu kibaya sana, kwa sababu nimekwenda kwenye kujibu hoja moja kwa moja hata wale waliochangia

sikuwataja. Lakini ndio jambo lolote ukifurahi. Mhe. Mwenyekiti, naomba kwa ruhusa yako niwatambuwe waliochangia hotuba yetu hii.

1. Mhe. Suleiman Hemed
2. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
3. Mhe. Marina Joel Thomas
4. Mhe. Mohammed Mbwana Hamad
5. Mhe. Saleh Nassor Juma
6. Mhe. Salma Mohammed Ali
7. Mhe. Ashura Sharif Ali
8. Mhe. Shadya Mohammed Suleiman
9. Mhe. Panya Ali Abdalla
10. Mhe. Ali Salum Haji
11. Mhe. Abdi Mosi Kombo
12. Mhe. Fatma Mbarouk Said
13. Mhe. Hija Hassan Hija
14. Mhe. Salma Mussa Bilal
15. Mhe. Abdalla Juma Abdalla
16. Mhe. Hamza Hassa Juma
17. Mhe. Naibu Waziri wa Afya

Mhe. Mwenyekiti, hawa ndio waliochangia kwa kusema. Waliochangia kwa maandishi ni:

1. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa
2. Mhe. Dk. Mussa Ali Hassan *(Makofi)*

Hao jumla yao Mhe. Mwenyekiti, ni 19 waliochangia hotuba ya Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Kazi na Utumishi wa Umma. Tunaendelea.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla alikuwa na suala la migogoro ya Zantel. Migogoro ya wafanyakazi wa Zantel haijesha inaendelea. Sasa hivi kesi yao iko *Industrial Court* ambayo iko chini ya makao makuu, kwa hivyo suala lao linashughulikiwa na *Industrial Court*.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu malimbikizo ya areas ya walimu. Mnajua tena nimekuwa waziri ninayehusika na mambo ya utumishi, tena maposho ya walimu na ya madaktari yote dhamana mimi, kwa hivyo nazuiliwa vifungu kwa sababu ya walimu hawajalipwa maposho yao.

Hii sio kazi ya wizara yangu jamani. Mimi kazi yangu ni kuletewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na Wizara ya Afya, Wizara ya Miundombinu na

Mawasiliano. Nikishaletewa nachukua juhudi ya kuzitafuta *data* zote, nikishazipata nampelekea bwana mkubwa mwenye pesa Waziri wa Fedha.

Waheshimiwa Wajumbe, kwanza nawaahidini kwamba yale malimbikizo yote tukijaaliwa ya walimu na wafanyakazi wengine, tayari serikali kwenye bajeti inayokuja imeshatenga fedha maalum, kwa ajili ya kuwalipa wote wale ambao wanadai haki zao. Sasa nimekuwa Waziri Kazi na Utumishi wa Umma, lakini sio waziri wa wizara zote.

Kweli utumishi kila mahali upo, lakini sasa mnaponiambia kwamba tunazuia shilingi kwa sababu walimu hawa bado hawajalipwa pesa zao, mnanionea mimi sihusiki huu mshahara wangu mnaonigaia mimi mtakaonizuilia mtaniumiza mimi na familia yangu, naomba msiuzuwie, niachieni nimalize keshokutwa mambo *Inshaallah* tumuombe Mwenyezi Mungu kwa mengine tena.

Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Mhe. Hamza Hassan Juma, kwa bahati mbaya hayupo, lakini namshukuru sana jana kachangia vizuri sana, kama kawaida yake anavyochangia alizungumza suala zima kwamba ukitaka kuongeza ajira kwa vijana wetu, ni kuanzisha utaratibu mzima wa kufungua *vocational training,* yaani mafunzo ya amali.

Nchi nyingi sasa hivi zimeendelea duniani kwa sababu ya mafunzo ya amali, kwa sababu pale unapata utaratibu na ufundi wa kutengeneza mambo mbali mbali. Kama uwashi, umeme na ujenzi ndio huo uwashi wenyewe ufundi umeme, lakini hata mambo ya utalii na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Pia ujasiriamali mdogo mdogo na mkubwa unaweza kupatikana kwa utaratibu wa mafunzo ya amali.

Mhe. Mwenyekiti, *Alhamdulillah* serikali imejitahidi imejenga vituo vya amali viwili vikubwa. Kimoja kiko pale Mkokotoni na chengine Vitongoji Pemba. Lakini pia kuna programu nyengine za ujenzi wa vituo vya mafunzo ya amali vinajengwa. Kwa bahati nzuri kimoja kitajengwa katika Jimbo la Makunduchi na kimoja kitajengwa Daya Mtambwe kule Pemba na mambo yote yameshakamilika.

Namshukuru Mwenyezi Mungu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali wametekeleza haya, wanaendelea na wanaendeleza juhudi za kuimarisha mafunzo ya amali kwa lengo la kuwasaidia vijana wetu. Nawatakia kila la heri na Mwenyezi Mungu *Inshaallah* awape nguvu zaidi ya kutekeleza majukumu yao.

Kwa hivyo, juhudi zimefanyika ni kweli. Mhe. Hamza Hassan Juma aliposema kwamba tuimarishe mafunzo ya amali. Mimi nakubali, nchi nyingi duniani zimeendelea kwa mafunzo haya ya amali, tunaita mafunzo ya amali na wenzetu

Bara hapo wanaita mafunzo ya ufundi. Taasisi nyingi sana za *VETA* zimepiga hatua kubwa, zinajiendesha. Ninachosema Mhe. Mwenyekiti, suala la ajira tusiamini kwamba serikali yoyote duniani ina uwezo wa kuwaajiri wananchi wake wote. Haiwezekani, hakuna uchumi ambao utaweza kusema kwamba leo tunaweza kuwaajiri wananchi wote, itakuwa ni miujiza! Mhe. Mwenyekiti, tutafurahi kusikia siku moja kwamba kila kijana anayemaliza skuli anapata ajira hapo hapo.

Mhe. Mwenyekiti, lakini hapa niipongeze ile hatua iliyopendekezwa na baadhi ya Waheshimiwa Wajumbe kwamba sekta binafsi ina nafasi kubwa sana ya kusaidia ajira.

Kwa hivyo, ninatoa wito Mhe. Mwenyekiti, tuendelee kuwahamasisha wananchi wetu wawekeze kwenye sekta binafsi hizi, ili waweze kuajiri. *Alhamdulillah* wamejitokeza wazalendo, Kiwanda cha Maziwa na hivi sasa kuna miradi mikubwa inaendelea Mwenyezi Mungu atujaalie salama *Inshaallah*.

Mhe. Mwenyekiti, Mwakilishi wa Jimbo la Matemwe anisamehe kidogo, alipendekeza akasema ajira Matemwe hawana. Mhe. Mwenyekiti, katika mahali ambapo kuna hoteli nyingi ni Matemwe. Sasa Mhe. Mwenyekiti, wale wafanyakazi wa pale kwenye hoteli zile asilimia kubwa ni vijana wenu wa pale pale. Sasa kama unataka ziongezwe tu wapatiwe na kwengine, hilo suala jengine, lakini eneo la Kiwengwa na Matemwe kuna hoteli nyingi na wafanyakazi ni wananchi wa pale pale.

Hata Mhe. Kazija Khamis Kona ninavyokumbuka alikuwa mfanyakazi wa hoteli hizo hizo pale wakati fulani. Sasa mheshimiwa ajira ndio hizo zinajitokeza.

Mhe. Mwenyekiti, jengine Waheshimiwa Wajumbe, tuwahamasishe wajiunge na vikundi vya ushirika. Wizara yetu ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto, kuna mifuko maalum ambayo imewekwa kwa ajili ya kuviwezesha vikundi hivyo. Mnakumbuka nyinyi wengine ni mashahidi nilipokuwa uwezeshaji pale, tulikusanyana katika wilaya zote tukatafuta fedha tukasaidiana kwa ajili ya kuvisaidia vikundi vyenu. Sasa zile pia ni ajira, zile takwimu zilizotolewa sio za kubahatisha.

Mhe. Hija Hassan Hija aliuliza swali, akasema nyie Waheshimiwa nikuulizeni nani ataweza kusema hapa kwamba katika Wilaya yake au katika jimbo lake kuna ajira kapata angalau ajira 20 au 30, sasa suala kama hilo unauliza Waheshimiwa hapa watakujibu vipi, kwa sababu wao hawashirikishwi kwenye utaratibu ule kuna utaratibu wa mambo ya utumishi Serikali ajira zinatangaziwa wanaomba.

Sasa ajira zilizotolewa na Serikali tumezisema kwenye sekta binafsi tumezisema na kama Mjumbe aliyezungumza suala hili anahitaji data zile takwimu zipo, Mhe. Hija nakuhakikishia ulikuwa karibu yangu sana mimi miaka yote ya nyuma, miaka hii miwili umeanza kunikimbia kimbia jitahidi urudi katika nafasi yako ile ile ya kuwa karibu na mimi utanufaika utapata mengi *inshaallah*.

Sasa alichosema kwamba kama kuna mtu atataja takwimu hizo Mhe. Hija niko tayari kukusaidia kupata takwimu utajua hatugawi watu kwa sababu ya kutoka Wilaya ya Kaskazini Pemba Kaskazini Unguja, hatugawi kiwilaya kwa sababu ya Upemba na Uunguja, hatugawi kazi kwa sababu hiyo hatuna hilo.

Mimi kuna kipindi fulani wakati nilipokuwa Waziri wa Elimu Shehe Mhe. Abubakar shahidi samahani lakini sikusemi kwa ubaya nakusema kwa uzuri siku zote na nitaendelea kukusema kwa uzuri *inshaallah*.

Lakini wakati fulani kulikuwa na kamati ile ya muwafaka nadhani yakaja malalamiko kwamba wanafunzi wanaokwenda vyuo vikuu wengi ni wa Unguja hawapo wanafunzi kutoka Pemba, Mheshimiwa alikusanya takwimu na ukitaka ushahidi sasa hivi nenda SUZA pale Naibu Waziri wa Elimu yupo yuko tayari kutusaidia kupata, tukatizame wanafunzi waliopo pale wangapi wanatoka Unguja wangapi wanatoka Pemba lakini hayo yatatusaidia nini. Mtu kama ana *qualifications* zake hata kama anakaa Chokocho, hata kama anatoka Makunduchi achukuliwe tu na akikosa hakoseshwi kwa sababu anatoka Pemba au anatoka Unguja.

Jamani hili tujitahidini sana hatugawi wafanyakazi wa utumishi hawa ajira zinapokuja, hatumchagui kwa sababu huyu anatoka wapi anakwenda wapi na hatufanyi na tutaadhibiwa na Mwenyezi Mungu tukifanya hivyo, Mungu atatusaidia *inshaallah.*

Mhe. Mwenyekiti, kuna pendekezo lilikuja hapa kwamba Waziri wewe basi hata vifaa vya kujikinga na usalama wa afya huwapi wafanyakazi wa Manispaa au wa Mawasiliano, jamani kweli Idara inayohusika na mambo ya usalama wa afya lakini mimi sina jukumu la kuwapa *gloves*, sina jukumu la kuwapa *rain boot*, sina jukumu la kuwapa *helmet* zile. Kila sekta, kila Wizara wahakikishe kuwa wao wanawapa wafanyakazi wao na wafanyakazi wasikubali kufanyishwa kazi kama hawana vifaa vya kujikinga, tujitahidi kila mmoja na jukumu lake jamani.

Mkiniambia mimi niwape *gloves* nitawapa wangapi, mkinambia niwape *rain boot* nitawapa wangapi. Kwa hivyo Waheshimiwa nakuombeni sana tushirikiane haya masuala ni yetu sote.

Maslahi nimeyazungumza watu wamependekeza kwamba kiwango cha mshahara kipandishwe lakini katika awamu ambayo imefanya marekebisho ya mshahara mara nyingi ni awamu ya Dkt. Ali Mohammed Shein. Kuna mara mbili tulifanya marekebisho ya mshahara kima cha chini tumesema. Na kwenye hotuba yangu nimesema na kila hali itakaporuhusu Serikali itakuwa tayari kufanya marekebisho hayo posho zimerekebishwa, hakuna *plural* ya posho posho ni posho tu tunakosea tukisema maposho.

Posho zimerekebishwa mara ngapi na hivi sasa tumetoa posho maalum kwa masekretari wa Mawaziri, kwa Makatibu Muhtasi wale, Madereva wote wale wa viongozi, madereva wa viongozi wote wanaofanya kazi katika maeneo nyeti, masjala za siri na nyenginezo tunawapa posho.

Tunatumia pesa nyingi jamani na Mungu atujaalie tupate pesa nyingi zaidi, ili inshaallah tuweze kunufaisha wananchi wetu, tuna nia ya kuwasaidia wananchi wetu na tutaendelea kuwasaidia tunaumwa sote, maana yake unapokuja ukasema mwananchi mnyonge jamani tunatoka huko sote sote ni wanyonge. Tusijenge dhana kwa wananchi kwamba kuna watetezi, kuna *class* ya watetezi na kuna *class* ya wakandamizaji. Serikali hii haimkandamizi mtu, sote ni wamoja jamani tushirikiane.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe naomba wale waliokuweko nje waitwe waingie ndani kwa sababu Mhe. Waziri anakaribia kumaliza na wanadhimu tusaidieni, ili tuweze kupata watu wa kutosha humu ndani.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma: Mhe. Mwenyekiti, umenisoma vizuri kwamba kweli nakaribia kumaliza mimi naomba nimalizie kwa kutoa shukurani zangu za dhati kwa wale wote waliochangia, kwa njia mbali mbali kwa staili zao tunashukuru na wala sina tatizo lolote na michango yoyote iliyotolewa kuna basi haina haja, lakini ninachosema Mhe. Mwenyekiti, niwashukuru wajumbe wote na Mwenyezi Mungu awabariki inshaallah Mwenyezi Mungu atujaalie, tuombe Mungu tumalize uchaguzi wetu kwa salama na amani ishaallah.

Baada ya kusema hayo sasa naomba kutoa hoja Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe sasa niwahoji wale wanaokubaliana na hoja wanyooshe mikono, wanaokataa. Wanaokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Baraza limejadili kuikabili hotuba ya bajeti ya Wizara ya Nchi Afisi ya Rais kazi na Utumishi wa Umma, sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Matumizi, ili kupitisha vifungu vya matumizi ya Wizara yangu.

KAMATI YA MATUMIZI

FUNGU V01 OFISI YA RAIS KAZI NA UTUMISHI WA UMMA

KIFUNGU E01 - OFISI YA RAIS KAZI NA UTUMISHI WA UMMA

Kifungu 06	Idara ya Usalama na Afya Kazini	Sh. 35,000,000
Kifungu 10	Idara ya Ajira	Sh. 26,000,000
Kifungu 11	Kamisheni ya Kazi	Sh.264,387,000
	Jumla Kuu	**Sh.325,387,000**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

KIFUNGU P01 -PROGRAM YA USIMAMIZI RASILIMALI WATU MIFUGO NA MIUNDO YA TAASISI

Kifungu S01	Maendeleo ya Rasilimali watu	Sh.345,691,000
Kifungu S02	Maendeleo ya Miundombinu na Mifumo ya taasisi	Sh.243,642,000
	Jumla ya Fungu	**Sh.589,333,000**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

KIFUNGU P02- PROGRAM KUU YA USIMAMIZI WA KUMBUKUMBU NA MAWASILIANO YA SERIKALI

Kifungu S01	Uhifadhi wa Nyaraka na Kumbu kumbu za Taifa	Sh364,050,000
Kifungu S02	Usimamizi na Undeshaji wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano	Sh583,804,000
	Jumla ya Fungu	**Sh.947,854,000**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

KIFUNGU P03 PROGRAM KUU YA URATIBU WA UANZISHAJI NA UPATIKANAJI WA AJIRA ZA STAHA

Kifungu S01	Utaribu wa Upatikanaji wa Ajira za Staha	Sh.117,232,000
	Juma ya Fungu	**Sh.117,232,000**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

KIFUNGU P04 PROGRAM KUU YA USIMAMIZI WA UTEKELEZAJI KWA SHERIA ZA KAZI

Kifungu S01 Program...

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru jana nilipochangia kwenye hoja hii ya ajira za staha kimataifa nilihoji kwamba Idara hii ya Kazi imekuwa ikifanya kazi ya kushirikiana na Mawakala wa ajira nje ya nchi, lakini Wazanzibari wanaopelekwa nje ya nchi wamekuwa wakikosa haki zao chini ya Idara hii nikatoa mfano nimeshuhudia kesi nyingi za Wazanzibari mikataba ambayo inakubaliana hapa Zanzibar na wanapofika nje ya Zanzibar mikataba ile inakuwa ni mingine.

Kwa maana ya kwamba Idara ya Kazi imekuwa ikiwatelekeza Wazanzibari na ushahidi wa hayo safari ya Kamati yangu ya Fedha ilipokwenda Dubai na Mheshimiwa Masoud na Marehemu Mheshimiwa Salmin Balozi wa Tanzania pale nchi za falme za kiarabu alithibitisha hivyo kwamba unafanyika uzembe Zanzibar na hatimae Wazanzibari wetu wanaokwenda nje ya nchi.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa Mjumbe twende kwenye hoja moja kwa moja, nini hoja yako?

Mhe. Hija Hassan Hija: Ndio nakuja ili Waziri afahamu nifafanue siwezi kusukuma tu halafu akasema sikufahamu, hata Balozi wa Tanzania pale Dubai alithibitisha kwamba Wazanzibari wanapofika kule wamekuwa wakitelekezwa hatimae wanakwenda ubalozini na kutaka nauli warudi kwao, hii ni udhaifu kwa Idara hii ya kazi. Sasa naomba fungu hili milioni mia nne na saba ni fedha nyingi kwa sababu hawana kazi ambayo wanaifanya na imebidi Wazanzibari walalamike, naomba ufafanuzi.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma: Mhe. Mwenyekiti, hili darasa itabidi tulifungue kweli jukumu la kupeleka wafanyakazi

wananchi kuweza kufanya kazi nje, sistahiki Idara ya Ajira, kuna taasisi maalum humu ndani wamo Wajumbe wawili wameshatangaza nia ya kufungua taasisi kama hizo za kupeleka wafanyakazi nje. Kuna wakati hapa Mhe. Mwenyekiti, Serikali iliwazuia kuwapeleka wananchi kwenda kufanya kazi nje Waheshimiwa mkawa wakali sana kwamba Serikali imezuia kutoa haki na fursa kwa wananchi wetu wanaokwenda kupata ajira nje, tulizuia kwa sababu ya hayo manyanyaso na mateso ambayo wanayapata wananchi wetu kule vijana wetu hasa wafanyakazi wa majumbani wanadhalilishwa sana, balozi kasema, ndio kasema sawa.

Kosa lile si la Wizara wala sio la Serikali wale ma-*agent* ambao wana jukumu la kuwapeleka vijana wale kwenda kufanya kazi ndio wenye majukumu ya kuhakikisha, kwanza sisi sasa hivi hatutoi kibali cha kwenda kufanya kazi nje kama hatujui ile taasisi inayofanya kazi kule inatambulikana na Serikali inaitambua.

Sasa tutatoaje wafanyakazi sisi Serikali tuwape ajira tuwapeleke nje kama tunashindwa kuwapa ajira hapa kutokana na matatizo mbali mbali. Kwa hivyo Mhe. Hija nakuomba ufahamu kwamba jukumu lile sila Idara ya Ajira, tuiachia Idara ya Ajira iendelee kuratibu masuala haya na ishirikiane na mawakala na Waheshimiwa hawa ambao waliniomba kwamba tuwaruhusu waendelee mmoja tushamruhusu na nina hakika na wa pili tutamruhusu tukijaaliwa.

Kwa hivyo tutulieni tutaratibu shughuli ambazo vizuri kwamba vijana wetu kama tutajitokeza sisi wenyewe humu ndani tuta-*create* ajira kama hizo ni vizuri zaidi kuliko kwenda kufanya kazi nje wanapata shida ni kweli, lakini si jukumu la Serikali kwamba ikalaumiwe Serikali mimi nakwenda huko huko nje hapo Dubai, Oman, Qatar na kwengineko tunakwenda na tunalalamikiwa hayo. Matokeo yake vijana wetu ni wakaidi kuna vijana kumi na moja kumi na mbili tunateremsha kwenye Oman Air. Hapa wanawake walikuwa wanakwenda kufanya kazi huko tukawateremsha kwenye ndege, kwa sababu hawana vibali na lazima Wizara ya Kazi ithibitishe, sasa matokeo yake kuna watu wanaojitokeza Mawakala wanachukua majukumu, wanachukua pesa nyingi kwa wananchi.

Natoa wito kwa wananchi wasikubali kurubuniwa kwa sababu matokeo yake ndio kama haya anayosema Mhe. Hija *you are right* lakini nakuhakikishia kwamba sio Serikali, sio Idara ya Ajira, naomba Mhe. Mwenyekiti, nimalizie hapo.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nadhani Mheshimiwa Waziri amenifahamu na ameeleza vizuri, hoja yangu ni kwamba bado nasema kwamba ni Serikali, Serikali imekasimu Baraka kwa Idara ya Ajira, wao ikiwa Mheshimiwa yeyote au kampuni yoyote inasema ni wakala wa ajira za nje mimi nakubaliana nae, lakini kabla ya kuja kuchukua hao wafanyakazi kampuni ile inakwenda Idara

ya Ajira, na mikataba inaonekana mimi nimeiona mikataba wanapofika hapa kwenye Idara yake. Mikataba inakuwa mingine na wanapofika nje ya nchi mikataba inabadilishwa.

Mtu wa kwangu Kiwani Pemba anapewa mkataba wa lugha ya kiingereza cha ndani bila ya msaada wa idara ya Ajira, kutafsiri na kuelekeza akifika kule anaambiwa hivyo sivyo ulivyoambiwa na nikwambieni Mhe. Mwenyekiti, mimi nimefuatilia kwa kina Idara ya Ajira inahusika mia kwa mia. Kwamba haiwapi ushirikiano kamili na hatimae wanalalamika.

Kwa hivyo tukubaliane Sio Waziri lakini Idara ya Ajira inahusika kikamilifu mimi mikataba nimeiona na mna baraka ya Idara yako, kwa nini wanawaruhusu watu kwenda kule bila ya taaluma na hatimae kule wanadhalilika watu wanarudishwa hapa. Kwa kweli hoja yangu Mwenyekiti ni kwamba milioni mia nne na saba kwa kuwapa watu wasiowajibika, ni nyingi zipunguzwe.

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimemfahamu vizuri sana Mhe. Hija Hassan Hija lakini vile vile nimemfahamu vizuri sana Mhe. Waziri, lakini nataka kwa heshima kiti chako na wewe uchukue tahadhari kubwa sana. Mhe. Hija Hassan Hija hoja yake haipo hapo anapozungumza Mhe. Hija Hassan Hija, amesimama kwenye kitungu P04. Ukisoma *activities* za P04 haizungumzii hiyo hoja ambayo Mhe. Hija Hassan Hija anayoieleza. Mhe. Hija Hassan hoja yake ipo kwenye kifungu P03 ambacho tumeshakipita. Nilikuwa nataka kutahadharisha tu kiti chako kiwe kinaelekeza kwamba hoja ambayo tumeshaipita sio pahala pake tena kuanza kuuliza maswali kwa sababu tumeshaipita.

Kwa hivyo hoja hiyo ambayo anaisema Mhe. Hija, kifungu cha P03, pesa zake ni milioni 117 na tushamaliza na hizi ni kidogo sana kuliko hizo pesa ambazo Mhe. Hija anazozizungumza milioni 400 ambazo hazihusiani na hii hoja ya Mhe. Hija. Kwa hivyo mimi naomba tu kwamba Mheshimiwa Kifungu cha Mhe. Hija, pesa ni kidogo tulizoziweka naruhusu tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Huu ndio uwanagenzi wa programu mpya, kwa sababu Mhe. Waziri ukiangalia kifungu ambacho unakizungumzia kuna suala zima la Uratibu wa Upatikanaji wa ajira za staha. Lakini Mhe. Hija aliposimama ni Usimamizi wa Viwango vya Kazi vya Kimataifa ya Majadiliano ya Pamoja. Sasa huu uwanagenzi wa hizi programu huu kidogo unatuchanganya, Lakini hebu tumsikilize Mhe. Hija Hassan Hija na yeye.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri wa Fedha, ndiye aliyoiandaa hii bajet na sikutaka kubishana na yeye. Lakini kama ni makosa ni makosa yangu mimi na Mhe. Haroun Ali Suleiman maana kajibu. (*Vicheko*)

Ninachosema kwamba ikiwa ni kifungu P03 kama alivyozungumza Mhe. Waziri wa fedha ajira za staha, wala sitaki nipingane na yeye. Itakuwa Wizara tayari hapo imepenya. Lakini hoja yangu ilikuwa nimeacha hapo kwa sababu nimeona kuna uratibu wa kazi za Kimataifa ambazo watu wanapelekwa Qatari, wanapelekwa Oman wanapelekwa sehemu nyengine. Lakini kama ni makosa sawa nakubaliana nayo. Lakini hoja yangu ni kwamba Idara hii isingestahiki kupewa pesa kiasi hicho kwa sababu haiwajibiki ipasavyo.

Labda Mhe. Waziri wa Nchi, kwa sababu labda mfumo mpya umetucheza labda anihakikishie tu kwamba lini atachukua hatua ili sasa utaratibu ule wa Wazanzibari wanaodhalilika kule nje ya nchi basi upungue. Mimi nimuombe labda atoe kauli angalau watendaji wake wasikie. Kwa sasa anithibitishie tu kwamba nimefatilia kwa kina, baadhi ya mikataba hadi idara yake inahusika kuwasukuma wale mawakala. Niwapongeze wale wenzangu walioanzisha nia njema ya kufanya mawakala waendelee lakini hili ni jambo muhimu sana. Ahsante Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimjibu lile suala lake kwamba anasema nimefanya makosa katika kumjibu. Sijafanya kosa mimi ni mwalimu, nyumbani mtoto anapokupiga picha ikawa mbaya unaambiwa usimwambie kama mbaya, mwambie nzuri, asante endelea. Sasa kauliza swali ningemu-*embarrass* nikamwambia kwamba kifungu alichotumia sicho. Nikaona nimjibu kwa faida yake yeye na wengine. (*Vicheko* na *Makofi*)

Kwa hivyo Mhe. suala hili tutalisimamia vizuri, tutaliendeleza ili kuhakikisha kwamba haya makosa madogo madogo hayafanyiki. Asante.

Kidungu P04 - Program ya Usimamizi wa Utekelezaji wa Sheria za Kazi

Kifungu S(01) Program ndogo ya Usimamizi wa Viwango vya Kazi vya Kitaifa na Majadiliano ya Pamoja.	Sh.279,830,000/=
Kifungu S(03) Program ndogo Juu ya Usimamizi wa Usalama na Afya, Kazini.	Sh. 128.002,000/=
Jumla ya Kifungu P04	**Sh. 407,832,000/=**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu zimepitishwa na Kamati yangu bila ya mabadiliko yoyote)

Kifungu P05 - Program ya Mipango na Utawala wa Kazi na Utumishi wa Umma

Kifungu (S01) Program ndogo ya Uongozi na Utawala	Sh. 933,071,000/=
Kifungu (S02) Program ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti	Sh. 990,702,000/=
Kifungu (S03) Program ndogo ya Kuratibu Shughuli za Kazi na Utumishi wa Umama Pemba.	Sh. 466,376,000/=
Jumla ya Kifungu P05 ni	Sh. **2,390,148,000/=**
Jumla Kuu ya Fungu E01	**Sh. 4,452,400,000/=**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu zimepitishwa na Kamati yangu bila ya mabadiliko yoyote)

KAMISHENI YA UTUMISHI

Kifungu P01- Program Kuu ya Usimamizi wa Mifungu ya Rasilimali watu Katika Utumishi wa Umma.

Kifungu (S01) Program ndogo ya Usimamizi wa Mifumo ya Usimamizi wa Rasilimali Watu Katika Uchumishi wa Umma	Sh. 341,506,000/=
Jumla ya Kifungu P01	**Sh.341,506,000/=**

Kifungu P02 - Program Kuu ya Utawala na Uendeshaji Kamisheni ya Utumishi wa Umma.

Kifungu (S01) Program Ndogo ya Utawala na Uendeshaji Kamisheni ya Utumishi wa Umma	Sh. 381,894,000/=
Jumla ya Kifungu P02	Sh.381,894,000/=
Jumla ya Kuu	**Sh. 723,400,000/=**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu zimepitishwa na Kamati yangu bila ya mabadiliko yoyote)

TUME YA UTUMISHI WA UMMA

Kifungu P01 - Program Kuu ya Usimamizi wa Watumishi Serikalini

Kifungu (S01) Program ndogo ya Usimamizi, Haki na Nidhamu kwa Watumishi wa Umma.

Mhe. Hija Hassam Hija: Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu hapa Usimamizi wa Haki, Nidhamu kwa Watumishi wa Serikali, bado naendelea kushikilia hoja yangu kwamba serikali najua imetenga bilioni 15 kwa ajili ya kuweka haki mbali mbali kwa wafanyakazi. Lakini nilimuhoji Mhe. Waziri jana kwamba ni kwa nini miaka minne ya serikali hii iliacha kutimiza haki za wafanyakazi ipasavyo na nikatoa mfano.

Malimbikizo ya nyongeza ya walimu, wapo walimu waliopewa nyongeza yao 2012 lakini kuna walimu hadi hii leo nyongeza yao hawajaipata. Ningetaka ufafanuzi je, wakati fedha hii itakapoingizwa hawa watu watapewa *error* na kwa nini fedha hii isilipwe kabisa kabla ya nyongeza hiyo. Kwa sababu wamesafa zaidi ya miaka minne kwa ajili ya mapato yao.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma: Mhe. Mwenyekiti, maana yake Mhe. Hija Hassan wakati nikijibu zile hoja zangu awe katulia ana nisikiliza. Suala hili wakati nalijibu alikuwa anazungumza Mheshimiwa fulani humu ndani, mimi nilikuwa namtizama. Na nimeshalijibu kwamba masuala yanayohusiana na walimu, madaktari ni Wizara husika ndizo zenye mamlaka hayo. Na nimesema kwamba serikali tayari imetenga fedha kwa ajili ya kuwalipa hao wote ambao wanadai mambo yao na kuna fungu maalum ambalo limetengwa. Nilisema hapa Mhe. Mwenyekiti.

Sasa tatizo ile *concentration* yetu hapa inakuwa haipo tunafanya mengine kwanza kwa lengo la kwamba tuje tupite miguu. Basi hamna matatizo Mheshimiwa nimesimama nakupa heshima hiyo na nakujibu kwamba hilo swali nimeshalijibu na tayari haki zao watapatiwa kwa mujibu wa sheria.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, napenda nikuhakikishie kwamba mimi nipo makini sana, niko makini zaidi ya makini. Naelewa kwamba walimu wapo Wizara ya Elimu, madaktari wapo kwenye Wizara ya Afya, lakini yeye ndiye mratibu Mkuu wa haki za wafanyakazi. Kwa maana hiyo ndiyo maana hawaachiwi tu wapandishe mishahara kule Wizara ya Elimu, yeye ndiyo anaye-*control* ndio mama wa ajira. Sasa akiwasukumia Wizara ya Elimu ambaokuwa wameshindwa kuwapa haki zao, yeye ndiye mama. Bado nataka ufafanuzi ni kwa nini taasisi yake imeshindwa kuwasukuma hao ambao yeye anawajuwa wazitoe haki za walimu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma: Mhe. Mwenyekiti, jukumu la Wizara ya Kazi na Utumishi tumeshaletewa, sisi jukumu letu ni kupeleka Wizara ya Fedha. Kwa hivyo na Wizara ya Fedha wameshatuthibitishia na kwenye hotuba yake Mhe. Waziri kalisema wazi wazi kwenye hotuba yake ya bajeti ya Serikali, kwamba kuna malimbikizo haya yote

ambayo tayari tumewasilishiwa kutokana na sekta mbali mbali, tutachukua hatua na Tuna Bajeti maalum imetengwa kwa ajili ya kuwalipa.

Sasa jukumu langu mimi kama Waziri Mhe. Hija Hassan *Inshaallah* Mwenyezi Mungu siku moja atakujaalia na wewe utakuwa Waziri. Ukishakupata uwaziri jukumu lako kuna mambo yatakuhusu wewe moja kwa moja na kuna mambo utakuwa unayaratibu kwa niaba ya Wizara nyengine, itatokezea tu. Sasa ili uwe Waziri mzuri *Inshaallah* uwe msikivu kama Mwalimu Harouna anavyowasikiliza watu.

Ninachosema kwamba Mheshimiwa kitu hichi tayari nimeshakitolea maelezo na tayari maombi yameletwa na mimi nimechukua hatua nimeshampelekea mweye pesa na mwenye pesa katoa tamko hapa kwamba *Inshaallah* suala hilo tukijaaliwa tutalichukulia hatua kadri hali itakavyokuwa inakwenda. Tayari fungu limetengwa kwa ajili ya kuwalipa walimu na wengine wote ambao wanadai malimbikizo yao. Ahsante Mheshimiwa.

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Mwenyekiti, nataka nisisitize kiti chako PBB hatupigi buti tu kama vile tulivyozowea. Narudia PBB hatupigi buti kama tulivyozowea. Hii programu ambayo ndugu yangu Mhe. Hija Hassan ameisimamisha haihusiani kabisa na hoja ambayo ameitoa. Ukiisoma, ndio kwa maana nimesema kwamba kila mwakilishi anapotaka kupiga buti katika eneo lolote lile aangalie *activities* zinasema nini.

Ukiisoma hii *activities* ya hicho kifungu ambacho amekisimamia Mhe. Hija hakizungumzi hivyo. Kwa hivyo mimi nasema Mhe. Haroun ameshasaidia kutoa ufafanuzi. Lakini ingekuwa mimi nakaa kwenye kiti chako ningezuia kwa sababu hapa haizungumzii masuala hayo. Sasa mimi nasema kwamba hoja hiyo hapa haipo, tusubiri kwenye hoja tutapata maelekezo.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri kama vile nilivyosema mwanzo bado Wajumbe wa Baraza hili ni wanagenzi na mambo hayo. Haya mambo pamoja na *activities* lakini kuna vitu vinachanganya bado. Kwa sababu eneo lenyewe linasema Usimamizi wa Watumishi Serikalini, lakini ukiteremka chini unapata Usimamizi, Haki na Nidhamu kwa Watumishi Serikalini ndipo maana mjumbe akaona, kwamba hili ni eneo husika kwa sababu na mimi nilipo sina *activities* nimekubaliana na hoja yake kuona kwamba hiyo hoja yake ilikuwa ni sahihi.

Kwa sababu kwamba wewe mwenzetu una *activities* hapo na umeweza kupambanua yale masuala huu ni uwanagenzi wa programu zetu mpya, na *Inshaallah* kila siku zikenda mbele watu watazidi kusoma zaidi na wataelewa zaidi na watakuwa wanaelekeza vitu kwa mujibu wa taratibu na sheria zilivyo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, tungependa sana kuheshimu sana kiti chako, tukiwa serikali, lakini sasa naona wewe sasa umekuwa ndio mtoa hoja badala ya kuongoza kiti.(*Makofi*)

Sasa Mhe. Waziri wa Fedha, amejaribu sana kukupa indhari kwamba kiti chako kiwe makini sana katika masuala haya. Programu ambayo ameiulizia hoja ndugu yangu Mhe. Hija Hassan Hija inasema Usimamizi Haki na Nidhamu kwa Watumishi wa Serikali. Hii programu inahusu taasisi ambayo inasimamia hivi kwa ajili ya shughuli za kiutawala, hapana fungu hapa la posho.

Jengine ambalo ningependa niliseme kwenye Baraza lako Tukufu kwamba pamoja na Wizara hii kuhusika na kutoa taarifa au idhini, hawa hawatoi idhini kwanza.

Hii Tume ya Utumishi kazi yake ni kusimamia Sera ya hizo haki na nidhamu za wafanyakazi. Maana hapa tupo Tume ya Utumishi Serikalini, tungekuwa Idara ya Utumishi na Maslahi ya Watumishi ndipo hasa Mhe. Hija angeweza kuzungumzia hilo analolizungumza. Kwa sababu yenyewe hiyo ndiyo ambayo inapokea *request* au maombi kutoka taasisi husika.

Kwa mfano kama anavyosema Mhe. Hija Hassan taasisi husika kwa mujibu wa maelezo yake ni Wizara ya Elimu, Wizara ya Afya, ambayo kuna malimbikizo ya maposho. Kwa hivyo Katibu Mkuu angepeleka Ofisi Kuu ya Utumishi, Idara ya Utumishi maslahi ya Watumishi ndio sasa ingepeleka *request* Wizara ya Fedha, hapa sipo, ndiyo maana yake hiyo. Pamoja na kwamba hawa wanasimamia Sera kwa jumla, kusimamia hizo haki.

Kwa hiyo mimi naomba kwanza lieleweke hilo. Lakini pia hata pesa zikitengwa wanaowajibu kupeleka maombi ni taasisi husika, yaani Wizara ya Elimu na Wizara ya Afya ipeleke kwanza maombi na wao ndipo wapeleke Wizara ya Fedha. Sasa mimi ningemuomba tu ndugu yangu Mhe. Hija Hassan kwamba hiki kifungu akiachie. Pamoja na kwamba tumeshatoa ufafanuzi na pamoja kwamba hizo pesa zipo, lakini na Wizara zenyewe ziwe zina-*request* Wizara ya Utumishi ili Wizara ya Utumishi wawapelekee Wizara ya Fedha bila ya wao kutengeneza vocha huko zinazohusiana na masuala ya mapoto na mengineyo, Wizara ya Utumishi hawawezi kufanya hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, asante sana.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, mimi nakiri kwamba hili jambo ni jipya, lakini pamoja na upya wake Mawaziri wasituzonge. Mimi natambua

kwamba wale walimu wasingedai maposho yao. Natambua, kaka angu Waziri wa Fedha na anaweza akanisuta kama si kweli. Fedha amewatiliwa kwa wakati, hutegemea vipaumbele tu vya Wizara yenyewe, natambua. Lakini Waziri na Wizara husika ya Utumishi wa Umma ni ya Mhe. Harouna. Ilivyokuwa Wizara Afya imeshindwa kwa uzembe wake kwa udhaibu wao, Wizara ya Elimu imeshindwa kwa udhaibu wao, nani wa kulaumiwa? Ni mama.

Mama wa Wizara hizi zote za Utumishi na Sekta za Utumishi ni Wizara ya Mhe. Harouna. Nakusudia kumwambia kwamba hao unaowapelekea pesa kupitia Wizara ya Fedha hayo ndio matendo yao. Sasa ukinambia mimi niwaachie hawa ambao ndio wajibu wao, mimi ukinambia Sera, Mipango, maana yake ndio utawala wenyewe huo. Na hapa ndio pa kukukamata hasa. Kwa hivyo Wizara hii ya Utumishi wa Umma chini ya Idara hii kwa sababu ndiyo yenye kusimamia Sera na Mipango na Utawala wa Sekta ya Ajira. Ningepasa niseme kwamba wao ndio wanaopaswa kusimamia hili jambo kuwasukuma hao kama vile ambavyo wakitaka kuongeza mshahara hawaongezi mpaka wapate idhini yao. Ni kwa nini mshahara kuongezwa mpaka ipatikane idhini yao lakini kutoa haki wachukue wale kule, Mhe. Mwenyekiti, jambo ni jipya lakini hawa ndio wenye haki ya kusimamia. Fedha inapelekwa Wizarani, vipa umbele vya wizara husika havitumiki, hatimaye jukumu linakuja kwa watumishi.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, mimi nasema kwamba kuachia si tatizo lakini wizara hii ya Mhe. Haroun, lazima isimamie haki za wafanyakazi, wakiachiwa wale Wizara husika hawaangalii vipa umbele vya wafanyakazi wao na ndio malalamiko haya yaliyopo. Mimi ninatambua Wizara ya Fedha haina tatizo la fedha, mfano Wizara ya Elimu fedha walipewa lakini kipaumbele hakikuzingatiwa. Na ili kuwa fedha walipewa ndio maana walimu mwaka 2012 wakalipwa Unguja. Kwa hivyo, bado Mhe. Mwenyekiti, ninasisitiza kwamba Wizara ya Mhe. Haroun, ndio wizara husika isimamie lazima iongoze na isimamie haki za wafanyakazi.

Mhe. Mwenyekiti: *Inshaallah* Serikali imesikia.

Mhe. Hija Hassan Hija: Si kusikia tu na kujibu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma: Ndio wajibu wa wizara yangu kusimamia, kuhakikisha kwamba haki ya wafanyakazi inapatikana pale ambapo hakutendewa haki ana wajibu wa kulalamika na kuleta. Kwa hivyo, *Inshaallah* tukijaaliwa ninashukuru katika *Job description* yangu kaikumbusha tu tutaendelea kuyafanya hayo *Inshaallah*.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, mimi ningeomba ufafanuzi wako, kwa kuwa Mhe. Waziri wa Fedha ndio mwenye *new programme*

hii ya *PBB* na wewe unakuwa unanukuu hapo kitabu chako ili na sisi kutupa ufafanuzi. Hapa ninajiuliza *which* is *correct?* Nani atakuwa ni zaidi kati ya wewe na yeye ili tuweze kwenda vizuri kama anavyotaka kutuelimisha Mhe. Waziri ili na sisi wajumbe tusichanganyikiwe.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Mjumbe, Waziri wa Fedha, ametukumbusha na sisi hapa tulipo tupo na vijana wetu ambao wanatuelekeza na kutuongoza, kwa hivyo, kiti kishatoa maelekezo na kishatoa muongozo tunasema kwamba tunaendelea na utaratibu na haya mambo yamekwisha kuwekwa sawa.

Kifungu P01 Programu Kuu ya Usimamizi wa Utumishi wa Serikalini

Kijifungu S01	Programu ndogo ya Usimamizi Haki na Nidhamu kwaWatumishi Serikalini	Sh.182,266,000
Kijifungu S02	Usimamizi wa Uajiri wa Watumishi wapya Serikalini	Sh. 89,660,000
Jumla ya kifungu		**Sh. 271,956,000**
Kifungu P02	**Programu ya Utawala na Uendeshaji wa Tume ya Utumishi Serikalini**	Sh.194,144,000
Kijifungu SO1	Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji wa Tume ya Utumishi Serikalini	Sh.194,144,000
Jumla Kuu		**Sh.466,100,000**

(Baraza linarudia)

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma: Mhe. Mwenyekiti, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha Makadirio ya Fedha ya Wizara yangu bila ya mabadiliko sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza liyakubali makadirio hayo.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora kwa mwaka wa Fedha 2015/2016

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Ikulu na Utawala Bora: Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako Tukufu likae kama Kamati kwa madhumuni ya kupokea, kujadili na kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya kazi za kawaida na kazi za maendeleo ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mwaka wa fedha wa 2015/2016.

Mhe. Spika, kwanza kabisa naomba kuchukua fursa hii adhimu kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehma kwa kutujaalia kukutana hapa tukiwa na afya njema na furaha. Naomba kutoa pole kwa wale wote walioathirika na mvua kubwa za Masika pamoja na upepo mkali. Namuomba Mwenyezi Mungu atuzidishie Baraka na neema katika nchi yetu na aendelee kutujaalia Amani na Utulivu.

Mhe. Spika, nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein kwa umahiri wake mkubwa katika kuiongoza nchi yetu. Chini ya uongozi wake, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imetekeleza kwa vitendo ahadi alizozitoa kwa wananchi wakati wa Kampeni ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010 kama zilivyoainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2010.

Mhe. Spika, mafanikio yaliyopatikana chini ya uongozi wake yameiwezesha nchi yetu kuendelea kuwa ya amani, utulivu na mshikamano mkubwa.Aidha, nachukua nafasi hii kuwapongeza kwanza, Mheshimiwa Maalim Seif Sharif Hamad, Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar na Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar kwa namna ambavyo wamekuwa wakimsaidia Mheshimiwa Rais katika kusimamia na kuongoza shughuli zote za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Spika, kwa namna ya pekee naomba nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambae ifikapo Oktoba, mwaka huu atakuwa anakamilisha Kikatiba muda wa vipindi viwili vya Uongozi wake akiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Spika, katika kipindi cha miaka kumi ya uongozi wake, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeendelea kuwa ni nchi yenye kujivunia kimaendeleo na inayoheshimika ndani na nje ya Afrika Mashariki. Kuendelea kuheshimika kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kumetokana na hekima, busara, uzoefu wa uongozi pamoja na uweledi wake katika kusimamia masuala mbali mbali ya

Kitaifa na Kimataifa. Naomba nitumie fursa hii kumtakia afya njema na maisha marefu. Ni matumaini yangu kuwa bado tutaendelea kushirikiana naye kwa kuchota falsafa zake katika kuiongoza nchi yetu hata baada ya kustaafu kwake.

Mhe. Spika, katika kuhakikisha kuwa nchi yetu inakuwa na mfumo imara wa kujiongoza, Serikali zetu mbili zimesimamia utaratibu wa kihistoria wa kuandika Katiba mpya. Utaratibu huu uliwashirikisha makundi mbali mbali ya Watanzania ambao walitoa maoni yao mbele ya Tume ya Mabadiliko ya Katiba. Vile vile, kuliundwa Bunge la kutunga Katiba ambalo hatimae lilitoa Katiba inayopendekezwa. Ni imani yangu kwamba Watanzania wote wataitumia haki yao ya msingi ya kuipigia kura Katiba inayopendekezwa wakati muda utakapofika.

Mhe. Spika, naomba kuchukua fursa hii kuwapongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa umahiri mkubwa na ukomavu wa kisiasa waliouonyesha katika kusimamia ipasavyo mpango wa mabadiliko ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hatua hii ambayo itaiwezesha Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa na Katiba mpya iliyotungwa kwa kuzingatia maoni ya Watanzania wenyewe, imefungua ukurasa mpya wa kuendelea kuimarisha demokrasia nchini.

Mhe. Spika, sambamba na hilo naomba kutumia fursa hii kutoa wito kwa Wazanzibari na Watanzania wote kwa ujumla kujitokeza kwa wingi katika kura ya maoni na kuipigia kura ya ‘NDIYO’ kwa Katiba Inayopendekezwa inayolenga kupata ufumbuzi wa kudumu wa hoja za Muungano.

Mhe. Spika, nawasilisha hotuba hii wakati ambapo Baraza letu linakaribia kukamilisha miaka mitano, muda wa muhula wake wa Kikatiba. Nitakuwa sijatenda haki kama sitokushukuru na kutoa pongezi kwako wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wa Baraza kwa kuwa makini na wavumilivu katika kuliongoza Baraza letu kwa kipindi chote cha miaka mitano. Baraza la Wawakilishi limepata heshima kubwa chini ya uongozi wako. Wananchi na wapiga kura wetu wamehamasika sana katika kufuatilia mijadala na kufahamu kinachoendelea ndani ya Baraza letu. Waheshimiwa Wawakilishi nao wameitumia ipasavyo haki yao ya Kikatiba ya kusimamia utendaji wa Serikali na kukosoa pale panapohitajika. Nawapongeza Waheshimiwa Wawakilishi wote kwa kuweza kutumia vyema haki yao hiyo.

Mhe. Spika, kabla ya kumaliza utangulizi wangu, kwa heshima kubwa naomba kuipongeza Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ikiongozwa na Mwenyekiti, Mhe. Hamza Hassan

Juma, Mwakilishi wa Jimbo la Kwamtipura, Makamu Mwenyekiti, Mhe. Saleh Nassor Juma, Mwakilishi wa Jimbo la Wawi na Waheshimiwa Wajumbe wote wa Kamati, kwa ushauri na maelekezo yao makini waliokuwa wakitupa katika kipindi chote hiki. Mimi binafsi na watendaji wote tunafarajika sana kuwa nao na kushirikiana nao vizuri katika utekelezaji wa kazi zetu.

Mhe. Spika, naomba nitumie nafasi hii pia kutoa shukurani zangu za dhati kwa Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi inayosimamia Hesabu za Serikali chini ya Mwenyekiti wake Mhe. Omar Ali Shehe, Mwakilishi wa Jimbo la Chake Chake na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Fatma Mbarouk Said Mwakilishi wa Jimbo la Amani na Waheshimiwa Wajumbe wote wa Kamati kwa kuendelea kuisimamia nidhamu ya matumizi ya fedha za Umma. Katika kipindi chao wamekuwa makini katika kuikosoa, kuielekeza, kuishauri na kuisimamia Serikali ipasavyo.

Mhe. Spika, miaka mitano ni mingi kwa maisha ya binadamu. Naomba kutoa pole kwa Waheshimiwa wote tuliokuwa nao Barazani kwa miaka mitano iliyopita ambayo tunaikamilisha hivi sasa ambapo hivi sasa wameshatangulia mbele ya haki. Mungu awaweke mahali pema peponi, *Amin*.

Mhe. Spika, mwanzoni mwa mwezi wa Mei, mwaka huu nchi yetu imepata maafa yaliyosababishwa na mvua kubwa iliyonyesha kwa zaidi ya saa 48 mfululizo. Mvua hizo zimeathiri miundombinu, makaazi na baadhi ya ndugu zetu kupoteza maisha. Naomba kutoa mkono wangu wa pole kwa wananchi waliopoteza jamaa zao na waliopatwa na maafa ya kuingiliwa na maji katika nyumba zao. Namuomba Mwenyezi Mungu awape moyo wa subira katika kipindi hiki kigumu huku Serikali ikiendelea kutoa misaada kwa wahusika. Nawaomba wananchi wachukue tahadhari za kiusalama hasa wale wanaoishi sehemu za mabondeni na maeneo ambayo mara nyingi huathiriwa na maji. Natoa wito kwetu sote kuhifadhi mazingira yetu na kuacha kabisa tabia ya kujenga kiholela bila ya mpango hasa mabondeni, kwenye njia za maji na msimoruhusiwa kisheria.

B: MAJUKUMU YA OFISI YA RAIS NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI

Mhe. Spika, kulingana na muundo uliopo, Ofisi hii inatekeleza majukumu yafuatayo:-

i. Kusimamia shughuli za Mheshimiwa Rais na kuendeleza taswira nzuri mbele ya jamii;

ii. Kusimamia mambo yanayohusu uendeshaji wa shughuli za Baraza la Mapinduzi;

iii. Kusimamia maendeleo ya uchumi wa nchi na kuratibu utekelezaji wa Dira 2020, MKUZA,

Malengo ya Milenia na Mpango wa Ustawi wa Jamii (R4P);

iv. Kuratibu ushirikiano wa kimataifa na uratibu wa Wazanzibari Wanaoishi Nchi za Nje (Diaspora);

v. Kusimamia utekelezaji wa shughuli za Ofisi ya Usalama wa Serikali (GSO);

vi. Kufanya ukaguzi wa hesabu za Wizara za Serikali na Taasisi zake zote; na

vii. Kuratibu utekelezaji wa misingi ya Utawala Bora na haki za binaadamu ikiwa ni pamoja na kusimamia maadili ya viongozi na kuzuia rushwa.

C: MAFANIKIO YA KIPINDI CHA MIAKA MITANO YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA OFISI YA RAIS NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI

Mhe. Spika, miongoni mwa agenda kuu za Kitaifa zilizopewa kipaumbele na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Awamu ya Saba ni pamoja na kuimarisha Misingi ya Utawala Bora kuanzia ngazi ya chini ya Shehia hadi ngazi ya Kitaifa. Misingi hiyo ni Uwazi, Uwajibikaji, Ushirikishwaji, Utawala wa Sheria na Ujumuishi.

Mhe. Spika, Serikali ilianzisha utaratibu wa kujitathmini katika utendaji wa kazi zake kupitia Wizara na Taasisi zake wenyewe. Utaratibu huo ambao unasimamiwa na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, unazitaka Wizara na Ofisi za Serikali kila baada ya miezi mitatu kueleza utekelezaji wa malengo waliyoyaweka na matumizi yaliyofanyika. Utaratibu huu umeimarisha uwazi na uwajibikaji kwa watendaji wa Serikali. Naomba kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Rais kwa kusimamia utaratibu huu ambao umeleta tija katika utendaji wa Serikali.

Mhe. Spika, juhudi za kuimarisha misingi ya Utawala Bora nchini zilikwenda sambamba na mageuzi ya kiutawala na kitaasisi ambayo yameweka mazingira mazuri ya utekelezaji wa Sera na Miongozo mbali mbali ili kuimarisha Utawala Bora, utoaji wa huduma bora kwa wananchi na ukuaji wa uchumi nchini.

Mhe. Spika, Serikali tayari imepitisha Sera ya Utawala Bora tokea 2011. Sera hii imetayarishwa mahsusi kwa ajili ya kukuza na kuimarisha misingi ya Utawala Bora kwa lengo la kuimarisha maendeleo ya wananchi kisiasa, kiuchumi, kijamii na kiutamaduni. Sambamba na hilo, Serikali imeridhia Tume ya Haki za Binaadamu na Utawala Bora kufanya kazi zake hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imetunga Sheria ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Namba 1 ya mwaka 2012. Sheria hii imeanza kazi mwaka 2012 kwa kuundwa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi. Hadi kufikia Machi, 2015 jumla ya tuhuma 70 zimepokelewa. Upelelezi umekamilika kwa tuhuma 25 na kesi zake tayari zimeshapelekwa kwa Mkurugenzi wa Mashtaka kwa hatua zaidi. Kesi moja tayari imeshapelekwa Mahakamani na mbili zimepata ridhaa ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa kupelekwa Mahakamani.

Mhe. Spika, katika kufanikisha dhamira ya Serikali ya kusimamia maadili ya Viongozi wa Umma. Serikali imepitisha Mswada wa Sheria ya Maadili ya Viongozi ya mwaka 2014 ili kuhakikisha kwamba mienendo na tabia za Viongozi wa Umma inazingatia misingi ya maadili bora ya uongozi. Sheria hii ina lengo la kuanzisha Tume ya Kusimamia Maadili ya Viongozi wa Umma.

Mhe. Spika, mawasiliano kati ya Serikali na wananchi yameimarishwa kwa kutoa taarifa sahihi na kwa wakati zinazohusu hatua mbali mbali zinazochukuliwa na Serikali katika kuwaletea maendeleo wananchi wake. Aidha, Ofisi ya Rais, Ikulu na Utawala Bora kupitia Idara ya Mawasiliano – Ikulu imeendelea kutoa taarifa kwa wananchi kuhusu shughuli za maendeleo zinazotekelezwa na Mheshimiwa Rais kwa njia ya redio, televisheni na majarida.

Mhe. Spika, katika kipindi cha 2010 – 2015, Serikali imeimarisha usalama, ubora na hadhi ya Nyumba za Ikulu na Nyumba za Serikali kwa kusimamia ujenzi na matengenezo makubwa ya nyumba hizo. Nyumba hizo ni pamoja na Ikulu za Migombani, Mkoani, Chake Chake, Kibweni, Liabon Dar es Salaam pamoja na Dodoma.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuimarisha Ushirikiano wa Kikanda wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Zanzibar imeteuliwa kuwa Makao Makuu ya Kamisheni ya Kiswahili ya Afrika Mashariki (*East African Kiswahili Commission*). Kwa upande wake Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imetoa jengo lililokua likitumiwa na EACROTANAL kuwa Makao Makuu ya Kamisheni hiyo mpya. Uanzishaji wa Kamisheni hii umeipa heshima kubwa Zanzibar ikiwa ni kitovu cha lugha ya Kiswahili.

Mhe. Mwenyekiti, Wazanzibari Wanaoishi Nje ya Nchi (*Diaspora*) wana mchango mkubwa katika kuchangia maendeleo ya nchi yao. Kwa kutambua hilo serikali imo katika hatua za mwisho za kuandaa sera mahsusi ya Wanadiaspora. Sera hii itaweka miongozo kwa Wanadiaspora kushiriki katika kuchangia maendeleo ya Zanzibar. Aidha, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein aliwaalika Wanadiaspora Ikulu Zanzibar tarehe 09 Agosti, 2014 kufanya mazungumzo nao. Utaratibu ambao serikali inakusudia kuuendeleza kila mwaka.

Mhe. Mwenyekiti, katika hatua ya kutayarisha, kuratibu na kuendeleza mipango ya kiuchumi na kijamii nchini, serikali imepitisha Sheria Nam.3 ya mwaka 2012. Sheria hii imeiunda upya Tume ya Mipango na kuiwezesha kufanya kazi zake kwa ufanisi.

Mhe. Mwenyekiti, serikali imefanikiwa vizuri katika utekelezaji wa MKUZA II, hasa katika kupunguza umasikini usio wa kipato kwa kuendeleza na kuimarisha ufikiaji wa huduma za afya na elimu ya msingi kwa wananchi. Aidha, katika kupunguza umasikini wa kipato, serikali imeimarisha miundombinu ya barabara na umeme ambayo ni muhimu kwa wananchi katika kuimarisha ustawi. Vyanzo vya mapato na ukusanyaji wa mapato pia umeendelea kuimarika.

Mhe. Mwenyekiti, mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ni nyenzo muhimu ya maendeleo pamoja na kukuza uchumi na kupunguza umasikini. Serikali imeshapitisha Sera na Mswada wa Sheria ya Mashirikiano kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (*PPP*). Kupitishwa kwa Sera na Mswada wa Sheria hiyo ni hatua muhimu inayokwenda sambamba na azma ya serikali ya kukaribisha sekta binafsi katika utekelezaji wa miradi na utoaji wa huduma muhimu.

Mhe. Mwenyekiti, msukumo mkubwa uliowekwa katika utoaji wa takwimu sahihi ambazo huwa zinasaidia katika mipango ya maendeleo pamoja na kufanya utekelezaji wa mipango na programu mbali mbali. Katika kuhakikisha uwepo wa takwimu sahihi, tafiti mbali mbali zilifanyika zikiwemo Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya wa mwaka 2009/2010 na utafiti wa kila mwaka wa Hali ya Uchumi wa Zanzibar. Aidha, mapitio ya Takwimu za Pato la Taifa yamefanyika kwa kuingiza maeneo mapya ya takwimu na kugeuza mwaka wa hesabu (*Rebasing of Gross Domestic Product Estimates*) kutoka 2001 na kuwa 2007.

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali imeratibu na kusimamia zoezi la Sensa ya Watu na Makaazi ya mwaka 2012 kwa upande wa Zanzibar. Matokeo ya sensa hiyo yanasaidia kupanga mipango inayozingatia masuala ya idadi ya watu.

Mhe. Mwenyekiti, serikali imeijengea uwezo Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ili iweze kusimamia majukumu yake ipasavyo. Katika kipindi cha 2010 - 2015, ofisi hii imeweza kukagua hesabu za Wizara na Taasisi za Serikali hadi kufikia mwaka 2013/2014. Aidha, ofisi hii imekamilisha ujenzi wa majengo ya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kote Unguja na Pemba.

MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA 2014/2015 UKUSANYAJI WA MAPATO

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2014/2015, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ilipanga kukusanya jumla ya shilingi milioni 18.0 ikiwa ni ada ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali. Hadi kufikia Machi 2015, ofisi imekusanya shilihngi milioni 9.0 sawa na asilimia 50 ya lengo lililowekwa.

UTEKELEZAJI WA KAZI ZA KAWAIDA NA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA 2014/2015

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2014/2015, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ilitengewa jumla ya shilingi milioni 23,652.9. Kati ya hizo shilingi milioni 13,551.2 kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na shilingi milioni 10,101.7 kwa ajili ya matumizi ya Programu na Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia Machi 2015, ofisi imeingiziwa shilingi 9,174.0 milioni kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida sawa na asilimia 67.7 ya fedha zilizotengwa. Aidha, kwa upande wa miradi ya maendeo, hadi kufikia Machi 2015, ofisi imeingiziwa shilingi 4,786.8 milioni sawa na asilimia 47.4 ya fedha zilizoidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2014/2015. (Angalia **Kiambatanisho Namba 9 na 10** kwa ufafanuzi zaidi).

Mhe. Mwenyekiti, utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2014/2015 ulizingatia Malengo ya Milenia (2000 – 2015), Dira ya 2020, Malengo ya MKUZA II, Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2010–2015, Maelekezo ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, Muongozo wa Utayarishaji wa Bajeti na Mipango kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015, Maelekezo ya Viongozi Wakuu wa Serikali pamoja na maoni na ushauri wa Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi. Sambamba na hayo, utekelezaji huu ulizingatia pia maeneo yaliyopewa vipaumbele katika bajeti ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ya mwaka 2014/2015.

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako sasa naomba kuwasilisha utekelezaji wa mambo yaliyokusudiwa kutekelezwa na Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika kila idara kwa mwaka wa fedha 2014/2015 kama ifuatavyo:-

OFISI YA FARAGHA YA RAIS

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Faragha ya Rais imeratibu shughuli mbali mbali na kusimamia huduma za Mhe. Rais kama zilivyopangwa. Katika mwaka wa fedha 2014/2015, Ofisi ya Faragha ilitengewa jumla ya shilling 2,446.8 milioni kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Machi 2015, ofisi iliingiziwa shilingi 1,757.0 milioni sawa na asililimia 71.8 ya makadirio ya matumizi.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2014/2015, Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Ali Mohamed Shein alifanya ziara mbili za kikazi nje ya nchi. Kwanza, aliongoza ujumbe wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa niaba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete katika Mkutano wa Tatu wa Kimataifa wa Nchi za Visiwa Vidogo Zinazoendelea uliofanyika katika Visiwa vya Samoa tarehe 1 - 4 Septemba, 2014. Maudhui ya mkutano huo, ulioratibiwa na Umoja wa Mataifa na kuhudhuriwa na Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa Mhe. Ban Ki-moon, yalikuwa ni maendeleo endelevu kwa nchi zinazoendelea za visiwa kwa ushirikiano thabiti na endelevu.

Mhe. Mwenyekiti, katika mkutano huo, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilipewa heshima ya kuwa Makamu Mwenyekiti na hotuba ya Mhe. Rais ilipokelewa vyema na wajumbe hasa kutokana na msimamo wake aliousisitiza kwa nchi za visiwa vidogo zinazoendelea katika kukabiliana na changamoto mbali mbali za mazingira. Wajumbe kutoka nchi mbali mbali walibadilishana uzoefu katika masuala ya kujikinga na maafa, bahari na *bioanuai*, maendeleo ya jamii, ushirikiano na ubia badala kutegemea misaada pamoja na masuala ya kujenga uwezo kwa nchi za visiwa vidogo zinazoendelea.

Mhe. Mwenyekiti, katika mkutano wa Samoa, ulizinduliwa Mpango wa Magharibi ya Bahari ya Hindi wa changamoto za Ukanda wa Pwani na mabadiliko ya Tabianchi ambapo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaunga mkono mpango huo wenye lengo la uhifadhi na usimamizi wa pamoja wa mazingira ya visiwa, fukwe na bahari zake pamoja na mabadiliko ya tabianchi. Mkutano wa Samoa ulipitisha Azimio linaloainisha mikakati ya kuzikwamua nchi za visiwa katika masuala ya Utalii, Mabadiliko ya Tabianchi, Usalama wa Chakula na Nishati endelevu.

Mhe. Mwenyekiti, mbali ya kuhudhuria mkutano huo, Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alikutana na kufanya mazungumzo na Rais wa Seychelles, Mhe. James Michel, Rais wa Muungano wa Comoro Mhe.Dkt. Ikililou Dhoinine na Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Kimataifa cha Biashara (*ITC*) chenye Makao Makuu yake Mjini Geneva Bibi Arancha Gonzalez.

Mazungumzo hayo yalilenga katika kukuza ushirikiano baina ya Zanzibar na nchi hizo pamoja na kuimarisha biashara.

Mhe. Mwenyekiti, ziara ya pili ya Mhe. Rais ilifanyika katika Muungano wa Visiwa vya Comoro kwa mwaliko wa Rais wa nchi hiyo Mhe. Dkt. Ikililou Dhoinine kuanzia tarehe 15 - 18 Septemba, 2014. Akiwa nchini humo, Mhe. Rais alifanya mazungumzo na mwenyeji wake na viongozi wengine wa nchi hiyo ambapo lengo kuu likiwa ni kuimarisha ushirikiano kati ya nchi mbili hizi kwa faida na ustawi wa wananchi wake. Aidha, ziara hiyo ilimuwezesha Mhe. Rais kutembelea Mji wa Kale wa Mitsamihouli, Chuo Kikuu cha Comoro, Kiwanda cha Uvuvi cha HAIRU, Kiwanda cha Kusindika mafuta ya Mlangilangi na Vanila pamoja na maeneo mbali mbali ya kihistoria.

Mhe. Mwenyekiti, katika ziara hiyo, Zanzibar na Muungano wa Visiwa vya Comoro zimetiliana saini makubaliano katika nyanja za elimu, afya, utalii, kilimo, uvuvi, habari na utamaduni, usafiri wa baharini, biashara na mambo ya dini. Ziara hiyo imepelekea kuimarika zaidi kwa udugu, uhusiano na ushirikiano baina ya Zanzibar na Muungano wa Visiwa vya Comoro. Kwa upande wa Uchumi, Kampuni ya HAIRU ya Srilanka ambayo imewekeza katika kiwanda cha kutengeneza boti, uhifadhi wa samaki na uvuvi wa bahari kuu Kisiwani Comoro imekubali kushirikiana na kuwekeza Zanzibar katika nyanja hizo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa elimu, Comoro imeamua kuleta wanafunzi wake katika Vyuo Vikuu vya Zanzibar. Kadhalika, ushirikiano katika sekta ya habari kwa njia ya kubadilishana ujuzi na utaalamu utaimarishwa. Vile vile, masuala ya kurejesha usafiri wa meli baina ya Zanzibar na Comoro pamoja na kuendeleza mahusiano ya kibiashara yamezingatiwa na kukubaliwa kwa pande zote mbili.

Mhe. Mwenyekiti, katika mikutano ya kukuza ushirikiano wa Kimataifa, Mhe. Rais amekutana na viongozi mbali mbali walipofanya ziara hapa Zanzibar akiwemo Mhe. Joachim Gauck, Rais wa Shirikisho la Jamhuri ya Ujerumani na ujumbe wake, tarehe 4 Februari, 2015, Mhe. Mtoto wa Mfalme Akishino wa Japan na mkewe, tarehe 4 Julai, 2014 pamoja na Mhe. Dkt. Marieta Cutino Readriguez, Naibu Waziri wa Ufundishaji na Utafiti, Wizara ya Afya ya Cuba na ujumbe wake, tarehe 29 Septemba, 2014. Viongozi wote hao walifurahishwa na maendeleo ya Zanzibar hasa hali ya amani iliyopo na hivyo kumpongeza Mhe. Rais, Dkt. Ali Mohamed Shein, kwa uongozi wake madhubuti. Orodha ya Wageni waliofika Ikulu kuonana na Mhe. Rais inaonekana katika **Kiambatanisho Namba 1.**

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Faragha ya Rais imeratibu ziara 31 za ndani za Mhe. Rais katika shughuli za Kiserikali. Ziara hizo zilifanyika Unguja, Pemba, Dar es

Salaam, Dodoma, Arusha na Lindi. Aidha, Ofisi imeweza kufuatilia maagizo na ahadi 40 za Mhe. Rais katika maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba jambo ambalo limepelekea kupatikana ufumbuzi kwa changamoto kadhaa na kuleta faraja kwa wananchi. Miongoni mwa maagizo na ahadi hizo ni ujenzi wa barabara ya Kisiwandui, umalizaji wa ujenzi wa Skuli ya Sekondari ya Wilaya ya Kusini, Paje Mtule, na udhibiti wa eneo la Kiwanda cha Matofali Kwarara kwa upande wa Unguja. Vile vile, ujenzi wa soko la Tumbe, maendeleo ya ukarabati wa skuli ya Kizimbani na ujenzi wa tangi la maji Ziwani kwa upande wa Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Faragha imeweza kuwaendeleza wafanyakazi wake katika masomo ambapo wafanyakazi wanne wamemaliza masomo yao katika fani ya Huduma za Hoteli na Ukarimu ngazi ya Stashahada. Maelezo zaidi Mhe. Mwenyekiti, yanasomeka katika kifungu 46 na 47. Wafanyakazi sita wanaendelea na masomo ya muda mrefu, watatu ngazi ya Stashahada, wawili ngazi ya Cheti na mmoja amepatiwa fursa ya kujiunga na Shahada ya Uzamivu (*PhD*) katika Lugha ya Kiswahili inayotolewa na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Aidha, Ofisi imewapatia fursa wafanyakazi wawili kuhudhuria mafunzo ya muda mfupi nchini China katika fani ya Uhusiano wa Kimataifa.

Mhe. Mwenyekiti, mbali na majukumu yalioanishwa, Ofisi imeweza kutekeleza kazi mbali mbali zifuatazo:-

(i) Kuchapisha hotuba mbali mbali za Mhe. Rais na kuweka kumbukumbu za hotuba hizo katika *CD* na *DVD*.

(ii) Kufanikisha Sherehe za Serikali pamoja na kutoa huduma mbali mbali kwa wageni rasmi wanaoalikwa na Mheshimiwa Rais.

(iii) Kutunza na kukarabati majengo ya Ikulu ya Mnazimmoja, Ikulu ndogo ya Migombani, Mkoani, Kibweni, Liabon, Dodoma na Chake Chake. Aidha, kununua vifaa mbali mbali vya kutendea kazi.

OFISI YA BARAZA LA MAPINDUZI

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Ofisi ya Baraza la Mapinduzi iliidhinishiwa jumla ya shilingi 1,458.2 milioni kwa matumizi ya kazi za kawaida. Hadi kufikia Machi 2015, ofisi imeingiziwa jumla ya shilingi 1,012.7 milioni sawa na asilimia 69.5 ya fedha zilizoidhinishwa.

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Baraza la Mapinduzi imeandaa vikao 18 vya kawaida vya Baraza la Mapinduzi, vikao vitano vya Kamati za Baraza la Mapinduzi na vikao 34 vya Kamati ya Makatibu Wakuu. Katika vikao hivyo, jumla ya nyaraka

72 zikiwemo za Sera na Miswada ya Sheria ziliwasilishwa, kujadiliwa na kutolewa maelekezo ambazo zinaonekana katika **Kiambatanisho Namba 2**. Mbali na nyaraka hizo, jumla ya taarifa 60 ziliwasilishwa mbele ya Baraza la Mapinduzi na Kamati zake.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuongeza ufanisi, kukuza uwajibikaji na kutekeleza kwa vitendo dhana ya Utawala Bora, Ofisi ya Baraza la Mapinduzi imeratibu vikao 17 vilivyojadili utekelezaji wa malengo ya bajeti za Wizara za SMZ. Vikao hivyo hufanyika kati ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Watendaji Wakuu wa Wizara, Idara na Taasisi za Serikali. Katika vikao hivyo, miongozo na maelekezo mbali mbali yalitolewa kwa shabaha ya kuongeza ufanisi na kukuza uwajibikaji kwa watendaji wa serikali.

Maelezo zaidi Mhe. Mwenyekiti, ya kazi zilizofanywa na Ofisi ya Baraza la Mapinduzi yanasomeka katika vifungu vya 51 na 52.

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Baraza la Mapinduzi kwa kushirikiana na Chuo cha Uongozi cha Dar es Salaam (UONGOZI *Institute*) iliratibu na kusimamia warsha ya Uongozi kwa ajili ya Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya. Warsha hiyo iliwashirikisha pia Makatibu Tawala wa Mikoa na Wilaya zote za Zanzibar pamoja na baadhi ya Mikoa ya Tanzania Bara. Warsha hii ilizungumzia masuala ya uongozi pamoja na muingiliano na mipaka baina ya Viongozi wa Kisiasa na Kiutendaji katika Mamlaka za Tawala za Mikoa. Washiriki wa Zanzibar walipata wasaa mzuri wa kubadilishana uzoefu na wenzao wa Tanzania Bara ambao utasaidia sana katika kuimarisha utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku.

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi hiki, Ofisi hii imewajengea uwezo wa kiutendaji wafanyakazi wake kwa lengo la kuwawezesha kutekeleza vyema majukumu yao na kupatiwa vitendea kazi vya kisasa. Jumla ya wafanyakazi watatu wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu ya Stashahada, Shahada ya Kwanza na ya Pili katika fani za Uhazili, Utawala na Uhusiano wa Kimataifa. Ofisi pia imewapatia wafanyakazi wake wanne mafunzo ya muda mfupi katika fani za Uongozi, Usimamizi wa Ofisi, Utunzaji wa Kumbukumbu na Udereva wa Viongozi Mashuhuri. Aidha, wafanyakazi wote wa Ofisi hii wamepatiwa taaluma kuhusu namna bora ya kujikinga na maambukizi mapya ya Virusi vya UKIMWI.

IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti iliidhinishiwa jumla ya Shilingi 428.3 milioni kwa matumizi ya kazi za kawaida na Shilingi 530.0 milioni kwa matumizi ya kazi za maendeleo. Hadi kufikia Machi 2015, Idara imeingiziwa jumla ya shilingi 188.2 milioni kwa ajili ya

matumizi ya kazi za kawaida sawa na asilimia 43.9 ya fedha zilizoidhinishwa na shilingi 350 milioni kwa ajili ya matumizi ya kazi za maendeleo sawa na asilimia 66.0 ya fedha zilizoidhinishwa.

Mhe. Mwenyekiti, idara imefanya maandalizi ya Utafiti wa Hali Uwajibikaji Kijamii kwa Taasisi za Umma na Taasisi Binafsi (*Corporate Social Responsibility*) kwa kushirikiana na Chuo cha Uongozi wa Fedha Chwaka. Utafiti huu ni muhimu sana katika kutoa taswira ya hali ya uwajibikaji kijamii kwa Taasisi za Umma na Binafsi kama ilivyosisitizwa katika Sera ya Utawala Bora ya Zanzibar ya mwaka 2011 pamoja na Mikataba ya Kimataifa. Matokeo ya utafiti huu yataiwezesha serikali kuangalia uwezekano wa kulifanya suala la uwajibikaji kijamii kuwa na nguvu za kisera na kisheria badala ya kuwa la hiyari kama ilivyo hivi sasa.

Mhe. Mwenyekiti, vifungu vya 55 na 56 vinafafanua zaidi utekelezaji wa kazi za Idara ya Mipango, Sera na Utafiti.

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi hiki, Idara ilifanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa Malengo ya Bajeti katika Idara na Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi pamoja na Mradi wa Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Ikulu na Nyumba za Serikali. Lengo la ufuatiliaji huo lilikuwa ni kuhakikisha kuwa hatua za utekelezaji zinaendana na mpango kazi na fedha zilizotolewa kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2014/2015. Aidha, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti pia imeandaa Taarifa za Utekelezaji wa Malengo ya Bajeti pamoja na Taarifa za Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Mwaka 2010.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2014/2015, Idara imeratibu maandalizi ya Sera ya Diaspora pamoja na Mswada wa Sheria ya Maadili ya Viongozi ambao tayari umeshapitishwa na Baraza lako Tukufu. Aidha, katika kuimarisha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (*ICT*), Idara imesimamia ufungaji wa Mtandao wa Ndani (*Intra Network*) wenye kuwaunganisha wafanyakazi wa Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora kwa lengo la kuongeza ufanisi wa utendaji kazi. Sambamba na hilo, Idara imekamilisha uungaji wa Mtandao wa Serikali (*e-Government*) katika Ofisi hii.

IDARA YA MAWASILIANO – IKULU

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha wa 2014/2015, Idara ya Mawasiliano – Ikulu iliidhinishiwa jumla ya shilingi 225.8 milioni kwa matumizi ya kazi za kawaida. Hadi kufikia Machi 2015, idara imeingiziwa shilingi 179.8 milioni sawa na asilimia 79.6 ya fedha zilizoidhinishwa.

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Mawasiliano - Ikulu imeandaa na kurusha hewani vipindi 24 vya redio na 16 vya televisheni ambavyo baadhi yake vimeainishwa katika **Kiambatanisho Namba 3**. Vipindi hivyo vilizungumzia na kuonesha hatua iliyofikiwa na serikali katika maendeleo ya mijini na vijijini kwenye sekta za maji, barabara na elimu. Aidha, taarifa hizo pia zilichapishwa katika magazeti na majarida ambapo makala mbali mbali yameandaliwa ili kutoa ufafanuzi zaidi juu ya utekelezaji huo. Katika kipindi hiki, matoleo matano ya Jarida la Ikulu yamechapishwa nayo ni Jarida Toleo Namba 015, 016, 017, 018 na 019. Jumla ya nakala 15,000 zilichapishwa na kusambazwa kwa wadau mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, idara imeandaa Kitabu Maalum kinachoitwa Miaka 4 ya Dkt. Shein chenye Ujumbe Mahsusi unaosomeka 'Tunajivunia Amani, Utulivu na Maendeleo'. Kitabu hicho kinaelezea kwa kina mafanikio yaliopatikana katika kipindi cha miaka minne (2010 – 2014) chini ya uongozi wake katika Sekta za Uchumi, Elimu, Kilimo na Maliasili, pia Afya, Utalii, Umeme, Maji, Miundombinu, Habari na Utamaduni. Maeneo mengine ambayo mafanikio yake yameainishwa katika kitabu hicho ni pamoja na masuala mtambuka (Mazingira, Dawa za Kulevya na UKIMWI), Ujasiriamali, Ufugaji na Uvuvi, Michezo na Mahusiano ya Kimataifa. Nakala ya Kitabu hiki zilisambazwa katika Taasisi mbali mbali, vituo vyote vya walimu Unguja na Pemba pamoja na wananchi. Aidha, kitabu hicho pamoja na majarida yanayochapishwa na idara hii vinapatikana pia katika Tovuti ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa anuani ya *www.ikuluzanzibar.go.tz*.

IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, idara hii iliidhinishiwa jumla ya shilingi 1,131.8 milioni kwa matumizi ya kazi za kawaida. Hadi kufikia Machi 2015, idara iliingiziwa jumla ya shilingi 721.7 milioni sawa na asilimia 63.8 ya fedha zilizoidhinishwa.

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Uendeshaji na Utumishi imeendelea kusimamia uendeshaji wa shughuli za kila siku za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kama zilivyotajwa katika vifungu Nam. 61, 62 na 63. Kwa kuhakikisha upatikanaji wa vifaa na huduma mbali mbali vikiwemo vifaa vya kuandikia, usafi, malipo ya umeme, maji, matengenezo ya simu na vyombo vya usafiri pamoja na vifaa vyengine vya kazi.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuhakikisha kuwa watumishi wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi wanatekeleza majukumu yao katika mazingira mazuri, Idara ya Uendeshaji na Utumishi imeendelea kusimamia upatikanaji wa maslahi ya watumishi wake ikiwemo kulipa mishahara na

kuwasilisha michango ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa wakati. Aidha, Idara imewajengea uwezo watumishi wanane kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu katika ngazi ya Cheti, Stashahada, Shahada ya Kwanza na Shahada ya Pili katika fani za Uboharia, Ununuzi na Ugavi, Uongozi wa Rasilimali Watu, Utunzaji kumbukumbu, Uhasibu, Utatuzi wa Migogoro, Ustawi wa Jamii na Utawala.

Mhe. Mwenyekiti, idara pia imeratibu mafunzo kwa watumishi 78 kutoka Idara na Taasisi zote zilizo chini ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Aidha, Mpango wa Mafunzo wa Ofisi ya Rais, Ikulu na Utawala Bora umeandaliwa. Mpango huo utaiwezesha Ofisi kuratibu na kusimamia masuala ya rasilimali watu kwa kuzingatia mahitaji.

Mhe. Mwenyekiti, mafunzo kwa idara na watumishi 75 kuhusu Sheria na Kanuni za Utumishiwa Umma na Maadili katika Utumishi wa Umma yametolewa. Lengo la mafunzo hayo ni kuwaelimisha watumishi kuepuka vitendo na mienendo inayochochea ukiukwaji wa maadili ya Utumishi wa Umma ikiwemo kutoa na kupokea rushwa.

Mhe. Mwenyekiti, idara pia imeandaa mkutano wa Kamati ya Uongozi ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi pamoja na vikao vitatu vya Kamati Tendaji. Aidha, vikao sita vya Bodi ya Zabuni na viwili vya Kamati ya Ukaguzi wa Ndani vimefanyika. Vikao hivyo vimesaidia sana kuimarisha utekelezaji wa Sheria Nam. 9 ya mwaka 2005 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma.

Mhe. Mwenyekiti, katika hatua ya kuimarisha michezo kazini, timu za michezo za Ikulu (*Ikulu Sports Club*) zimewezeshwa kushiriki mashindano mbali mbali yakiwemo yale na wenzao wa Ofisi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, timu ya mpira wa miguu ya Ikulu imewezeshwa kushiriki mashindano ya Mei Mosi yaliyoshirikisha Wizara, Idara na Taasisi mbali mbali za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kuweza kucheza fainali.

Mhe. Mwenyekiti, juhudi zimekuchukuliwa za kukuza na kuimarisha mashirikiano baina ya Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora Zanzibar na Ofisi ya Rais Ikulu ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania juu ya masuala ya Utawala Bora. Katika kufanikisha azma hiyo, pande mbili hizo zimeunda Kamati ya Pamoja kwa lengo la kuimarisha ushirikiano wa kikazi na mahusiano mema. Kamati hiyo tayari imeainisha maeneo ambayo pande hizi mbili zinaweza kushirikiana katika utekelezaji wa masuala ya Utawala Bora na Haki za Binaadamu.

OFISI YA USALAMA WA SERIKALI (*GSO*)

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Ofisi ya Usalama wa Serikali iliidhinishiwa jumla ya Shilingi 47.1 milioni kwa matumizi ya kazi za kawaida. Hadi kufikia Machi 2015, Ofisi ya Usalama wa Serikali imeingiziwa Shilingi 18.0 milioni sawa na asilimia 38.2 ya fedha zilizoidhinishwa.

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Usalama wa Serikali imepokea maombi ya ukaguzi 323 kutoka wizara na taasisi mbali mbali za serikali. Maombi yote hayo yamefanyiwa kazi na ushauri stahiki umetolewa. Aidha, ofisi imefanya ukaguzi wa kuangalia hali ya usalama wa majengo, watumishi pamoja na utunzaji wa nyaraka katika Kituo cha Kurushia Matangazo ya Redio (*ZBC*) - Bungi, Kiwanda cha Matrekta Mbweni, Ikulu ya Mkoani – Pemba, Kituo cha Mauzo ya Karafuu Chake Chake Pemba, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Pemba, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka Zanzibar, Idara ya Nishati na Uwanja wa Amani. Ripoti za ukaguzi huo zimekamilika na kuwasilishwa katika taasisi husika kwa kufanyiwa kazi.

IDARA YA UTAWALA BORA

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Idara ya Utawala Bora iliidhinishiwa jumla ya Shilingi 227.7 milioni kwa matumizi ya kazi za kawaida. Hadi kufikia Machi 2015, idara imeingiziwa Shilingi 130.6 milioni sawa na asilimia 57.4 ya fedha zilizoidhinishwa.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuimarisha misingi ya Utawala Bora, Idara ya Utawala Bora imetoa elimu ya Uraia kwa umma katika masuala ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. Elimu hiyo ilitolewa kwa Kamati saba za Shehia na kwa wananchi wa Shehia 18 kwa njia ya mikutano ya hadhara ambazo zinaonekana katika **Kiambatanisho Namba 4**.

Aidha, idara imeendelea kuielimisha jamii juu ya masuala ya utawala bora kwa njia ya televisheni na redio ambapo jumla ya vipindi 22 vya redio na 13 vya televisheni viliandaliwa na kurushwa hewani kupitia Shirika la Utangazaji la Zanzibar (*ZBC*) ambapo mada za vipindi hivyo zimeorodheshwa katika **Kiambatanisho Namba 5**. Vipindi hivyo vya televisheni vinaendelea kurushwa hewani kila siku ya Jumatatu kuanzia saa 1:30 usiku na kwa vipindi vya redio hurushwa hewani kila siku ya Jumanne kuanzia saa 1:30 usiku na kurejewa siku ya Jumamosi saa 3:45 usiku. Sambamba na hayo, idara pia imeandaa matangazo mafupi (*Jingles*) na maelezo baada ya habari ambayo yalitolewa na Shirika la Utangazaji Zanzibar (*ZBC*) kupitia Televisheni na Redio.

Mhe. Mwenyekiti, idara pia imefanya utafiti mdogo juu ya masuala ya Utawala Bora kwa lengo la kupata taarifa za utekelezaji wa misingi ya Utawala Bora ili ziweze kutumika katika kuandaa ripoti ya mwaka ya utawala bora. Utafiti huo umefanyika katika wizara tisa, Taasisi tatu za Serikali, Asasi 12 za Kiraia na Shehia 20 kwa Unguja na Pemba. Matokeo ya utafiti huo yametumika kuandaa Rasimu ya Ripoti ya Utawala Bora ya mwaka 2014 ambayo imepangwa kuwasilishwa katika vikao vya juu hivi karibuni.

Mhe. Mwenyekiti, idara pia imefanya semina kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusu yaliyomo ndani ya Mswada wa Sheria ya Maadili ya Viongozi. Tume ya Maadili ya Viongozi inatarajiwa kuanza kazi rasmi katika mwaka wa fedha 2015/2016.

OFISI YA OFISA MDHAMINI – PEMBA

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Ofisi ya Ofisa Mdhamini iliidhinishiwa jumla ya Shilingi 599.9 milioni kwa matumizi ya kazi za kawaida. Hadi kufikia Machi 2015, ofisi imeingiziwa Shilingi 380.3 milioni sawa na asilimia 63.4 ya fedha zilizoidhinishwa.

Mhe. Mwenyekiti, ofisi imesimamia upatikanaji wa huduma katika majengo ya Ikulu Pemba, ikiwa ni pamoja na ufukizaji (*fumigation*), usafi na uimarishaji wa bustani. Aidha, Ofisi imekamilisha matengenezo makubwa ya jengo jipya la Ofisi ya Ofisa Mdhamini wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Pemba katika eneo la Chake Chake na tayari ofisi hiyo imeshahamiwa. Ofisi ya Ofisa Mdhamini Pemba pia imesimamia ujenzi na matengenezo makubwa ya Ikulu ya Mkoani; ujenzi wa Ikulu hiyo umekamilika na tayari kuanza kutumika. Sambamba na hayo, ofisi imesimamia upatikanaji wa hatimiliki za majengo ya Ikulu ya Chake Chake na Mkoani Pemba, hati hizo tayari zimeshapatikana.

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Ofisa Mdhamini Pemba imetoa Elimu ya Uraia kupitia Redio Jamii Micheweni. Elimu hiyo ilihusu umuhimu wa Utawala Bora, Ushirikishwaji wa wananchi katika mambo yanayowahusu, haki za mtuhumiwa na athari za uvunjaji wa haki za binaadamu. Elimu ya Uraia pia ilitolewa kupitia mikutano ya hadhara kwa wananchi wa Shehia 15 na Kamati za Sheha katika Shehia 15 ambazo zimeainishwa katika **Kiambatanisho Namba 6 na 7**. Aidha, mijadala kuhusu Utawala Bora imefanyika katika Chuo cha Ualimu cha Benjamin Mkapa, Chuo cha Kiislamu Micheweni na Chuo cha Mafunzo ya Amali, Vitongoji.

IDARA YA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA NA URATIBU WA WAZANZIBARI WANAOISHI NJE YA NCHI

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Idara hii iliidhinishiwa jumla ya Shilingi 808.2 milioni kwa matumizi ya kazi za kawaida. Hadi kufikia Machi 2015, idara hii imeingiziwa Shilingi 378.5 milioni sawa na asilimia 46.8 ya fedha zilizoidhinishwa.

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa Wazanzibari Wanaoishi Nje ya Nchi imewawezesha Maofisa kutoka Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhudhuria Mkutano wa 29 wa Baraza la Mawaziri la Afrika Mashariki pamoja na Mkutano wa kupitia Sheria za Mkataba wa Ubia wa Kiuchumi uliofanyika Arusha. Aidha, idara pia imemuwezesha Mtaalamu kutoka Wizara ya Afya kushiriki katika Mkutano wa 11 wa Baraza la Mawaziri la Kisekta la Afya pamoja na Kongamano la tano la Afya na Sayansi la Afrika Mashariki na Maonesho ya Biashara ya Kimataifa ya Afya yaliofanyika nchini Uganda.

Mhe. Mwenyekiti, idara iliratibu ushiriki wa Zanzibar katika Mkutano wa majadiliano ya Makao Makuu ya Kamisheni ya Kiswahili pamoja na Mkutano wa majadiliano baina ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Kenya. Taratibu zote za kuanzisha Kamisheni hiyo zimekamilika. Hata hivyo, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeipelekea Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki mapendekezo ya marekebisho ya vifungu vya Mkataba wa Makao Makuu ili viangaliwe tena kwa manufaa ya Zanzibar na Tanzania kwa jumla. Vifungu hivyo vinahusu ajira ya wafanyakazi wa ngazi za chini (*general staff*).

Mhe. Mwenyekiti, Rasimu ya Sera ya *Diaspora* Zanzibar imekamilika na hatua inayofuata ni kuipitisha Rasimu hiyo katika utaratibu wa kiserikali. Sera hii itaweka miongozo sahihi na mazingira rafiki yatakayowawezesha *Diaspora* wa Zanzibar kushiriki kikamilifu katika maendeleo ya nchi yao.

Mhe. Mwenyekiti, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kushirikiana na Benki Kuu ya Tanzania, kwa mwaka wa fedha 2015/2016, itafanya utafiti wa kutambua kiwango cha fedha zinazoletwa nchini kutoka kwa Wanadiaspora. Vile vile, katika mwaka huu wa fedha, serikali kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Uhamiaji (*IOM*) inakusudia kufanya utafiti wa kuweka "*Data base*" ya Wanadiaspora wote ili wajulikane mahala walipo na shughuli wanazofanya.

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi hiki, idara imeendelea kuwajengea uwezo watendaji wake kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na mrefu. Mfanyakazi mmoja aliwezeshwa kuhudhuria mafunzo ya muda mfupi ya Diplomasia

(*Diplomatic Training Course*) nchini Malaysia na mfanyakazi mmoja amehudhuria mafunzo ya uhasibu katika Chuo cha *Kampala International University* (*KIU*) '*Campus'* ya Dar es Salaam. Aidha, Maofisa watatu wamewezeshwa kushiriki ziara ya mafunzo juu ya *Diaspora* nchini India.

MAMLAKA YA KUZUIA RUSHWA NA UHUJUMU WA UCHUMI ZANZIBAR

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Mamlaka iliidhinishiwa jumla ya Shilingi 815.4 milioni kwa matumizi ya kazi za kawaida na Shilingi 621.7 milioni kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia Machi 2015, Mamlaka imeingiziwa Shilingi 525.9 milioni sawa na asilimia 64.5 ya fedha zilizoidhinishwa kwa kazi za kawaida na Shilingi 319.6 milioni sawa na asilimia 51.4 ya fedha zilizoidhinishwa kwa kazi za Maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia Machi 2015, Mamlaka imekamilisha uchunguzi wa tuhuma 26 za rushwa na uhujumu wa uchumi kati ya tuhuma 40 zilizopokelewa. Majalada mawili ya watuhumiwa wa makosa hayo tayari yamewasilishwa katika Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (*DPP*) kwa hatua zaidi. Mamlaka inaendelea na uchunguzi wa tuhuma 14 zilizosalia.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuimarisha mazingira bora ya kazi, Mamlaka imeendelea kuweka mkazo katika kuwajengea uwezo wa kiutendaji watumishi wake. Jumla ya watumishi sita wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi katika fani mbali mbali na watumishi wawili bado wanaendelea na mafunzo ya muda mrefu. Watumishi wengine 14 wamejengewa uwezo kwa kupatiwa mafunzo kwa vitendo katika Ofisi ya Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Tanzania (TAKUKURU). Sambamba na hayo, watumishi watatu wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi ya kupambana na rushwa katika Serikali za Mitaa, nchini Austria. Aidha, maofisa watatu walifanya ziara ya kimafunzo nchini Romania kwa lengo la kubadilishana uzoefu na watendaji wa Taasisi hizo nchini humo.

Mhe. Mwenyekiti, katika juhudi za kuimarisha shughuli za ufuatiliaji na utendaji wa kazi za kila siku za Mamlaka, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, serikali imeipatia mamlaka gari mbili zitakazotumiwa na mamlaka hiyo. Moja kati ya gari hizo inatumika katika ofisi yake mpya iliyofunguliwa hivi karibuni Chake Chake, Pemba na nyengine inatumiwa na Ofisi iliyopo Unguja.

OFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI ZANZIBAR

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali iliidhinishiwa jumla ya Shilingi 2,023.0 milioni kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida. Hadi kufikia Machi 2015, Ofisi hii imeingiziwa jumla ya Shilingi 1,661.3 milioni sawa na asilimia 82.1 ya fedha zilizoidhinishwa.

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imeimarisha uwezo wa wafanyakazi wake kitaaluma katika fani mbali mbali za ukaguzi zikiwemo ukaguzi wa kimazingira, ukaguzi wa Kompyuta, uchambuzi wa taarifa za ukaguzi, ukaguzi yakinifu (*Value for Money*) na muongozo wa ukaguzi (*Regulatory Audit Manual*).

Mhe. Mwenyekiti, Wafanyakazi 50 wamepatiwa mafunzo ya ukaguzi yakinifu (*Value for Money Audit*), Wafanyakazi 30 wamepatiwa mafunzo ya tathmini ya kugundua maeneo hatarishi ya ukaguzi (*Risk Based Audit*), wafanyakazi 25 wamepatiwa mafunzo ya ukaguzi kwa kompyuta (*IT Audit*) na wafanyakazi watatu wamepata mafunzo ya ukaguzi yakinifu yalioandaliwa na Jumuiya ya Taasisi za Ukaguzi Afrika (*AFROSAI-E*).

Mhe. Mwenyekiti, vile vile, wafanyakazi hao wamepatiwa mafunzo juu ya ukaguzi wa hesabu unaozingatia viwango vilivyowekwa Kitaifa na Kimataifa katika ufungaji wa hesabu na uwekaji wa kumbukumbu za hesabu. Aidha, ofisi imeweza kutoa mafunzo kwa wakaguzi kuhusu mabadiliko ya bajeti kutoka Mfumo wa Vifungu (*Line Item Budget)* kwenda katika Mfumo Unaozingatia Matokeo (*Program Based Budget*).

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa mafunzo ya muda mrefu, jumla ya wafanyakazi 24 wapo katika vyuo mbali mbali wanaendelea na mafunzo yao katika ngazi ya Stashahada na Shahada katika fani za Ukaguzi.

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia Machi 2015, ofisi imefanya ukaguzi wa hesabu za mwaka 2013/2014 katika taasisi mbali mbali za Serikali kwa kufuata muongozo wa ukaguzi. Ukaguzi wa hesabu hizo upo katika hatua za mwisho.

Mhe. Mwenyekiti, Jengo la Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Pemba limekamilika na kuwekwa samani pamoja na vifaa vya kisasa vya teknolojia. Jengo hilo limezinduliwa rasmi na Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi tarehe 2 Disemba, 2014.

TUME YA MIPANGO

Mhe. Mwenyekiti, majukumu ya Tume ya Mipango yanatekelezwa kupitia Idara ya Mipango ya Kitaifa, Maendeleo ya Kisekta na Kupunguza Umasikini, Idara ya Ukuzaji Uchumi, Idara ya Mipango na Maendeleo ya Watenda Kazi, Divisheni ya Uendeshaji na Utumishi. Aidha, Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali ni taasisi inayojitegemea ndani ya Tume ya Mipango.

IDARA YA MIPANGO YA KITAIFA, MAENDELEO YA KISEKTA NA KUPUNGUZA UMASIKINI

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Idara ya Mipango ya Kitaifa, Maendeleo ya Kisekta na Kupunguza Umasikini iliidhinishiwa jumla ya Shilingi 441.4 milioni kwa ajili ya kazi za kawaida na Shilingi 1,888.1 milioni kwa matumizi ya kazi za maendeleo. Hadi kufikia Machi 2015, Idara imeingiziwa Shilingi 238.9 milioni sawa na asilimia 54.1 ya fedha zilizoidhinishwa kwa matumizi ya kazi za kawaida na Shilingi 1,382.4 milioni sawa na asilimia 73.2 ya fedha zilizotengwa kwa matumizi ya kazi za maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, idara imekamilisha Mapitio ya Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2014/2015. Aidha, maandalizi ya Kitabu cha Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo Zanzibar kwa mwaka 2015/2016 yamekamilika kwa kuwashirikisha Wakurugenzi Mipango, Sera na Utafiti wa Wizara za Serikali. Sambamba na hilo, idara imeandaa Taarifa ya Awali (*Baseline Report*) ya viashiria kwa ajili ya ufuatiliaji wa kazi za Maabara ya Utalii (*R4P*) baada ya kujadiliwa katika ngazi mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, idara imefanya ufuatiliaji wa baadhi ya miradi ya maendeleo katika sekta za miundombinu, nishati, kilimo, maji, viwanda na elimu. Lengo la ufuatiliaji huo lilikuwa ni kuhakikisha kuwa kazi za utekelezaji wa miradi zinaendana na mpango kazi na fedha zilizotolewa. Ripoti ya ufuatiliaji huo tayari imeshajadiliwa katika kikao maalum cha Wakurugenzi Mipango, Sera na Utafiti na kutoa mapendekezo yatakayofanikisha utekelezaji wa Programu na Miradi kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Mipango ya Kitaifa, Maendeleo ya Kisekta na Kupunguza Umasikini imeandaa Maadhimisho ya Wiki ya Umasikini Duniani ambapo vitabu na vipeperushi vyenye kutoa taarifa za Mipango ya Kitaifa na utekelezaji wake vimechapishwa na kusambazwa kwa Unguja na Pemba. Maadhimisho hayo yamefanyika kwa kuandaa Tamasha tarehe 15 Oktoba, 2014

katika Ukumbi wa uwanja wa Gombani, Pemba na Tamasha la Kilele lililofanyika tarehe 18 Oktoba, 2014 katika Ukumbi wa *EACROTANAL*.

Mhe. Mwenyekiti, Idara imepitia na kujadili maandiko ya Miradi (*Project Proposals*) kutoka sekta mbali mbali na kutoa mapendekezo ya hatua zinazofaa kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi hiyo. Aidha, Idara imeanza kuandaa nyaraka mbali mbali zenye kuonesha hali halisi ya utekelezaji wa Malengo ya Milenia (*MDGs*) na Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini (MKUZA II).

Mhe. Mwenyekiti, idara imetoa mafunzo kwa Maofisa 35 wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Wizara za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Mafunzo hayo yalihusu matumizi ya mfumo mpya wa Ufuatiliaji na Tathmini pamoja na zana (*tools*) za kukusanyia taarifa husika. Aidha, Maofisa Mipango wa Tume wamepatiwa mafunzo ya namna ya kuandaa Maandiko ya Miradi na Programu pamoja na kufanya uchambuzi (*Project Appraisal*).

Mhe. Mwenyekiti, idara pia imeandaa, kuchapisha na kusambaza kwa wadau mbali mbali nakala 300 za Ripoti ya Mpango wa Ufuatiliaji na Tathmini kwa lugha ya Kiswahili. Aidha, nakala 500 za Ripoti ya utekelezaji wa Malengo ya Milenia ya mwaka 2013 tayari zimechapishwa.

IDARA YA UKUZAJI UCHUMI

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Idara ya Ukuzaji Uchumi iliidhinishiwa jumla ya Shilingi 463.7 milioni kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na Shilingi100.0 milioni kwa ajili ya matumizi ya kazi za maendeleo. Hadi kufikia Machi 2015, idara hii imeingiziwa Shilingi 285.4 milioni kwa matumizi ya kazi za kawaida sawa na asilimia 61.5 ya fedha zilizoidhinishwa na Shilingi 57.0 milioni kwa matumizi ya kazi za maendeleo sawa na asilimia 57.0 ya fedha zilizotengwa.

Mhe. Mwenyekiti, idara imetoa taarifa ya Mwenendo wa Hali ya Uchumi kwa kila mwezi. Taarifa hizo pamoja na mapendekezo huwa zinawasilishwa na kujadiliwa katika kikao cha ukomo (*Ceiling Committee*) kinachoratibiwa na Wizara ya Fedha. Taarifa za hali ya Mwenendo wa Uchumi zinajumuisha Kasi ya Mfumko wa Bei, Mwenendo wa Sekta, mapato na matumizi ya Serikali na Deni la Taifa. Jumla ya Vikao tisa vya Wataalamu vya kufanya Tathmini ya mwenendo wa hali ya uchumi vimefanyika. Vikao hivyo vilijumuisha Wajumbe kutoka Taasisi za Serikali, Vyuo Vikuu, Taasisi za Fedha nchini na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali.

IDARA YA MIPANGO NA MAENDELEO YA WATENDAKAZI

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Idara ya Mipango na Maendeleo ya Watendakazi iliidhinishiwa jumla ya Shilingi 243.8 milioni kwa matumizi ya kazi za kawaida na Shilingi 261.9 milioni kwa ajili ya matumizi ya kazi za maendeleo. Hadi kufikia Machi 2015, idara hii imeingiziwa Shilingi 166.7 milioni kwa matumizi ya kazi za kawaida sawa na asilimia 68.4 ya fedha zilizoidhinishwa na Shilingi 128.3 milioni kwa ajili ya matumizi ya kazi za maendeleo sawa na asilimia 49.0 ya fedha zilizoidhinishwa.

Mhe. Mwenyekiti, idara imeunda kikundi kazi kinachowajumuisha watendaji kutoka sekta mbali mbali kilichopewa jukumu la kuratibu mapitio ya taarifa za msingi za wilaya (*District Profiles)* katika Wilaya tano za Mjini, Kati, Kusini, Chake Chake na Micheweni. Idara tayari imepokea taarifa hizo na hatua inayofuata ni kufanya uchambuzi na uandishi.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuimarisha utekelezaji wa masuala ya kustaafu kazini, Idara imetoa mafunzo ya siku tatu kuhusu usimamizi na taratibu za kustaafu kwa Maofisa Utumishi 100 wa Taasisi za Serikali na Sekta Binafsi za Unguja na Pemba. Idara pia imeandaa utafiti juu ya athari ya uhamiaji wa watu mijini ambapo uchambuzi wa taarifa zilizokusanywa unaendelea.

DIVISHENI YA UTUMISHI NA UENDESHAJI

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Divisheni ya Utumishi na Uendeshaji iliidhinishiwa jumla ya TZS. 810.1 milioni kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida. Hadi kufikia Machi 2015, Divisheni imeingiziwa jumla ya TZS. 515.0 milioni sawa na asilimia 63.6 ya fedha zilizoidhinishwa.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2014/2015, Divisheni ya Utumishi na Uendeshaji imewawezesha wafanyakazi 17 kupata mafunzo ya muda mfupi na wafanyakazi wawili kupata mafunzo ya muda mrefu. Aidha, Idara imeratibu vikao 17, kati ya hivyo, vikao vitatu vya Tume ya Mipango, vikao vinne vya Kamati ya Wataalamu, vikao vinane vya Bodi ya Zabuni na vikao viwili vya Ukaguzi wa Hesabu.

AFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali iliidhinishiwa TZS. 1,380.0 milioni kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na TZS. 6,700.0 milioni kwa ajili ya matumizi ya kazi za maendeleo. Hadi kufikia Machi 2015, Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali imeingiziwa TZS. 1,013.9 milioni sawa na asilimia 73.5 ya fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya

matumizi ya kazi za kawaida na TZS. 2,549.6 milioni kwa ajili ya matumizi ya kazi za maendeleo sawa na asilimia 38.1ya fedha zilizoidhinishwa.

Mhe. Mwenyekiti, Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali inaendelea na zoezi la ukusanyaji wa taarifa za Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya wa mwaka 2014/2015. Utafiti huu umeanza rasmi mwezi wa Oktoba, 2014 na unatarajiwa kukamilika mwezi wa Septemba, 2015. Huu ni utafiti wa tano kufanyika hapa Zanzibar tokea baada ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ya mwaka 1964. Madhumuni makuu ya utafiti huu ni kupata taarifa za viashiria vya umasikini vitakavyotumika kupima kiwango cha umasikini, kutathmini utekelezaji wa Mpango wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Zanzibar, Malengo ya Maendeleo ya Milenia pamoja na kupata viashiria vitakavyotumika kufanya mapitio ya takwimu mbali mbali zikiwemo za fakharishi ya bei na takwimu za pato la Taifa.

Mhe. Mwenyekiti, maelezo ya kina ya utekelezaji wa shughuli zilizopangwa kwa kila Idara na Taasisi za Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kipindi cha Julai 2014 – Machi 2015 yameainishwa katika Jadweli Namba 1.

PROGRAMU NA MIRADI YA MAENDELEO

Mhe. Mwenyekiti, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mwaka wa fedha 2014/2015, imeendelea kuratibu na kutekeleza Programu na Miradi ya maendeleo kupitia Idara na Taasisi zilizo chini yake. Maelezo kuhusu utekelezaji halisi wa Programu na Miradi hiyo yameainishwa kama ifuatavyo.

MRADI WA UJENZI NA UKARABATI WA MAJENGO YA IKULU NA NYUMBA ZA SERIKALI

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Mradi wa Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Ikulu na Nyumba za Serikali uliidhinishiwa jumla ya TZS. 530.0 milioni. Hadi kufikia Machi 2015, mradi huu umeingiziwa TZS. 350.0 milioni sawa na asilimia 66.0 ya fedha zilizoidhinishwa.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuimarisha majengo ya Ikulu, Afisi imeendelea kuyafanyia matengenezo majengo mbali mbali, hadi kufikia Machi 2015, Ikulu ya Mnazimmoja imefanyiwa matengenezo madogo madogo. Aidha, nyumba ya walinzi Dodoma na nyumba ya wafanyakazi Liabon Dar es Salaam ujenzi wake umekamilika. Sambamba na hayo, Ikulu ya Mkoani imemalizika pamoja na uwekaji wa samani zake. Majengo mengine ambayo yamefanyiwa matengenezo ni Ikulu ya Kibweni na Afisi ya Rais Mstaafu wa Awamu ya sita iliyopo Mazizini. Vile vile, Afisi imefanya utanuzi wa ukuta wa Ikulu ya Migombani pamoja na kibanda cha walinzi.

Mhe. Mwenyekiti, Afisi pia imekamilisha matengenezo ya nyumba moja iliyopo ndani ya Ikulu ya Chake Chake ambayo itatumiwa na Wasaidizi wa Mheshimiwa Rais. Aidha, imejengwa milango mikuu ya kuingilia katika Ikulu hiyo. Sambamba na hayo, matengenezo ya jengo la Afisa Mdhamini wa Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi yamekamilika na tayari limeshahamiwa. Katika azma ya kuijenga Ikulu ndogo ya Micheweni, michoro ya Ikulu hiyo imefanyiwa mapitio na utoaji wa zabuni na utaratibu wa kumpata mjenzi unaendelea.

MRADI WA UIMARISHAJI WA JUHUDI ZA KUZUIA RUSHWA ZANZIBAR

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Mradi wa Uimarishaji wa Juhudi za Kuzuia Rushwa Zanzibar uliidhinishiwa jumla ya TZS. 621.7 milioni kwa ajili ya matumizi ya kazi za maendeleo. Hadi kufikia Machi 2015, mradi huu umeingiziwa jumla ya TZS. 319.6 milioni sawa na asilimia 51.4 ya fedha zilizotengwa.

Mhe. Mwenyekiti, Mamlaka kwa kushirikiana na Shirika la Mpango wa Maendeleo la Umoja wa Mataifa imeandaa Mkakati Jumuishi wa Uadilifu na Kuzuia Rushwa Zanzibar, yaani *Zanzibar Integrated Strategy and Anti-Corruption 2015 - 2020*. Mkakati huu una madhumuni ya kuweka juhudi za pamoja kwa kuwashirikisha wadau mbali mbali katika kuzuia rushwa na uhujumu uchumi kwa kuzingatia misingi ya uadilifu.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuhakikisha kuwa Sheria ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Nam. 1, mwaka 2012 inatekelezwa ipasavyo, Mamlaka imeandaa Kanuni za Sheria hiyo ambazo zipo katika hatua ya mwisho ya kutiwa saini na kuanza kutumika. Sambamba na hilo, Mamlaka pia imefanya tathmini ya mahitaji yake hususan katika mahitaji yanayohusu majengo, vitendea kazi na rasilimali watu. Taarifa ya tathmini hiyo tayari imekamilika na imepangwa kufanyiwa kazi katika mwaka wa fedha wa 2015/2016.Maelezo zaidi juu ya mradi huu yanasomeka katika vifungu 119 na 120.

MRADI WA MPANGO WA UFUATILIAJI WA TATHMINI WENYE KULETA MATOKEO YA MKUZA II

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Mradi wa Mpango wa Ufuatiliaji wa Tathmini wenye Kuleta Matokeo ya MKUZA II uliidhinishiwa jumla ya TZS. 768.3 milioni. Hadi kufikia Machi 2015, Mradi huu umeingiziwa TZS. 224.4 milioni sawa na asilimia 29.2 ya fedha zilizoidhinishwa.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2014/2015, mfumo wa ufuatiliaji na uwajibikaji umetayarishwa na kujadiliwa katika vikao mbali mbali vikiwemo vikao vya Tume ya Mipango. Mapendekezo ya Muundo mpya wa Idara ya Ufuatiliaji na Tathmini yamekubaliwa. Aidha, kupitia Mradi huu, maandalizi ya uandaaji wa Ripoti ya Utekelezaji wa MKUZA *AIR* 2013/2014 yameratibiwa. Kikundi kazi kilichoundwa na watalaamu kutoka sekta mbali mbali za Serikali na zisizo za Kiserikali tayari kimeanza kazi ya ukusanyaji wa taarifa husika.

MRADI WA KUJENGA UWEZO WA UTEKELEZAJI KWA TAASISI ZA SERIKALI

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Mradi wa Kujenga Uwezo wa Utekelezaji kwa Taasisi za Serikali uliidhinishiwa jumla ya TZS. 769.8 milioni. Hadi kufikia Machi 2015, Mradi huu umeingiziwa TZS. 907.5 milioni sawa na asilimia 117.9 ya fedha zilizoidhinishwa.

Mhe. Mwenyekiti, Rasimu ya Mpango Mkakati wa Tume ya Mipango imetayarishwa. Aidha, ukumbi wa mkutano ambao vile vile hutumika kwa ajili ya maktaba umefanyiwa matengenezo na umeanza kutumika. Mafunzo ya siku tatu ya uongozi katika fani ya '*coaching and mentoring*'yamefanyika kwa kuwajengea uwezo watendaji juu ya mbinu mpya na bora za uongozi shirikishi.

Mhe. Mwenyekiti, katika kukijengea uwezo Kitengo cha Kuratibu na Kufuatilia utekelezaji wa kazi za maabara *Results for Prosperity*, Afisa mmoja ameshiriki katika Maabara ya Huduma ya Afya, Tanzania Bara kwa kipindi cha wiki sita kwa lengo la kujifunza shughuli za kuandaa Maabara. Maelezo zaidi Mhe. Mwenyekiti, yanasomeka katika kifungu namba 126.

PROGRAMU YA MPANGO WA KURASIMISHA RASILIMALI NA BIASHARA ZA WANYONGE TANZANIA (MKURABITA)

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka fedha 2014/2015, Programu ya Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania iliidhinishiwa jumla ya TZS. 200.0 milioni. Hadi kufikia Machi 2015, Programu hii imeingiziwa TZS. 125.0 milioni sawa na asilimia 62.5 ya fedha zilizoidhinishwa.

Mhe. Mwenyekiti, zoezi la urasimishaji ardhi linaendelea katika Shehia ya Limbani Wete Pemba na usajili wa ardhi Chwaka umeanza kwa hatua za uhakiki na kufanya uchambuzi wa taarifa. Aidha, jumla ya fomu 650 zimewasilishwa kwa Mrajis wa Ardhi Pemba kwa ajili ya usajili wa ardhi. Sambamba na hayo, kazi ya ufuatiliaji kwa wafanya biashara waliopatiwa mafunzo ya uendeshaji na usimamizi

wa biashara kwa mwaka 2014 imefanyika ili kuweza kujua mwenendo wao na kuleta matokeo yaliyokusudiwa.

Mhe. Mwenyekiti, vikao vya Kamati ya Wataalamu ya MKURABITA vimefanyika kwa ajili ya kujadili ripoti za utekelezaji wa shughuli za Programu ya Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania pamoja na maeneo yaliyoteuliwa kufanyiwa Urasimishaji wa ardhi yakiwemo maeneo ya Jang'ombe na Chwaka kwa upande wa Unguja na Limbani, Kiungoni na Chokocho kwa upande wa Pemba.

MRADI WA KUIFANYIA MABADILIKO NA KUIMARISHA TUME YA MIPANGO

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Mradi wa Kuifanyia Mabadiliko na Kuimarisha Tume ya Mipango uliidhinishiwa jumla ya TZS. 150.0 milioni. Hadi kufikia Machi 2015, mradi huu umeingiziwa TZS. 125.4 milioni sawa na asilimia 83.6 ya fedha zilizoidhinishwa.

Mhe. Mwenyekiti, kazi ya utayarishaji wa Muundo wa Mfumo wa Usimamizi wa Programu na Miradi umekamilika. Aidha, mafunzo ya Mfumo huo yametolewa kwa Maofisa wa Tume ya Mipango ili kuwapa uelewa wa taarifa zitakazohitajika kuingizwa katika Mfumo huo. Sambamba na hayo, Maofisa wawili wamepatiwa mafunzo ya wiki mbili ya '*Project Contract Management'* na wawili '*Project Financial Management'* nchini Uganda kwa lengo la kuimarisha utendaji wa majukumu yao.

Mhe. Mwenyekiti, uandaaji wa tovuti yaani W*ebsite* ya Tume ya Mipango uko katika hatua za mwisho kukamilika ambapo Mshauri Elekezi aliyepewa jukumu la kufanikisha kazi hiyo tayari amewasilisha mwelekeo wa tovuti hiyo. Matengenezo ya ghala ya Tume ya Mipango yamekamilika na imeanza kutumika.

MRADI WA KUIMARISHA KITENGO CHA UTAFITI

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Mradi wa Kuimarisha Kitengo cha Utafiti uliidhinishiwa jumla ya TZS. 100.0 milioni. Hadi kufikia Machi 2015, Mradi huu umeingiziwa TZS. 57.0 milioni sawa na asilimia 57.0 ya fedha zilizoidhinishwa.

Mhe. Mwenyekiti, Idara imeratibu uandaaji wa maeneo ya tafiti kitaifa ambayo yamepewa kipaumbele katika kipindi cha miaka mitano ijayo. Kitabu kilichojumuisha maeneo ya vipaumbele vya tafiti kimetolewa. Maeneo ya tafiti yaliyoainishwa ndani ya kitabu hicho yameibuliwa na Sekta husika na kupitiwa

katika ngazi mbali mbali za Serikali kabla ya kuchapishwa. Kazi ya utayarishaji wa kitabu hicho imefanywa kwa mashirikiano kati ya Tume ya Mipango, Tume ya Sayansi na Teknolojia ya Tanzania yaani *COSTECH* na Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Mwenyekiti, matokeo ya tafiti zitakazofanywa kutokana na maeneo hayo, yataisaidia Serikali kufanya maamuzi sahihi ikiwa ni pamoja na kuandaa Sera zitakazozingatia matokeo ya tafiti zilizofanyika. Aidha, muongozo wa utekelezaji wa tafiti hizo umetayarishwa na Rasimu ya awali imetolewa kwa wadau kwa mazingatio. Vile vile, Mradi huu umeweza kuwapatia mafunzo ya muda mfupi nchini Uganda wafanyakazi wawili kuhusu mbinu za kuandaa na kufanya uchambuzi wa matokeo ya tafiti.

MRADI WA MASHIRIKIANO BAINA YA SEKTA YA UMMA NA SEKTA BINAFSI (*PPP*)

Mhe. Mwenyekiti, lengo kuu la Mradi huu ni kushajihisha ushiriki wa Sekta Binafsi katika Mipango ya Maendeleo. Fedha zilizotumika kwa mwaka wa fedha 2014/2015, zilitoka kwa Washirika wa Maendeleo, Benki ya Dunia na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika fedha zilizotengwa kwa *R4P*.

Mhe. Mwenyekiti, Serikali tayari imepitisha Sera na Rasimu ya Mswada wa Sheria ya Mashirikiano Baina ya Sekta ya Umma na Binafsi. Miongoni mwa vipaumbele vilivyoainishwa katika Sera ya *PPP* ni kuimarisha huduma za Kijamii ili kukuza uchumi na kuleta maendeleo endelevu kwa kushirikiana na Sekta Binafsi. Utekelezaji wa Sera hii utaiwezesha Serikali kufaidika na miradi ya mashirikiano kwa ufanisi. Aidha, utekelezaji wa Sera hii utaiwezesha Zanzibar kufaidika na teknolojia ya kisasa na ujuzi kupitia katika miradi itakayotekelezwa kwa mfumo wa mashirikiano.

Mhe. Mwenyekiti, Serikali tayari imeanza kuainisha miradi yenye tija inayoweza kutekelezwa kwa njia ya Mashirikiano Baina ya Sekta ya Umma na Binafsi. Miongoni mwa Miradi hiyo ni Mradi wa Uwanja wa Ndege, Bandari na Uvuvi wa Bahari Kuu.

MRADI WA UTAFITI WA HALI YA UTUMISHI NCHINI

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha wa 2014/2015, Mradi wa Utafiti wa Hali ya Utumishi Nchini uliidhinishiwa jumla ya TZS. 61.9 milioni. Hadi kufikia Machi 2015, Mradi huu umeingiziwa TZS. 4.1 milioni sawa na asilimia 6.6 ya fedha zilizoidhinishwa.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2014/2015, mikutano miwili ya Kamati ya Wataalamu iliojadili Rasimu ya ripoti ya utafiti wa hali ya utumishi nchini imefanyika. Hivi sasa, ripoti hiyo inafanyiwa mapitio ya mwisho kabla ya kuwasilishwa katika mikutano ya wadau Unguja na Pemba ili waweze kuweka mapendekezo yao.

MRADI WA KUOANISHA MASUALA YA IDADI YA WATU KATIKA AFYA YA UZAZI, JINSIA NA KUPUNGUZA UMASIKINI KATIKA MIPANGO YA MAENDELEO

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Mradi wa Kuoanisha Masuala ya Idadi ya Watu katika Afya ya Uzazi, Jinsia na Kupunguza Umasikini Katika Mipango ya Maendeleo uliidhinishiwa jumla ya TZS. 200.0 milioni. Hadi kufikia Machi 2015, Mradi huu umeingiziwa TZS. 124.2 milioni sawa na asilimia 62.1ya fedha zilizoidhinishwa.

Mhe. Mwenyekiti, kupitia Mradi huu, Ripoti ya Mwaka 2014 juu ya masuala ya Idadi ya Watu yenye ujumbe "Athari za Uhamiaji Mijini" inaendelea kutayarishwa. Sambamba na hilo, andiko la kitaalamu yaani *Thematic Paper* kuhusu athari za idadi ya watu katika maendeleo limeandaliwa. Ripoti ya andiko hilo tayari imejadiliwa katika mikutano ya wadau iliyofanyika Unguja na Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, Mradi pia umeendelea na uratibu wa mapitio ya Daftari la Shehia katika Shehia 30 za Wilaya mbili za Kaskazini 'A' Unguja na Wete Pemba. Katika kufanikisha Maadhimisho ya Siku ya Idadi ya Watu Duniani, mkutano wa Waandishi wa Habari kuelezea Siku ya Idadi ya Watu Duniani umefanyika. Aidha, Maofisa wawili wameshiriki katika mikutano minne ya matayarisho iliyofanyika Dar es Salaam na kushiriki katika Maadhimisho ya Siku ya Idadi ya watu Kitaifa yaliofanyika Mwanza.

MRADI WA UIMARISHAJI TAKWIMU TANZANIA (*STATCAP*)

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Mradi wa Uimarishaji Takwimu Tanzania uliidhinishiwa jumla ya TZS. 6,700.0 milioni. Hadi kufikia Machi 2015, Mradi huu umeingiziwa TZS. 2,549.6 milioni sawa na asilimia 38.1 ya fedha zilizoidhinishwa.

Mhe. Mwenyekiti, zoezi la ukusanyaji wa takwimu za Utafiti wa Uajiri na Mapato (*Employment and Earning Survey*, 2014) umekamilika na hatua inayofuata ni kufanya uchambuzi wa takwimu zilizokusanywa. Aidha, Afisi imeweza kutoa ripoti ya Utafiti wa Hali ya Uchumi na Kijamii, yaani *Socio-Economic Survey, 2014*.

Mhe. Mwenyekiti, kazi za ukusanyaji takwimu za Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya *Household Budget Survey 2014* zimeanza. Takwimu za miezi sita tayari zimekusanywa na zoezi la kuzifanyia uhakiki taarifa zilizokusanywa linaendelea ili ziweze kuingizwa kwenye kompyuta kwa uchambuzi. Aidha, takwimu za faharisi za bei ya mlaji zimeendelea kutolewa kwa kila mwezi pamoja na kutoa ripoti mbili za takwimu za Pato la Taifa za robo mwaka.

Mhe. Mwenyekiti, utaratibu wa ujenzi wa Makao Makuu ya Ofisi ya Mtakwimu Mkuu Zanzibar unatarajiwa kuanza mwanzoni mwa mwaka wa fedha ujao. Benki ya Dunia tayari imeshatoa ridhaa ya ujenzi huo ambao utagharimu TZS. 8,000.0 milioni.

Mhe. Mwenyekiti, Afisi imeendelea kuwajengea uwezo wafanyakazi wake sita ambao wanasomea Shahada ya Kwanza na ya Pili katika fani za Uchumi na Fedha, Takwimu na '*Geographical Information System*, yaani *GIS*. Aidha, Mradi umewawezesha wafanyakazi kuhudhuria vikao vya kitaalamu vya *MEFMI, SADC* na *EAC* na kupata taaluma pamoja na kuongeza ujuzi wa kazi. Aidha, maofisa 11 wamehudhuria vikao vilivyojadili Rasimu ya Mswada wa Sheria Mpya ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu.

MWELEKEO WA BAJETI INAYOTUMIA MFUMO WA PROGRAMU (*PBB*) YA OFISI YA RAIS NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016

Mhe. Mwenyekiti, Hotuba ya bajeti ya Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ya mwaka wa fedha 2015/2016 ni ya mwisho katika muhula huu wa kwanza wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya Awamu ya Saba mwaka 2010 - 2015. Juhudi za Serikali katika awamu hii zimefanikiwa sana katika kuimarisha maisha ya wananchi, kudumisha amani, umoja na utulivu. Aidha, Awamu hii pia imefanikiwa kuimarisha utawala bora kwa kujenga misingi ya Utawala Bora pamoja na kujenga uchumi madhubuti ambao ni endelevu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kulihakikishia Baraza lako Tukufu kuwa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi itaendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia maelekezo na miongozo madhubuti ambayo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Awamu ya Saba imeiandaa. Lengo ni kuhakikisha kuwa Zanzibar inapiga hatua zaidi za kimaendeleo pamoja na kudumisha mafanikio yaliyopatikana.

MAMBO MAKUU YATAKAYOTEKELEZWA NA OFISI YA RAIS NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI KWA MWAKA WA FEDHA WA 2015/2016

Mhe. Mwenyekiti, katika utekelezaji wa Programu zake Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi imeweka kipaumbele katika utekelezaji wa mambo yapatayo 15 kama yanavyooneshwa katika kifungu 151, naomba kwa haraka haraka niyasome:-

i. Kusimamia uundwaji wa Serikali baada ya Uchaguzi Mkuu;
ii. Kuimarisha misingi ya Utawala Bora, Demokrasia na Haki za Binadamu;
iii. Kusimamia ukuzaji wa uchumi na kutayarisha mpango wa maendeleo;
iv. Kuundwa kwa Idara ya Mashirikiano Baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi;
v. Kuunda Idara ya Ufuatiliaji na Tathmini katika Tume ya Mipango;
vi. Kuanza Utekelezaji wa Muongozo wa vipaumbele vya Utafiti vilivyoibuliwa na Sekta;
vii. Kuanza Utekelezaji wa kutumia *Model* ya "*Financial Programming"* kwa kufanya makadirio ya mapato na matumizi *Macro – Indicators Zanzibar*;
viii. Kuwajengea uwezo Watendaji ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi;
ix. Kuimarisha usalama katika Nyumba za Ikulu na Nyumba za Serikali;
x. Kuendelea na kukamilisha ujenzi wa nyumba ya Ikulu ndogo Micheweni;
xi. Kukamilisha na kuanza kuitekeleza Sera ya Diaspora;
xii. Kuwawezesha watendaji wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kushiriki katika majadiliano ya jumuiya za kikanda yenye kuleta tija kwa Zanzibar;
xiii. Kuendelea na ukaguzi wa hesabu za Mawizara na Taasisi za Serikali kwa mwaka 2014/2015;
xiv. Kujenga mashirikiano mazuri na jumuiya za ukaguzi za kanda *(AFROSAI-E, SADCOPAC)* na za Kimataifa *INTOSAI*); na
xv. Kushajihisha ukaguzi wa utekelezaji wa matokeoya malengo (*Audit of Performance).*

H: PROGRAMU KUU NA NDOGO ZA OFISI YA RAIS YA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi imeandaa bajeti ya 2015/2016 kufuata Mpango mpya wa Bajeti kutoka Mfumo wa "*Line Item Budget"* kwenda katika Mfumo wa bajeti inayozingatia matokeo *(Programme Based Budget).* Mfumo huu mpya wa uandaaji wa bajeti wa *PBB* unaonesha viashiria vya matokeo ya utekelezaji ambapo Taasisi zetu zitajipima kutokana na

viashiria vyake ikiwa zipo katika mwelekeo sahihi katika utekelezaji wa shughuli zake.

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi itakuwa na jumla ya Programu Kuu 15 sambamba na Programu Ndogo 21zitakazotekelezwa na Ofisi zifuatazo:-

i. Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora;
ii. Ofisi ya Baraza la Mapinduzi;
iii. Tume ya Mipango;
iv. Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali; na
v. Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi.

MALENGO NA MATOKEO YANAYOTARAJIWA KATIKA PROGRAMU KUU NA NDOGO PAMOJA NA MAKISIO YA FEDHA INAZOHITAJIKA

Mhe. Mwenyekiti, kwa ufupi sasa naomba niwasilishe Programu Kuu na Programu Ndogo zitakazotekelezwa katika mwaka wa fedha 2015/2016, malengo, matokeo yanayotarajiwa na fedha zinazohitajika katika kila fungu.

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora Fungu A01 ina jumla ya Programu Kuu tatu na Programu Ndogo saba kama ifuatavyo:-

1. Programu ya Kusimamia Shughuli za Mhe. Rais na Kuimarisha Mawasiliano Ikulu

Lengo kuu la Programu hii ni kuwaeleza wananchi na washirika wengine juu ya shughuli zinazotekelezwa, mafanikio na maendeleo yaliyofikiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kutumia njia mbali mbali zikiwemo vyombo vya habari. Aidha, Programu hii inalenga kuimarisha mawasiliano baina ya Serikali na wananchi kwa kuwapatia taarifa sahihi na kwa wakati muafaka. Matokeo ya utekelezaji wa Programu hii ni kuona kuwa umma na washirika wote kwa ujumla wanakuwa na uelewa mzuri kuhusu shughuli zinazotekelezwa na Serikali yao. Programu hii itakuwa na Programu Ndogo mbili zifuatazo:-

i. Programu Ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Mhe. Rais; na
ii. Programu Ndogo ya Uimarishaji wa Mawasiliano Baina ya Serikali na Wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, Programu hii itatekelezwa sambamba na Mradi wa Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Ikulu na Nyumba za Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, ili Programu ya Kusimamia Shughuli za Mhe. Rais na Kuimarisha Mawasiliano Ikulu iweze kutekelezwa, kwa mwaka wa fedha 2015/2016, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya TZS. 2,575.2 milioni kwa matumizi ya kazi za kawaida zilizopangwa katika Programu hii na TZS. 1,200.0 milioni kwa kazi za maendeleo.

2. Programu ya Utawala Bora na Usalama wa Watumishi wa Umma

Programu hii inalenga kuimarisha misingi ya Utawala Bora na Haki za Binadamu pamoja na kuimarisha usalama wa Watumishi wa Umma. Matokeo yanayotarajiwa katika utekelezaji wa Programu hii ni kuimarika kwa utawala bora katika sekta ya umma na sekta binafsi na usalama wa Serikali na Watumishi wake. Programu hii itakuwa na Programu Ndogo mbili zifuatazo:-

i. Programu Ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Utawala Bora; na
ii. Programu Ndogo ya Usimamizi wa Usalama wa Watumishi wa Umma.

Mhe. Mwenyekiti, ili Programu ya Utawala Bora na Usalama wa Watumishi wa Umma iweze kutekelezwa, kwa mwaka wa fedha 2015/2016, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya TZS. 216.0 milioni kwa matumizi ya kazi za kawaida zilizopangwa katika Programu hii.

3. Programu ya Utawala na Uendeshaji wa Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora

Programu hii ina malengo makuu mawili ambayo ni kuimarisha shughuli za Mipango, kuandaa na kuchambua Sera na Utafiti; na kuimarisha uwezo wa kiutendaji na uratibu wa shughuli za Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora. Matokeo yanayotarajiwa katika utekelezaji wa Programu hii ni kuwepo kwa mazingira mazuri ya utendaji kazi ambayo yatafanikisha utoaji wa huduma bora na maamuzi yatayotokana na matokeo ya utafiti. Programu hii itakuwa na Programu Ndogo tatu zifuatazo:-

i. Programu Ndogo ya Uratibu na Usimamizi wa Shughuli za Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora;
ii. Programu Ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Mipango, Sera na Utafiti za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi; na
iii. Programu Ndogo ya Uratibu na Usimamizi wa Shughuli za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi – Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, ili Programu ya Utawala na Uendeshaji wa Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora iweze kutekelezwa, kwa mwaka wa fedha 2015/2016, naliomba

Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya TZS. 2,151.9 milioni kwa matumizi ya kazi zilizopangwa katika Programu hii.

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Baraza la Mapinduzi Fungu A02 ina jumla ya Programu Kuu mbili na Programu Ndogo nne kama ifuatavyo:-

1. Programu ya Usimamizi wa Majukumu ya Kikatiba na Kisheria ya Baraza la Mapinduzi na Kamati ya Makatibu Wakuu

Lengo la Programu hii ni kutayarisha na kusimamia vikao vya Baraza la Mapinduzi na Kamati ya Makatibu Wakuu. Matokeo yanayotarajiwa kupitia programu hii ni kuimarika kwa Sheria, Sera na Miongozo yenye kusaidia uendeshaji wa Serikali, ukuaji uchumi na kupunguza umasikini. Programu hii itakuwa na Programu Ndogo nne zifuatazo:-

i. Programu Ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Shughuli za Baraza la Mapinduzi na Kamati zake;
ii. Programu Ndogo ya Tathmini ya Utendaji Kazi na Uwajibikaji wa Taasisi za Umma;
iii. Programu Ndogo ya Uimarishaji Uwezo wa Utendaji kwa Viongozi wa Ngazi za Juu Serikalini na Sekretarieti ya Baraza la Mapinduzi; na
iv. Programu Ndogo ya Kukuza Ufanisi wa Kitengo cha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano.

Mhe. Mwenyekiti, ili Programu ya Usimamizi wa Majukumu ya Kikatiba na Kisheria ya Baraza la Mapinduzi na Kamati ya Makatibu Wakuu iweze kutekelezwa, kwa mwaka wa fedha 2015/2016, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya TZS. 479.0 milioni kwa matumizi ya kazi zilizopangwa katika Programu hii.

2. Programu ya Uongozi na Utawala katika Ofisi ya Baraza la Mapinduzi

Programu hii inalenga kuimarisha mazingira ya kazi, mahusiano ya umma na kuwaongezea ujuzi wafanyakazi wa Ofisi. Matokeo yanayotarajiwa kupitia Programu hii ni kuimarika kwa mazingira ya kazi, uwajibikaji na utoaji bora wa huduma za kiofisi.

Mhe. Mwenyekiti, ili Programu ya Uongozi na Utawala wa Ofisi ya Baraza la Mapinduzi iweze kutekelezwa, kwa mwaka wa fedha 2015/2016, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya TZS.1,184.0 milioni kwa matumizi ya kazi zilizopangwa katika Programu hii.

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa Wazanzibari Wanaoishi Nchi za Nje Fungu A03 ina jumla ya Programu Kuu tatu kama ifuatavyo:-

1. Programu ya Kuratibu Ushirikiano wa Kikanda na Mashirika ya Kimataifa

Programu hii ina jukumu la kuiwezesha Zanzibar kushiriki katika mikutano ya kikanda na kimataifa. Matokeo yanayotarajiwa katika utekelezaji wa Programu hii ni kuimarika kwa ushiriki wa Zanzibar katika mikutano ya kikanda na kimataifa na kuhakikisha kuwa Zanzibar inanufaika na uhusiano huo.

Mhe. Mwenyekiti, ili Programu ya Kuratibu Ushirikiano wa Kikanda na Mashirika ya Kimataifa iweze kutekelezwa, kwa mwaka wa fedha 2015/2016, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya TZS. 389.7 milioni kwa matumizi ya kazi za kawaida zilizopangwa katika Programu hii.

2. Programu ya Uratibu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar n mm kwa Wazanzibari Wanaoishi Nchi za Nje

Lengo kuu la Programu hii ni kuwashirikisha ipasavyo Wazanzibari wanaoishi nje ya nchi katika maendeleo yakiuchumi na kijamii ya nchi yao. Matokeo yanayotarajiwa katika utekelezaji wa Programu hii ni Zanzibar kufaidika na michango ya Wazanzibari wanaoishi nje ya nchi katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

Mhe. Mwenyekiti, ili Programu ya Kuwashajihisha Wazanzibari Wanaoishi nchi za Nje kuwekeza na kuchangia katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii iweze kutekelezwa, kwa mwaka wa fedha 2015/2016, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya TZS. 112.1 milioni kwa matumizi ya kazi zilizopangwa katika Programu hii.

3. Programu ya Utawala na Uendeshaji wa Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa Wazanzibari Wanaoishi Nchi za Nje

Lengo kuu la Programu hii ni kuimarisha maslahi ya wafanyakazi, mazingira ya kazi na kuwajengea uwezo wafanyakazi wa Idara ili kuimarisha ufanisi katika utoaji wa huduma. Matokeo yanayotarajiwa katika utekelezaji wa Programu hii ni kuwepo kwa mazingira mazuri ya utendaji kazi ambayo yatafanikisha utoaji wa huduma bora.

Mhe. Mwenyekiti, ili Programu ya Utawala na Uendeshaji wa Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa Wazanzibari Wanaoishi Nchi za Nje iweze kutekelezwa, kwa mwaka wa fedha 2015/2016, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya TZS. 161.6 milioni kwa matumizi ya kazi ilizopangwa katika Programu hii.

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Tume ya Mipango Fungu A04 ina jumla ya Programu Kuu tatu na Programu Ndogo tano kama ifuatavyo:-

1. Programu ya Kuratibu Mipango ya Kitaifa na Maendeleo ya Watendakazi

Programu hii malengo yake makubwa ni kuimarisha Uratibu wa Mipango ya Maendeleo na kufanya ufuatiliaji na tathmini ya Mipango. Matokeo ya Programu hii ni kuimarisha ufanisi katika utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Zanzibar. Programu hii ina Programu Ndogo tatu nazo ni:-

i. Programu Ndogo ya Uratibu wa Mipango ya Kitaifa na Kupunguza Umaskini;
ii. Programu Ndogo ya Maendeleo ya Watendakazi na Masuala ya Idadi ya Watu;na
iii. Programu Ndogo ya Tathmini na Ufuatiliaji wa Mipango ya Maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, Programu hii itatekelezwa sambamba na Miradi ifuatayo:-

a) Mradi wa Kuifanyia Mabadiliko na Kuimarisha Tume ya Mipango;
b) Programu ya Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge (MKURABITA); na
c) Mradi wa Kujenga Uwezo wa Utekelezaji kwa Taasisi za Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, ili Programu ya Kuratibu Mipango ya Kitaifa na Maendeleo ya Watendakazi iweze kutekelezwa, kwa mwaka wa fedha 2015/2016, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya TZS. 704.1 milioni kwa matumizi ya kazi za kawaida zilizopangwa katika Programu hii na TZS. 1,120.9 milioni kwa kazi za maendeleo.

2. Programu ya Usimamizi wa Uchumi Mkuu

Mhe. Mwenyekiti, Programu hii lengo lake ni kuandaa Sera madhubuti za kiuchumi na Sera za kodi na kufanya tafiti za kiuchumi na kijamii kutokana na vipaumbele vya Taifa. Matokeo ya Programu hii ni Zanzibar kuimarika kwa Viwanda vidogo vidogo na vya kati. Aidha, kuwa na huduma bora za miundombinu ya kiuchumi na kijamii kwa kupitia idadi ya miradi inayoratibiwa katika mfumo wa mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi.

Programu hii ina Programu Ndogo mbili nazo ni:-
i. Programu Ndogo ya Ukuzaji Uchumi na Sera za Kodi; na
ii. Programu Ndogo ya Mashirikiano Baina ya Sekta ya Umma na Binafsi

Mhe. Mwenyekiti, Programu hii itatekelezwa sambamba na Miradi ifuatayo:-

a) Mradi wa Kuimarisha Kitengo cha Utafiti; na
b) Mradi wa Uimarishaji Takwimu Tanzania (*STATCAP*).

Mhe. Mwenyekiti, ili Programu ya Usimamizi wa Uchumi Mkuu iweze kutekelezwa, kwa mwaka wa fedha 2015/2016, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya TZS. 1,975.6 milioni kwa matumizi ya kazi zilizopangwa katika Programu hii kwa kazi za kawaida na TZS. 11,597.3 milioni kwa kazi za maendeleo.

3. Programu ya Utawala na Uendeshaji wa Tume ya Mipango

Programu hii lengo lake ni kuhakikisha kazi zote za Tume ya Mipango zinatekelezwa kwa umakini na ufanisi. Matokeo ya muda mfupi ni ufanisi wa kazi za Tume ya Mipango umeimarika kwa kuwepo kwa wafanyakazi wenye ujuzi na wanaoweza kutoa huduma kwa ufanisi.

Mhe. Mwenyekiti, ili Programu ya Utawala na Uendeshaji wa Tume ya Mipango iweze kutekelezwa, kwa mwaka wa fedha 2015/2016, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya TZS. 931.0 milioni kwa matumizi ya kazi zilizopangwa katika Programu hii.

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Fungu A05 ina jumla ya Programu Kuu mbili na Programu Ndogo mbili kama ifuatavyo:-

1. Programu ya Udhibiti wa Fedha na Rasilimali za Umma

Lengo la Programu hii ni kusimamia uwazi na uwajibikaji katika matumizi ya fedha na rasilimali za umma. Matokeo ni kuwa na ufanisi katika huduma za Umma na Utawala Bora.

Mhe. Mwenyekiti, ili Programu ya Udhibiti wa Fedha na Rasilimali za Umma iweze kutekelezwa, kwa mwaka wa fedha 2015/2016, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya TZS. 1,101.9 milioni kwa matumizi ya kazi zilizopangwa katika Programu hii.

2. Programu ya Utawala na Uendeshaji wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali

Lengo la Programu hii ni kuijengea uwezo Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Matokeo ni kuwa na mazingira mazuri ya kazi. Programu hii ina Programu Ndogo mbili kama ifuatazo:-

i. Programu Ndogo ya Usimamizi na Uendeshaji wa Udhibiti na Ukaguzi; na
ii. Programu Ndogo ya Udhibiti na Ukaguzi Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, ili Programu ya Utawala na Uendeshaji wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali iweze kutekelezwa, kwa mwaka wa fedha 2015/2016, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya TZS. 1,239.7 milioni kwa matumizi ya kazi zilizopangwa katika Programu hii.

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Fungu A06 ina jumla ya Programu Kuu mbili kama ifuatavyo:-

1. Programu ya Kupunguza Matendo ya Rushwa na Uhujumu wa Uchumi

Lengo la Programu hii ni kuzuia vitendo vya rushwa na kukuza uelewa wa wananchi juu ya madhara ya rushwa na uhujumu wa uchumi. Matokeo yanayotarajiwa kupatikana kutoka Programu hii ni kupunguza kwa vitendo vya Rushwa na Uhujumu wa Uchumi nchini.

Mhe. Mwenyekiti, ili Programu ya Kupunguza Matendo vya Rushwa na Uhujumu wa Uchumi iweze kutekelezwa, kwa mwaka wa fedha 2015/2016, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya TZS. 111.6 milioni kwa matumizi ya kazi zilizopangwa katika Programu hii.

2. Programu ya Utawala na Uendeshaji Katika Mapambano ya Rushwa na Uhujumu wa Uchumi

Lengo la Programu hii ni kutoa huduma bora za kiutawala na kiuendeshaji katika Ofisi ya Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar, ili kuongeza ufanisi na ubora wa kiutendaji katika kudhibiti, kuchunguza na kutoa elimu ya madhara ya rushwa na uhujumu wa uchumi. Matokeo yanayotarajiwa katika utekelezaji wa Programu hii ni kuwepo kwa mazingira mazuri ya utendaji kazi ambayo yatafanikisha utoaji wa huduma bora.

Mhe. Mwenyekiti, ili Programu ya Utawala na Uendeshaji Katika Mapambano ya Rushwa na Uhujumu wa Uchumi iweze kutekelezwa, kwa mwaka wa fedha

2015/2016, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya TZS. 725.6 milioni kwa matumizi ya kazi zilizopangwa katika Programu hii.

Mhe. Mwenyekiti, maelezo ya kina ya Programu Kuu na Programu Ndogo za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi yameainishwa katika Kitabu cha MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA BAJETI INAYOTUMIA PROGRAMU (*PBB*) KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016 – 2017/2018, *VOLUME – I* hayo mabuku makubwa, kitabu kilichotolewa na Wizara ya Fedha. Maelezo hayo yapo kuanzia ukurasa 41 hadi ukurasa 102.

J: MAPATO NA MAOMBI YA FEDHA KWA PROGRAMU ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016

J.1 MAPATO

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka 2015/2016, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi imekadiria kukusanya mapato ya kiasi cha TZS. 28.2 milioni. Kiasi hiki kitatokana na Makusanyo ya Ada ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali kupitia Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Zanzibar.

J.2 MAOMBI YA FEDHA KWA KAZI ZILIZOPANGWA UTEKELEZWA KATIKA MWAKA WA FEDHA 2015/2016

Mhe. Mwenyekiti, ili kuiwezesha Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kutekeleza Programu zilizoandaliwa kwa mwaka wa fedha 2015/2016, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha makadirio ya matumizi ya Programu za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi pamoja na Taasisi zake zenye jumla ya TZS. 27,977.2 milioni. Kati ya fedha hizo, TZS. 14,059.0 milioni kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na TZS. 13,918.2 milioni kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za maendeleo. Mgawanyo wa fedha zitakazotumika kwa utekelezaji wa kila Programu zimeainishwa katika Kiambatanishonamba 11.

K: HITIMISHO

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kuhitimisha hotuba yangu, naomba kusisitiza suala muhimu ambalo wengi wetu wameshalizungumza la kudumisha Amani na Utulivu wakati tukielekea katika harakati za Uchaguzi Mkuu mwezi Oktoba, 2015. Sote tutambue kuwa Amani na Utulivu ni tunu na hazina kubwa ambayo Mwenyezi Mungu ametujaalia. Amani na Utulivu zikitoweka zina gharama kubwa kuzirejesha na hata pale zinaporejea huchukua miaka mingi kuimarika tena. Ninawaomba Waheshimiwa Wajumbe na Wananchi wote kwa ujumla kuithamini Amani na Utulivu tulionayo na tuienzi kwa gharama yoyote ile.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumshukuru Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein kwa uvumilivu, ustahamilivu na moyo wake wa dhima kuiona Zanzibar siku zote ipo tulivu na inasonga mbele kwa maendeleo. Namuomba Mwenyezi Mungu amjaalie maisha marefu na afya njema ili aendelee kutuongoza katika miaka mitano mengine ijayo. Aidha, naomba kumshukuru kwa dhati kabisa Mhe. Rais kwa kuniamini na kuniteua kushika wadhifa wa Uwaziri katika kipindi hiki cha Awamu ya Saba anayoiongoza. Hii ni heshima kubwa kwangu binafsi na wananchi wote wa Jimbo langu la Dimani, ambao kuendelea kwao kuniamini ni chachu ya maendeleo katika Jimbo hili.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia, naomba kuwasilisha salamu za pongezi kwa Mhe. Rais kutoka kwa wananchi wa Jimbo la Dimani zinazoeleza kuwa wamefarijika sana na uongozi wake katika kipindi chote cha miaka mitano ya Awamu yake na wanamuomba aendelee kuiongoza tena nchi hii kwa kipindi kijacho.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mara nyengine, nachukua fursa hii kutoa shukurani zangu za dhati kwako wewe pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza lako Tukufu kwa ushirikiano mkubwa mlionipa katika kipindi chote cha miaka mitano. Ushirikiano wenu umeiwezesha Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kufanikisha utekelezaji wa majukumu yake kwa ufanisi mkubwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa mkutano huu wa 20 itakuwa ni mara yetu ya mwisho kukutana katika Baraza la Nane, nawatakia kila la kheri Waheshimiwa Wajumbe wote. Wale ambao wameamua kwenda kuomba ridhaa ya wananchi tena, tutakiane mafanikio mema pamoja na mimi mwenyewe. Aidha, kwa wale ambao wameamua kustaafu, nawatakia maisha yenye furaha na tuwe pamoja katika kuijenga nchi yetu. Nawaombea nyote kwa Mwenyezi Mungu awajaalie umri mrefu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa kipindi cha miaka mitano ni muda mrefu, bila ya shaka mijadala yetu katika Baraza ilikuwa na mitazamo tofauti. Sote tunaamini kuwa yale yote yaliyofanyika katika Baraza hili yalikuwa na lengo la kuleta maendeleo kwa Wazanzibari. Inawezekana pia katika mijadala yetu baadhi ya wakati iliwagusa baadhi ya watu ambao hawakuifurahia. Hivyo, naomba kuchukua fursa hii kuwaomba tusameheane na tufungue ukurasa mpya kama Wazanzibari.

Mhe. Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee ninawashukuru watendaji wote wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa ushirikiano wao mkubwa walionipa katika kutekeleza majukumu mbali mbali ya Ofisi hii. Kwanza, Katibu Mkuu Kiongozi na Katibu Baraza la Mapinduzi, Dkt. Abdulhamid Yahya Mzee na Naibu Katibu Baraza la Mapinduzi, Ndugu Salmin Amour Abdalla wote wanastahiki pongezi maalum kwa uwajibikaji wao mkubwa na wenye kupigiwa

mfano. Nawashukuru pia Katibu Mkuu wangu Ndugu Salum Maulid Kibanzi, Naibu Katibu Mkuu Ndugu Said A. S. Natepe, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Ndugu Fatma Mohammed Said, Katibu Mtendaji Tume ya Mipango Ndugu Amina Khamis Shaaban, Katibu wa Rais Ndugu Haroub Shaib Said na Naibu wake Ndugu Maryam Haji Mrisho, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Ndugu Mussa, Mnikulu, Mhasibu Mkuu, Ofisa Mdhamini Pemba Bi. Jokha, Wakurugenzi na wafanyakazi wote wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa ujumla wao, wote ninasema ahsanteni sana kwa utendaji wenu. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuchukua nafasi hii kuyashukuru mashirika ya Kimataifa kwa ushirikiano wao mzuri na Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa misaada yao iliyoiwezesha na kuisaidia Zanzibar kuimarisha maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Mashirika haya yanajumuisha Jumuiya ya Nchi za Ulaya *(EU), UNDP, UNFPA, World Bank, UNICEF, AfDB, IOM* na *BADEA*. Aidha, naomba kutoa shukurani zangu kwa Jumuiya za Kikanda zikiwemo *COMESA, SADC, EAC, AU*, na *ACP*. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2015/2016, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi itaendelea kuwa na ushirikiano mzuri na wa karibu na nchi rafiki na Mashirika ya Kikanda na Kimataifa yanayosaidia utekelezaji wa majukumu ya Ofisi yangu na Serikali kwa ujumla. Aidha, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi itaendeleza ushirikiano mzuri uliopo kati yake na sekta nyengine hasa Sekta Binafsi ambazo zinachangia katika kutoa huduma bora kwa wananchi na kuchangia kukua kwa uchumi wa nchi hii.

Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima kubwa naomba kutoa hoja.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri, kabla hujatoa hoja, hujaomba fungu la fedha kwa Wajumbe hawa la ujumla.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Nimetaja mafungu mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti: Umeshaomba eeh! Haya *Inshaallah*, ya ujumla hatujaiona hapa lakini *Inshaallah*.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Naam!

Mhe. Mwenyekiti: Lakini *Inshaallah.*

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Eeh! nimetaja humu. eeh! zote hakusikia. Mhe. Mwenyekiti, nimetaja.

Mhe. Mwenyekiti: Tuendelee Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Nimetaja hapa Mhe. Mwenyekiti. Ngoja nitarudia kuondoa wasi wasi wako, nimetaja bwana.

Maombi ya fedha kwa kazi zilipangwa kutekelezwa kwa mwaka 2015/2016, Kifungu 181 Mhe. Mwenyekiti, nimekisoma.

Mhe. Mwenyekiti: Sawa tuendelee.

Waheshimiwa Wajumbe, kwa muda tulionao ilikuwa sasa tumkaribishe Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Viongozi Wakuu wa Serikali aje kutoa taarifa yake, lakini muda ni mdogo. Kwa hivyo, hautoshi. Lakini pia ilikuwa kuna nafasi ya Mwenyekiti wa *PAC* naye. Sasa kwa vile muda hautoshi na kuna taarifa ya Serikali juu ya suala la Micheweni, tumkaribishe basi Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ili aweze kutoa taarifa hiyo na baadae tusitishe shughuli zetu hadi jioni.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi. Ni maelezo mafupi tu kutokana na yaliyojitokeza asubuhi hii.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kuwasiliana na Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Kaskazini, alielezea kuwa siku ya tarehe 23/05/2015 majira ya usiku kati ya saa mbili na saa tatu usiku kulitokea tafrani katika nyumba ya Bwana Hamad Faki Kombo kwenye Kijiji cha Kwale Wilaya ya Micheweni, jambo ambalo lilisababishwa na kutaka kushushwa kwa bendera katika nyumba yake; bendera ya Chama cha CUF.

Lakini baada ya kufika kwa Polisi tafrani hiyo ilidhibitiwa na watu walitawanyika. Hata hivyo, Polisi walianzisha kesi na leo hii watuhumiwa wanne walipelekwa Mahakamani. Kwa hivyo, kwa sababu jambo lenyewe tayari lipo katika mkondo wa sheria hatuna haja sasa kuliendeleza. Kwa hivyo, lipo Mahakamani, tusubiri mkondo wa sheria uchukue nafasi yake.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Waziri, kwa taarifa yako hii ambayo umeitoa inayotokana na lile tatizo lilitokea pale asubuhi. Tukimaliza hapo kuna taarifa

nyengine ile ambayo tuliwahi kuitoa jana, sasa tunaisisitiza, wale Wajumbe wa Jumuiya ya UWAWAZA Kamati Tendaji wanaomba tukisitisha kikao hichi wakutane juu katika *hall* kubwa.

Baada ya maelekezo hayo sasa, kwa heshima na taadhima ninakushuruni sana kwa mashirikiano ambayo mumenipa, *Inshaallah* tutaendelea shughuli zetu jioni ya leo saa 11:00 barabara kwa kushirikiana na Mhe. Naibu Spika.

Kwa hivyo, naomba kusitisha shughuli hizi hadi saa kumi na moja jioni.

(Saa 6.50 mchana Baraza liliahirishwa hadi saa 11.00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, majadiliano yanaendelea huku nina jina la Mhe. Makame Mshimba Mbarouk. Waheshimiwa Wajumbe, kidogo juu huko hakukuwekwa vizuri, sasa tunamwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa.

Mhe. Shadya Mohammed Suleiman (Kny: Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa): Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kukutana kwa mara nyengine katika kikao hichi cha bajeti cha mwaka 2015/2016 tukiwa hai na wazima wa afya, ambayo ni neema kubwa kwetu aliyotujaalia *Allah* (*S.W*) kwa lengo la kujadili bajeti ya mwaka 2015/2016 kwa nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, pia, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kuweza kunipatia nafasi hii mbele ya Baraza lako tukufu, kuweza kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, juu ya utekelezaji wa Bajeti kwa Ofisi ya Rais, Ikulu na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Mhe. Naibu Spika, naungana na wenzangu kwa kumpa pole Mhe Rais wetu wa Zanzibar kwa kufiliwa na dada yake mpenzi, hayo ni majaaliwa yake *Subhanahu Wataalah*, kwa hiyo, tunawaomba familia wawe na subira na tunamuomba Mwenyeezi Mungu amlaze mahali pema peponi. *Amin.*

Mhe. Naibu Spika, kabla ya kuwasilisha maoni ya kamati vile vile napenda kutoa mkono wa pole kwa wale wote walioathirika na maafa ya mvua zinazoendelea kunyesha, ambapo tunawataka wawe na subra katika kipindi hiki kigumu, kwani ni mipango ya Mwenyezi Mungu aliyotuletea sisi waja wake.

Mhe. Naibu Spika, kwanza kwa niaba ya kamati naomba kumpongeza sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa kuweza kutuongoza katika kipindi chake hiki cha mwanzo cha miaka mitano, kipindi ambacho kimeshuhudia mabadiliko makubwa ya kisiasa na kiuchumi; kwani amekabidhiwa kuiongoza Serikali ya Zanzibar yenye mfumo mpya kabisa duniani yenye Mfumo wa Umoja wa Kitaifa, ambayo bila ya kuyumba ameiongoza kwa umahiri na utulivu mkubwa ambapo hadi hivi sasa anamaliza kipindi hiki cha mwanzo nchi yetu iko katika amani na utulivu mkubwa, huku wananchi wote wa Zanzibar wakiendelea na shughuli zao bila ya bughudha ya aina yoyote.

Mhe. Naibu Spika, pongezi zetu nyingine kwa Rais wetu ni kwa kuanzisha utaratibu wa serikali yetu wa kujitathmini katika utekelezaji wa mipango yake kwa kila kipindi cha miezi mitatu maarufu kama (Bango Kitita). Pamoja na matatizo madogo madogo, lakini mpango huu umeanza kuleta matunda, kwani leo hii uchumi wetu umeimarika kwa kiasi kikubwa hapa nchini. Kwa hiyo, hatuna budi kumpongeza sana Mhe. Rais wetu kwa mipango imara, isipokuwa tunamuomba awe mkali pale wanapotokea wachache kurejesha nyuma yale anayoyapanga.

Mhe. Naibu Spika, Rais wetu wakati wa Kampeni zake za Uchaguzi na mara tu baada ya kuapishwa na kukabidhiwa kuiongoza nchi yetu, alitoa ahadi kuwa yeye akichaguliwa kuiongoza Zanzibar basi moja ni kuhakikisha ataiongoza nchi kwa kufuata Katiba na Sheria. Na kweli, kwani hayo yote tumeyashuhudia, kwani tayari ndani ya kipindi chake ameweza kuunda Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa na Uhujumu wa Uchumi hapa Zanzibar. Pia, ameweza kuunda Tume ya Kuchunguza na Kusimamia Maadili ya Viongozi wa Umma. Taasisi hizi zote zimeanza kufanya kazi. Hivyo, hayo yote ni misingi mikuu ya utawala bora, kwani taasisi hizi kisheria ziko huru kufanya kazi zake bila ya kuingiliwa na mtu.

Mhe. Naibu Spika, kamati pia inapenda kumshukuru Mhe Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Ikulu na Utawala Bora pamoja na watendaji wa ofisi hii kwa utendaji mzuri wa kazi zao, ambao umepelekea kamati kuweza kutekeleza majukumu ya kazi zake za kila siku kwa ufanisi mzuri katika kipindi chote cha miaka mitano.

Hata hivyo, napenda kuishukuru ofisi hii kwa kuweza kuwasilisha mbele ya Baraza lako tukufu bajeti ya wizara yao kwa mwaka 2015/2016 kwa umahiri mkubwa katika mfumo mpya wa *PBB*. Kamati yangu inaungana na waziri alivyompongeza Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuweza kuiongoza Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuweza kumaliza ngwe yake ya miaka kumi, ambapo ndani ya ahadi zake za mwanzo ilikuwa ni kumaliza mgogoro wa kisiasa Zanzibar.

Kwa kweli kauli yake hiyo aliyoitoa Bungeni katika ufunguzi wa Bunge la mwanzo la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hakuna atakayebisha, leo hii Zanzibar hakuna tena mgogoro wa kisiasa, lakini pia Dkt. Jakaya Kikwete baada ya kusikia kilio cha muda mrefu hasa cha wananchi wa Zanzibar kwenye kero za Muungano, tunamshukuru Rais wetu wa Muungano kwa kushirikiana na Rais wa Zanzibar kwa kuwaruhusu wananchi wetu kupendekeza nini kifanyike ili kuondoa kero za Muungano na hivi sasa na *Alhamdulillah*, tayari Katiba inayopendekezwa imeshakuwepo, tunaamini wananchi wote wa Tanzania tutaipigia kura ili kuweza kuijenga Jamhuri ya Muungano yenye matumaini mapya.

Tunaamini katiba hiyo itatoa fursa kubwa za kiuchumi hapa Zanzibar ambapo mwanzo hazikuwepo. Kwa niaba ya kamati tunamuomba Mhe. Waziri aweze kutupelekea salamu zetu hizo kwa Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano kwa maandishi na pia amwambie kuwa tunamuombea maisha mema ya kustaafu kwake na kumtakia umri mrefu wenye afya njema.

Mhe. Naibu Spika, kamati inaipongeza serikali kupitia Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa na Wazanzibari wanaoishi nje ya nchi kwa kazi nzuri wanazozifanya, kwa kuiwakilisha Zanzibar katika vikao mbali mbali vya kikanda na Jumuiya. Lakini pia kuanza utaratibu wa kuwatafuta na kuwaorodhesha Wazanzibari wanaoishi nchi za nje ili kuwatambua na kutafuta njia za kushirikiana nao katika maendeleo ya kiuchumi hapa Zanzibar.

Pamoja na pongezi hizo, kamati imepitisha fungu la idara hii kwa shingo upande, kwani pesa zilizotengwa ni chache, kwani kuna uwezekano mkubwa wakashindwa kushiriki vikao vingi hasa vile vya Sekretarieti kwani wao wanakuwa ndio wapishi au waandaaji wakubwa wa agenda na mipango ambayo baada ndio waziri husika huja kujadili na kutia saini. Pia, pesa hizo hazitoweza kuwatosheleza kutembea sehemu mbali mbali duniani ili kupata nafasi ya kuwaona na kuzungumza na Wazanzibari hao kwa kujadili na kuangalia fursa kwa upande wa Zanzibar.

Mhe Naibu Spika, kwakua serikali yetu hivi sasa kwa makusudi tumeamua kuwashirikisha *Diaspora* katika maendeleo ya nchi yetu, basi kamati yangu inaishauri serikali kuweza kutoa *special offer* kwa Wazanzibari wote waishio nchi za nje kuingia nchini bila ya kulipa *viza*, kwani tumeona baadhi ya nchi duniani wameweza kuwaruhusu *Diaspora* wao kuingia katika nchi zao bila ya kulipia *viza* ili kuweza na wao kujisikia kua damu yao kwa nchi yao inathaminiwa, vile vile, kuweza kupewa kadi maalum kama vile *permit* maalum ya kuweza kukaa nchini kwa muda mrefu zaidi kulinganisha na wageni wengine. Jambo hili litaweza kuwavutia na kuwafanya kuongeza mapenzi kwa nchi yao.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa tunamalizia kipindi hiki cha miaka mitano ya mwanzo kwa Serikali hii ya Awamu ya Saba haitokuwa vyema kutokuwapa pongezi zetu za dhati kwa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu Zanzibar wakiongozwa na Mwanamama shupavu, muadilifu, asiyeyumba wala kubabaika, kwa kuweza kuiongoza taasisi hiyo na kuweza kuisaidia sana Kamati yetu ya *PAC*, kwani bila ya afisi hii ya *CAG*, basi kamati hiyo isingeweza kujua na kufichua manyago na ubadhirifu wa pesa za umma, lakini kazi yao kubwa imelisaidia sana Baraza lako hili kuweza kuisimamia vizuri serikali. Kwa hivyo, tunatoa pongezi na wito, *Inshaallah* Mwenyezi Mungu awajaalie nguvu na moyo wa kufanyakazi na tukijaaliwa mwakani basi tuendelee kutumia maarifa yao katika kulinda mali za umma.

Pia, tunawapongeza kwa kuimarisha majengo yao kwa Unguja na Pemba, pongezi pia kwa kuweza kuwapa fursa vijana wake kwa kujiendeleza na kuweza kuzalisha wataalamu wake mwenyewe bila ya kutegemea kuajiri wataalamu kutoka nje ya ofisi hii na wengine inafaa waende wakaige kwa *CAG*.

Mhe. Naibu Spika, pia, kamati inatoa pongezi kwa Tume ya Mipango ambayo Mhe. Rais yeye mwenyewe ndiye Mwenyekiti, ambapo wasimamizi wakuu katika utendaji pia inaongozwa na Mwanamama shupavu, mtaalamu aliyebobea katika masuala ya mipango pamoja na Kamishna, ambao kwa kweli tumeona matunda yao, kwani hata huu Utaratibu wa *PBB* ni matunda ya tume hii.

Kwa kweli tume hii ndio moyo wa mipango yote ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kamati yangu inaipongeza serikali kupitia Tume ya Mipango kwa kuleta sheria ya *PPP*. Tunaiomba serikali kama tulivyoshauri kwenye kamati kuwa serikali yetu itafute wawekezaji wenye uwezo katika miradi ya *PPP*, ili kuhakikisha nchi yetu inapiga hatua kubwa za maendeleo na kiuchumi hapa Zanzibar, kwani tunaamini miradi hiyo ndiyo itakayotoa ajira nyingi na tija kwa nchi yetu hapo baadae.

Mhe. Naibu Spika, ili kuwapa nafasi wajumbe wengine kuweza kuogelea katika mafanikio ya Afisi hii ya Rais, basi naomba nimalizie hapa kwa leo hii.

Mhe. Naibu Spika, kamati kwa mara nyengine inawapongeza Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais na Mhe. Mwakamu wa Pili wa Rais, kwa kuweza kumshauri vizuri Rais wetu katika kuiweka nchi yetu katika amani na utulivu, lakini pia kuiongoza kwa busara na kuimarika kwa uchumi wa nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, aidha, nitakuwa mwizi wa fadhila nisipowashukuru Wajumbe wa Kamati kwa kazi kubwa waliyoifanya kwa muda wote wa kipindi cha miaka mitano. Ushirikiano wao pamoja na moyo wa dhati katika kutekeleza majukumu

yao katika kufanikisha kazi za kamati ikiwemo hii ya kuchambua na kuijadili bajeti ya Ofisi ya Rais, Ikulu na Utawala Bora. Sasa kwa ruhusa yako Mhe. Naibu Spika, naomba niwatambue Wajumbe wa Kamati kama ifuatavyo:-

1.	Mhe Hamza Hassan Juma	Mwenyekiti
2.	Mhe. Saleh Nassor Juma	Makamu Mwenyekiti
3.	Mhe. Ali Mzee Ali	Mjumbe
4.	Mhe. Ashura Sharif Ali	Mjumbe
5.	Mhe.Shadya Mohammed Suleiman	Mjumbe
6.	Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Mjumbe
7.	Mhe. Subeit Khamis Faki	Mjumbe
8.	Ndg.Rahma Kombo Mgeni	Katibu
9.	Ndg.Othman Ali Haji	Katibu

Mhe. Naibu Spika, baada ya utangulizi huo naomba kutoa maoni ya kamati kwa Ofisi ya Rais, Ikulu na Utawala Bora kwa bajeti hii ya mwaka 2015/2016 kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, kamati inapenda kuipongeza Ofisi ya Rais kwa kutekeleza kwa kiasi mpango wa bajeti kwa mwaka 2014/2015 ambapo imeweza kufanya mambo mengi mazuri ambayo yameweka misingi ya uchumi imara na endelevu, pamoja na mambo mengine mbali mbali ikiwemo kuandaa Rasimu ya Sera ya *Diaspora*, kuanzisha Sheria ya *PPP* ambayo ndio ufunguo wa maendeleo kwa nchi yetu, kukamilisha ujenzi wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kuanza kutumika kwa Ikulu ya Kibweni na Ikulu ya Mkoani, kufanya matengenezo ya Ofisi ya Afisa Mdhamini Pemba ambayo ilikuwa ni kilio cha muda mrefu kwa upande wa Pemba na mambo mengine mengi ambayo kamati imeona ni hatua nzuri iliyofikiwa na ofisi hii, kwa vile kulikuwa na mambo ya muda mrefu hayajafanyiwa kazi, lakini kwa sasa yameweza kutekelezwa kwa kiasi kikubwa ambapo kamati inatoa pongezi kwa utekelezaji huo.

Mhe. Naibu Spika, lakini kamati bado pia inaendelea kuihimiza wizara iendelee kuyatekeleza yaliyobakia; ikiwemo ujenzi wa *Rest House* ya Micheweni na *Rest House* ya Fumba ikiwemo kujenga ukuta wa kuzuia mmong'onyoko kwa upande wa baharini kwa lengo la kuleta ufanisi wa majukumu yao japo kuwa utekelezaji huo kwa kiasi kikubwa unakwamishwa kutokana na uingizwaji mbaya wa fedha na kupelekea kutofikiwa kwa malengo yaliyokusudiwa na wizara. Kamati inaamini kwa utaratibu huu mpya wa *PBB* tunategemea mwakani mambo yatakwenda vizuri.

Mhe. Naibu Spika, kamati pia imeridhishwa na utekelezaji wa miradi kwa mwaka 2014/2015 ambapo Ofisi ya Rais imeweza kutekeleza ikiwemo mradi wa

uimarishaji wa nyumba za viongozi na nyumba za serikali, mradi wa kuimarisha juhudi za kuzuia rushwa na uhujumu uchumi, programu ya kujenga uwezo wa utekelezaji kwa taasisi za serikali, mradi wa kurasimisha rasilimali na biashara za wanyonge (MKURABITA), mradi wa kuifanyia mabadiliko na kuimarisha tume ya mipango, mradi wa uimarishaji wa takwimu Zanzibar, mradi wa utafiti wa hali ya utumishi nchini, mradi wa kuainisha masuala ya idadi ya watu, afya na uzazi, jinsia na umaskini katika mipango ya maendeleo, mpango wa ufuatiliaji na tathmini yenye kuleta matokeo ya MKUZA II na mradi wa mashirikiano baina ya sekta ya umma na sekta binafsi (*PPP*).

Mhe. Naibu Spika, baada ya kueleza mafanikio katika utekelezaji wa wizara kwa kipindi cha miaka mitano, kwa hivyo, tulipata kuipitia bajeti ya Ofisi ya Rais katika mfumo mpya wa *PBB* ambao kama tulivyoona ulikuwa na changamoto kwa kiasi fulani. Kutokana na kuwa ni mfumo mpya tofauti na ule tuliouzoea, lakini hata hivyo kamati ilipitia na kutoa mawazo yao na hatimaye kuipitisha na leo hii tunatoa maoni ya kamati kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, Bajeti ya Ofisi ya Rais, Ikulu na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2015/2016 itakuwa na jumla ya programu kuu kumi na tano (15) na programu ndogo ishirini na moja (21) kupitia katika ofisi zifuatazo:-

i. Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora;
ii. Ofisi ya Baraza la Mapinduzi;
iii. Tume ya Mipango;
iv. Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali; na
v. Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa Idara ya Faragha katika Ofisi ya Rais kamati inawapongeza, kwa kweli wamefanya kazi kubwa sana ya kuboresha Ikulu zetu lakini pia kushughulikia huduma za Mhe. Rais, ikiwemo kusimamia ahadi za Mhe. Rais.

Kwa kweli tunampongeza sana Rais kwa kutekeleza ahadi zake ndani ya kipindi cha miaka mitano, kwani moja katika ahadi yake aliahidi ni kuongeza bei ya zao la karafuu. Kwa kweli ameweza kufanya hivyo jambo ambalo kwa miaka mingi lilishindwa kutekelezeka.

Mhe. Naibu Spika, vile vile, ameweza kutekeleza ahadi yake ya kununua meli mpya ya abiria na mizigo ili kuondoa kero ya usafiri baina ya Zanzibar, Pemba na Tanzania Bara. Halikadhalika, Mhe. Rais ndani ya miaka mitano ameweza kurejesha nidhamu ya fedha serikalini, kwani ameweza kusimamia na kuziba kwa kiasi kikubwa ile mianya ya uvujaji wa fedha za umma na hivi sasa tunaweza

kujivunia kuwa ndani ya miaka mitano hii makusanyo ya fedha kila mwaka yamekuwa yakiongezeka siku hadi siku. Hii inatuonesha kuwa Rais wetu anao uwezo mkubwa wa kuiongoza Zanzibar na hata Tanzania nzima.

Mhe. Naibu Spika, pia, Rais wetu ameweza kuyashughulikia matatizo makubwa yaliyokuwepo kwenye ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Zanzibar na jitihada zake hizo pamoja na busara kubwa hivi sasa uwanja huo umeanza tena kujengwa na tunategemea ni yeye mwenyewe ndiye atakayekuja kuuzindua uwanja wetu huo.

Mhe. Naibu Spika, kama alivyoeleza waziri kwa upande wa Ofisi ya Rais, Ikulu na Utawala Bora fungu A01 ina jumla ya programu kuu tatu na programu ndogo saba, ambapo kwa mwaka wa fedha 2015/2016 imetengewa jumla ya Shilingi Bilioni Nne, Mia Tisa na Arobaini na Tatu Milioni na Laki moja (4,943,100,000). Kwa upande wa fedha za maendeleo zimetengwa jumla ya Shilingi Bilioni Moja na Milioni Mia Mbili (1,200,000,000) kwa mwaka 2015/2016.

Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi fungu A02 nayo ina jumla ya programu kuu mbili na programu ndogo nne. Kwa mwaka wa fedha wa 2015/2016 ambapo jumla ya Shilingi Bilioni Moja, Mia Tano na Thamanini na Nane Milioni na Laki Moja (1,588,100,000) zimekadiriwa kutumika kwa kazi za kawaida.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa Ofisi ya Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa Wazanzibari wanaoishi nje ya nchi, fungu A03 ina jumla ya programu kuu tatu na programu ndogo tatu kwa mwaka wa fedha 2015/2016 ambapo jumla ya Tanzania shilingi Milioni mia Sita na Sitini na tatu na laki nne. (663,400,000) zinakadiriwa kutumika katika kazi za kawaida.

Mhe. Naibu Spika, Tume ya Mipango yenye fungu A04 kwa upande wake ina jumla ya programu kuu tatu na programu ndogo tano. Kwa mwaka wa fedha 2015/2016 ambapo zimekadiriwa kutumika jumla ya Tanzania Shilingi Bilioni Kumi na Sita, Mia tatu na ishirini na nane milioni na laki tisa (16,328,900,000) ambazo Bilioni Tatu, Milioni mia sita na kumi na laki Saba (3,610,700,000). Makadirio ya kazi za kawaida na Bilioni Kumi na mbili, Mia saba na kumi na nane milioni na laki mbili (12,718,200,000) kwa makadirio ya kazi za maendeleo.

Mhe. Naibu Spika, Kwa upande wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali yenye fungu A05 ina jumla ya programu kuu mbili na programu ndogo mbili. Kwa mwaka wa fedha 2015/2016 ambapo zimekadiriwa kutumika jumla ya Tanzania Shilingi Bilioni Mbili,Milioni mia tatu na arobaini na moja na laki tano (2,341,500,000) kama makadirio ya kazi za kawaida.

Mhe. Naibu Spika, Na kwa upande wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi yenye fungu A06 nayo kwa upande wake ina jumla ya programu kuu mbili na programu ndogo tatu, ambapo kwa mwaka wa fedha 2015/2016 imekadiriwa kutumia jumla ya Tanzania Shilingi Milioni Mia nane na thalathini na saba na laki mbili (837,200,000) kwa kazi za kawaida.

Mhe. Naibu Spika, kamati yangu imeridhishwa na fedha zilizotengwa katika kitengo cha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano ambapo jumla ya Tanzania Shilingi Milioni Sabini na tatu, laki nne na hamsini na mbili elfu (73,452,000) zimekadiriwa kwa mwaka 2015/2016 ambapo zitasaidia kwa kiasi kuweza kukiendesha kitengo na kufanya kazi ipasavyo, kwani bado kitengo kinahitaji kuboreshwa ili kwenda sambamba na kupiga hatua katika masuala ya teknolojia na mawasiliano kama ilivyo katika nchi zilizoendelea huko ulimwenguni.

Mhe. Naibu Spika, Bado kamati yangu inaendelea kuisisitiza Ofisi ya Rais, Ikulu na Utawala Bora kuendeleza juhudi katika kusimamia utekelezaji wa majukumu yake, kwani hii ni Ofisi nyeti inayosimamia makaazi ya viongozi wetu ambayo yanahitaji uangalizi wa hali ya juu kiusalama na kihadhi kama makaazi ya viongozi.
Kwa mnasaba huo kamati inasisitiza kumalizwa suala la ujenzi wa Ikulu ya Micheweni ambayo imekuwa ni kilio cha muda mrefu sasa.

Mhe. Naibu Spika, Kwa upande wa Mamlaka ya Rushwa na Uhujumu Uchumi kamati yangu inaendelea kusisitiza kuangaliwa zaidi katika kupatiwa vifaa na nyenzo wanazostahiki katika utendaji wa kazi zao, ili iweze kutekeleza malengo ya uwepo wake na sio kupelekea kutoa mianya ya kuwalinda wala rushwa, kutokana na mapungufu ya utekelezaji wa kazi zao, kwani itakuwa lengo lililokusudiwa na Serikali halikufikiwa.

Mhe. Naibu Spika, ili taasisi hii iweze kufanya kazi zake vizuri, basi ni lazima kuboresha maslahi yao, kwani mazingira ya kazi zao sawa na Afisi ya *CAG* huwa wanapungukiwa na marafiki wengi, kwani huhisi kama ni tishio kwa maisha yao kutokana na kazi zao.

Mhe Naibu Spika, pamoja na kazi kubwa na nzuri inayofanywa na Mamlaka ya kuzuia na kupambana na rushwa, kama nilivyosema awali kua suala la kuangaliwa maslahi kwa watumishi wa mamlaka hii ni muhimu, Mhe Naibu Spika, kamati yangu haijaridhika kabisa na kiwango cha mshahara na stashiki nyingine kwani Mkurugenzi huyu kutokana na majukumu yake kitaifa huwezi kumfananisha na Wakurugenzi wengine, kwa hiyo kamati yangu inaitaka Serikali kushirikiana na Kamisheni ya Utumishi wa Umma kuiangalia upya *Scheme of Service* ili kuweza kumpangia maslahi Mkurugenzi huyu malipo yanayolingana na ugumu wa kazi

yake pamoja na maofisa wake. kwani yeye in mtu ambae kazi yake inamsababishia mazingira hatarishi katika kupewa rushwa tofauti na wakurugenzi wengine.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo machache, naomba Wajumbe wenzangu tuichangie,tuiboreshe na baadaye tuipitishe bajeti hii ili waende wakayatekeleze hayo yote tuliyowaagiza .

Ahsante sana, naomba kuwasilisha.

Mhe. Salma Mussa Bilal (Kny: Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika PAC): Mhe. Naibu Spika, sifa njema zisizoweza kumalizika wala kumithilika kwa mwengine yeyote, zenye ukamilifu pekee na zilizoepuka upungufu wa aina zote tunaoufahamu na tusioufahamu, zinamstahikia Muumbaji wa Dunia na Ulimwengu. Aliyetuumba sisi na viumbe wengine wote, anayehesabu matendo yetu na kujua kwa kina mwenendo wa kila kiumbe aliyemuumba, tuwajuao na wengi sana tusiowajua, mwenye hekima na mkamilifu sana wa uadilifu, na kutupa khiyari ya matendo na maamuzi yetu, lakini atakayetulipa kwa uzuri na ubaya wa tunayoendelea kuyafanya tukiwa katika maisha yetu.

Mhe. Naibu Spika, Namuomba Muumbaji wa Dunia na Ulimwengu, kunifungulia kifua changu, anipe wepesi wa matendo na mambo yangu, aupe wepesi na usahihi ulimi wangu, ili Waheshimiwa Wajumbe na wananchi wote kwa ujumla waweze kufahamu hotuba yangu.

Mhe. Naibu Spika, Kamati iliyonipa fursa ya kusimama leo hii ni Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika, ambayo nikiitamka hivi pekee, wananchi wengi hawataifahamu mpaka nitakapoiita kwa ufupi na umaarufu wake, ambayo ni *P.A.C.* Kamati hii kwa takriban mwaka wa tatu sasa, inapitia makadirio ya mapato na matumizi ya mwaka ya Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kazi ambayo imeelekezwa na kifungu cha 34(2) cha Sheria ya Fedha ya Zanzibar, namba 5 ya mwaka 2005.

Mhe. Naibu Spika, Utafiti uliofanywa na Kitengo cha Utafiti cha Afisi ya Baraza la Wawakilishi, uliotokana na Mjumbe wa Kamati hii, Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando), umethibitisha kuwa, Kamati zote za *P.A.C* Barani Afrika, zinafanya kazi ya awali ya kufuatilia taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, pamoja na ukweli kuwa, baadhi ya Kamati hizo zimepewa uwezo mkubwa zaidi wa ufuatiliaji wa matumizi ya fedha za Serikali kwa namna Kamati zinavyoona inafaa, bado inabakia kuwa, nyenzo ya awali ya Kamati hizi ni ripoti za ukaguzi zinazoandaliwa na Afisi hii ya Mkaguzi Mkuu.

Mhe. Naibu Spika, Uhusiano uliopo baina ya Kamati za *P.A.C* na Afisi za *CAG* ni wa karibu mno, kiasi ya ambacho, kama ripoti za ukaguzi hazitafahamika vyema kwa Kamati, basi hazitakuwa na majibu fanisi kwa wananchi.

Aidha, Bajeti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ndio msingi mkuu wa ubora na uzuri wa ripoti za ukaguzi na utekelezaji mzima wa majukumu ya Afisi hii. Bajeti hii inapozingatia upeo wa kina wa kuitosheleza Afisi hii katika utekelezaji mzima wa majukumu yake, ni kuisaidia sana Kamati kutekeleza majukumu yake na hatimaye kuinua kiwango kikubwa cha mapato ya Serikali na kudhibiti matumizi mabaya ya fedha za wananchi, ambazo mdhamini wa fedha hizo ni Serikali.

Mhe. Naibu Spika, Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu imekadiriwa kukusanya Tsh. 28,213,000 kwa mwaka 2015/2016, makadirio yanayotarajiwa kupatikana kutokana na ada ya ukaguzi wa hesabu. Kamati imeelezwa kuwa, mwaka jana Afisi ilikadiriwa kukusanya Tsh. 18,000,000 na chanzo kikiwa ni hicho hicho cha ada ya ukaguzi, lakini mwaka huu kuna nyongeza ya Tsh. 10,213,000 hali inayoilazimisha Afisi hii kuongeza gharama za ada ya ukaguzi ili iweze kupata fedha zilizokadiriwa.

Mhe. Naibu Spika, mahojiano ya awali ya Kamati kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu kuhusiana na makisio haya mapya ni iwapo Afisi hii ilijikadiria yenyewe katika kufanya makisio hayo, na Kamati imethibitishiwa kuwa kiwango hiki cha mwaka huu kimekadiriwa na Wizara ya Fedha na hata Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu amekiona kikubwa, isipokuwa hana uwezo wa kukataa kwani ni maelekezo ya Wizara ya Fedha. Na kwa upande wa Wizara ulieleza kuwa, wao hufanya makisio kwa kuzingatia maendeleo ya makusanyo kwa mwaka uliopita. Aidha, sababu ya Serikali kwa mwaka huu wa fedha kutotegemea fedha za *GBS*, kunazifanya taasisi zake ikiwa ni pamoja na Afisi hii kuongeza mapato kwa lengo la kukidhi hali hiyo.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na ukweli wa Afisi ya Mdhibiti kutakiwa kuongeza makusanyo hayo kwa kulazimika kuongeza ada ya ukaguzi, kwa mnasaba wa makisio ya mwaka jana ambayo ni Tsh. 18,000,000 taarifa zilizoelezwa kwa Kamati ni kuwa, hadi kufikia Machi 2015, fedha halisi ambazo zilikuwa zimeshakusanywa zilikuwa Tsh. 9,000,000 sawa na asilimia 50 (50%) ya makadirio, hali ambayo kwa kawaida inaleta ugumu wa kujiridhisha kwamba, Afisi ina uwezo kamili wa kukusanya makadirio yote wanayopangiwa kwa asilimia 100(100%), hata kama ilielezwa kuwa, kwa kipindi cha miezi iliyobakia hadi kufikia tarehe 30 Juni 2015, ndio Afisi inataraji kupata asilimia 50 iliyobakia.

Mhe. Naibu Spika, Matumizi ya Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu kwa mwaka 2015/2016 yanakadiriwa kuwa Tsh. 2,341,600,000 fedha ambazo

zitatumika kwa kazi za kawaida, ambapo Tsh. 822,819,000 zitatumika kwa mishahara, maposho nayo yatatumia Tsh. 426,205,000 na matumizi ya uendeshaji wa Ofisi yatakuwa Tsh. 1,092,476,000. Fedha zilizokadiriwa kwa matumizi ya kawaida kwa mwaka uliopita zilikuwa Tsh. 2,023,000,000 na hivyo, kwa mwaka huu wa fedha kuna nyongeza ya Tsh. 318,600,000 hali inayoipa matumaini Kamati kuwa, Afisi hii itakuwa na uwezo mkubwa zaidi ukilinganishwa na wa mwaka jana wa kutekeleza majukumu yake.

Mhe. Naibu Spika, Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu kupitia fungu lake la A05, imepangiwa programu kuu mbili za kuzitekeleza kwa mwaka wa fedha wa 2015/2016. Programu kuu ya kwanza ni Udhibiti wa Fedha na Rasilimali za Umma ambayo programu yake ndogo ni hiyo hiyo na programu kuu ya pili ni Utawala na Uendeshaji wa Udhibiti na Ukaguzi, yenye programu ndogo mbili ambazo ni Usimamizi na Uendeshaji wa Udhibiti na Ukaguzi na Udhibiti na Ukaguzi Pemba.

Mhe. Naibu Spika, Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika ya Baraza la Wawakilishi (*P.A.C*), imeridhika kutumiwa kwa Tsh. 1,101,888,000 kwa programu kuu na ndogo ya Udhibiti wa fedha na Rasilimali za Umma, imeridhika pia kutumiwa Tsh. 727,297,000 kwa programu ndogo ya Usimamizi na uendeshaji wa Udhibiti na Ukaguzi ambapo huduma inayotarajiwa kutolewa ni za utumishi na uendeshaji vile vile jumla ya Tsh. 512,415,000 zimeridhiwa pia na Kamati kutumiwa na Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa ajili ya programu ndogo ya Udhibiti na Ukaguzi Pemba, kwa ajili ya huduma za utumishi na uendeshaji, Pemba.

Mhe. Naibu Spika, Kamati ilipopitia Idadi ya Watendakazi wa Afisi hii, ilijiridhisha kwamba, kuna wafanyakazi 154 kwa upande wa Unguja na Pemba kwa mwaka 2014/2015. Kwa ajili ya Programu ndogo ya Udhibiti wa Fedha na Rasilimali za Umma itasimamiwa na wafanyakazi 82, idadi ambayo itaendelea hivyo hadi mwaka 2017/2018; programu ndogo ya Usimamizi na Uendeshaji wa Udhibiti na Ukaguzi itasimamiwa na wafanyakazi 33 na wataendelea wafanyakazi hao hao hadi mwaka 2017/2018 na kwa programu ndogo ya Udhibiti na Ukaguzi, Pemba itasimamiwa na wafanyakazi 39 ambao kwa idadi hiyo hiyo hadi mwaka 2017/2018.

Mhe. Naibu Spika, ninayo imani kwamba, Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili wanakumbuka miongoni mwa changamoto inayoikabili Afisi hii ni pamoja na kukosa wataalamu wa kutosha katika ukaguzi wa miradi mbali mbali hasa ya Uhandisi na Ujenzi wa barabara.

Kamati yetu kwa nguvu zote, katika kila ripoti iliyokuwa inaiwasilisha hapa, ilitilia mkazo sana Afisi hii kupatiwa maslahi ya watendaji wake pamoja na kuongezewa wigo wa kupata wataalamu hao kwa uajiri mpya. Hivyo, kama taarifa hizi za idadi ya wafanyakazi itabaki kuwa hivi, suala hili litaendelea kuipa wasi wasi Kamati iwapo Afisi itaweza kweli kufikia kiwango cha asilimia 100 cha wataalamu kwa kipindi hiki cha miaka mitatu kutoka sasa.

Mhe. Naibu Spika, Kamati ilipouliza suala hili wakati wa kujadili bajeti hii, ilielezwa kuwa taarifa hizo ni makadirio tu *(projection)*, lakini pia kuwa sawa kwa kila idadi ya watumishi hadi mwaka 2017/2018 kunategemea sana kuwa, mwaka huu wataajiri na hivyo nafasi hizo zitaendelea kuwepo, kwani zitakuwa wazi kwa sababu mbali mbali ikiwa ni pamoja na kustaafu. Taarifa hii pamoja na usahihi wake, ni vyema ikatizamwa tena kwa maslahi ya Afisi kupatiwa fursa ya kuajiri watendaji wapya kwa namna ukaguzi unavyobadilika duniani.

Mhe. Naibu Spika, Kamati yetu inashuhudia kwa takriban miaka mitatu sasa ya fedha, Afisi hii haina Mradi wowote wa Maendeleo. Mwaka wa mwisho kwa Afisi hii kuwa na Mradi wa Maendeleo ulikuwa 2011/2012, Mradi wa Kuimarisha Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu *(Strengthening of the CAG Office)*, na fedha zilizokadiriwa kwa mwaka huo zilikuwa Tsh. 196,350,000 ambazo zote zilifadhiliwa na Benki ya *ADB*, kupitia Mikopo ya Nje, huku Serikalini kukiwa hakuna fedha yoyote iliyokadiriwa katika mradi huo.

Mhe. Naibu Spika, Wale Wajumbe wa awamu zote za Kamati ya *P.A.C* mbali na awamu hii tunayomalizia kazi mwaka huu, watakumbuka namna Mdhibiti alivyokuwa anaisaidia Kamati kupitia miradi mbali mbali ya kujenga Afisi yake huku akielewa fika kwamba, uwezo wa Afisi yake tu haungelitosha bila ya kuijengea uwezo Kamati. Wajumbe wa Kamati ya *P.A.C* walipata msaada mkubwa wa kujengewa uelewa mkubwa wa kazi zao, kupitia mafunzo ambayo yalifanyika ndani na nje ya nchi.

Mhe. Naibu Spika, Kwa mfano, Wajumbe wa Kamati yetu walipata nafasi ya kusafiri kwenda Maleysia, Singapore, Zimbabwe, Zambia, Afrika Kusini, Dar es Salaam, Arusha na kwengineko kwa msaada wa moja kwa moja wa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu na katika mikutano mbali mbali ya *SADCOPAC*, Mdhibiti aliweza kusaidia kuongeza idadi ya Wajumbe walioshiriki katika mikutano hiyo, baada ya Afisi ya Baraza kutokuwa na uwezo wa kuwapeleka Wajumbe wote.

Mhe. Naibu Spika, Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika, inaendelea kusikitika kwa Afisi hii kutopata Mradi wa Maendeleo kwa

kipindi kirefu, huku hali hii ikidhoofisha maendeleo na ubora wa utendaji kazi wa Afisi ya Mdhibiti na Kamati ya *P.A.C* kwa ujumla.

Mhe. Naibu Spika, katika ufunguzi wako wa Ripoti ya Tathmini ya Uwezo wa Kibunge na Mahitaji ya Mafunzo kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi *(Report on Capacity Assesment on Legislative Skills and Training Needs for Members of the House)* ya mwaka 2012, ukurasa wa 6 ulieleza kuwa:

"It is often said that there is no school for parliamentarians, much less for politicians. When aspiring politicians are elected into office – as legislators – often they have to learn –on – the –job-. While they bring with them various life experiences, academic and other professional qualifications, none of these prepare them sufficiently for the multilayered and multi-faceted office of parliamentarian."

Mhe. Naibu Spika, katika ufunguzi huo kama nilivyousoma hapo juu, ulikusudia maana ifuatayo:

"Mara nyingi husemwa kuwa hakuna Skuli Maalum ya Wabunge kujifunza, kama ilivyo zaidi kwa Wanasiasa. Mara Wanasiasa wanapochaguliwa kuwa Wabunge, wanalazimika kujifunza namna ya kufanya kazi zao katika utekelezaji wa kazi zao. Wakati huo huo huja na uzoefu mbali mbali wa maisha, wa elimu na sifa nyengine za Kitaaluma, lakini hakuna hata moja kati ya hizo zinazowaandaa vya kutosha kwa majukumu tofauti ya Ofisi za Kibunge."

Mhe. Naibu Spika, maneno yako yanaendelea kusadikiwa na kila mtu, na hata katika Kamati yetu ya *P.A.C* hupata tabu sana ya kujua kutekeleza majukumu yetu, kwani hakuna hata mmoja kati yetu aliyejifunza kuwa Mjumbe wa Kamati hii. Mapungufu haya yalikuwa yanasaidiwa sana kuondoshwa kwa Msaada wa elimu iliyokuwa inatolewa na Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu, lakini ameshindwa kwa miaka hii kutekeleza hili kutokana na kukosa Miradi ya Maendeleo.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na ukweli wa bajeti ya mwaka huu kutozingatia sana wafadhili, lakini hoja na ukweli huu hauwezi kuwa kisingizio kwa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali iliyokosa mradi wowote wa maendeleo kwa miaka zaidi ya mitatu sasa. Hivyo, ni vyema Waziri akatusaidia majibu kwani athari zake ni kubwa kwa Afisi ya *CAG* na Kamati ya *P.A.C.*

Mhe. Naibu Spika, katika Taarifa ya Haki za Binadamu Tanzania ya mwaka 2013, taarifa ambayo pia imehusisha Taarifa ya Haki za Binadamu Zanzibar, iliyoandaliwa na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu cha Tanzania kwa

mashirikiano na Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar, katika ukurasa wa 488 inaeleza kuhusu Rushwa kama ifuatavyo:

"Rushwa bado ni changamoto na inaendelea kukua siku hadi siku. Inasemekana kuwa Taasisi za Serikali zinahusika moja kwa moja na vitendo vya rushwa ambavyo huathiri Utawala Bora. Taarifa ya vitendo hivi vibaya imeifikia Serikali Kuu ambayo imeanza kuchukua hatua za kupambana na tatizo hili."

Mhe. Naibu Spika, katika chombo kikuu cha Serikali ukiacha Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar, Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu ni Taasisi nyengine muhimu Zanzibar na duniani kote katika mapambano ya rushwa na vitendo viovu. Mapambano hayo hayatawezekana hata kidogo, iwapo Afisi ya Mdhibiti kwa umuhimu wake, haitowezeshwa na kuwa na uwezo wa kifedha na kitaaluma juu ya kufichua uovu huo, lakini pia iwapo Kamati ya P.A.C, Kamati ambayo ni muhimu sana katika mapambano ya rushwa na vitendo viovu, haitopata mafunzo na kujengewa uwezo wa kufanya kazi zake za kupambana na rushwa na kufichua uovu.

Mhe. Naibu Spika, Benki ya Dunia kupitia wataalamu wake Ndg. Rick Stapenhurst na wengine wamezungumzia sana nafasi na jukumu la Bunge pamoja na Ofisi za Mkaguzi Mkuu katika kupambana na Rushwa. Katika Kitabu kiitwacho **"Jukumu la Bunge katika kupambana na Rushwa"***, (The Role of Parliament in curbing corruption),* ukurasa wa 101 kinasemwa:

"Building strong accountability institutions is a key challenge of development and is critical to controlling corruption. Among state institutions, the supreme audit institutions (SAIs) play a central role because they help promote government accountability and transparency through sound public financial management"

Mhe. Naibu Spika, nukuu hii ina maana ifuatayo "Kujenga taasisi madhubuti za uwajibikaji ni changamoto ya msingi ya maendeleo na katika mapambano dhidi ya rushwa. Miongoni mwa taasisi za dola, Afisi za Ukaguzi wa Hesabu za Serikali hutekeleza jukumu la msingi kwa sababu husaidia kuongeza uwazi na uwajibikaji wa Serikali kupitia udhibiti wa fedha za umma."

Mhe. Naibu Spika, hoja ya Kamati ni ile ile niliyoieleza awali na ambayo tulikwisha ieleza katika ripoti zetu za miaka iliyopita, ni kuhusiana na Miradi ya maendeleo ya kuijengea uwezo Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu pamoja na Kamati ya *P.A.C.* Na kinyume chake, tunaendelea kueleza kuwa, pamoja na hoja muhimu zinazotolewa na Serikali juu ya kuikosesha miradi Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, huku ikijua athari zake za kudhoofisha

uwezo wa *CAG* na *P.A.C*, lakini ifahamike na ikumbukwe kuwa kuna khofu kwa wananchi, vyombo huru vya uwajibikaji pamoja na taasisis za kupigania utawala bora na kupambana na rushwa kwamba, Serikali hufurahishwa kukosekana kwa uwezo wa Afisi ya *CAG* ikiwa ni pamoja na kuipatia miradi ya maendeleo, kwani iwapo Afisi ya *CAG* ikiwezeshwa vizuri nayo itaiwezesha Kamati ya *P.A.C* ambayo kwa mashirikiano ya pamoja baina ya *CAG* na *P.A.C*, kutaiweka Serikali katika wakati mgumu wa uwajibikaji na uwazi wa matumizi ya fedha za wananchi wake.

Mhe. Naibu Spika, katika kitabu nilichokinukuu hapo punde cha *World Bank Institute*, ukurasa wa 104, kinaeleza hali halisi inayozikumba Kamati zetu za *P.A.C* kama ifuatavyo:

"In many countries, the public accounts themselves are poorly maintained, parliament may be weak, and finance ministry may not ensure that audit queries or observations are addressed. Flagrant abuses identified by the SAIs are often not prosecuted, and in some cases, SAIs' work may be subrogated"

Yaani, "Katika nchi nyingi, Kamati za *P.A.C* zenyewe hazishughulikiwi ipasavyo, Bunge linaweza kuwa dhaifu, na Wizara ya Fedha haiwezi kuhakikisha hoja za Mdhibiti au mapendekezo yake yanawekwa wazi. Ubadhirifu wa wazi wazi unaoibuliwa na Mkaguzi Mkuu mara nyingi huwa hakuna mashtaka yoyote yanayofunguliwa kwa washtakiwa, na katika hali nyengine, kazi za Mkaguzi Mkuu huweza kuchakachuliwa"

Mhe. Naibu Spika, nukuu yangu ya hapo juu inaendelea kusisitiza tu kwamba, Afisi ya Mdhibiti inahitaji sana kujengewa uwezo na kuwezeshwa kwa fedha za Serikali pamoja na fedha za miradi ya maendeleo na kitendo cha kuikosesha fedha za Maendeleo, kuna athari kubwa na kama tutaendelea hivi, tutaendelea kudhoofisha uwezo wa *CAG* sambamba na uwezo wa Kamati ya *P.A.C*.

Mhe. Naibu Spika, naomba sasa kumalizia hotuba yangu hii fupi kwa kukushukuru wewe, Katibu wa Baraza la Wawakilishi sambamba na watendaji wote wa Afisi ya Baraza la Wawakilishi kwa msaada mnayoipatia Kamati yetu ikiwa ni pamoja na kuipa muda wa kufanya kazi zake, ingawaje bado tunaendelea kukuomba pamoja na Katibu wa Baraza, kuipa muda mwingi zaidi Kamati yetu, ili iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Mhe. Naibu Spika, tunamshukuru sana Mhe. Waziri wa Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na watendaji wake pamoja na Katibu Mkuu wa Ofisi ya Rais, Ikulu na Utawala Bora, kwa juhudi zao na mashirikiano yao waliyoyaonesha kwa Kamati wakati wa kupitia

bajeti hii, na kuwa wawazi na wakweli katika kujibu masuala mbali mbali yaliyoulizwa na Kamati.

Mhe. Naibu Spika, napenda tena kuchukua fursa hii kuwapongeza na kuwashukuru Wajumbe wa Kamati yetu kwa mashirikiano ya pamoja na kufanya kazi za Kamati kwa uadilifu mkubwa, hali iliyopelekea hadhi ya Kamati kuimarika. Napenda kuwaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati kuendelea kuitumia elimu na uzoefu walioupata katika Kamati yetu katika harakati mbali mbali za kujenga Taifa hili kwa maslahi ya wananchi.

Mhe. Naibu Spika, niwashukuru sana Makatibu wa Kamati yetu na tunaendelea kuliomba Baraza hili kujenga uwezo na uimara wa Makatibu mbali mbali wanaopangiwa kufanya kazi na Kamati za Kudumu za Baraza. Kuwajengea uwezo Makatibu Kamati ni jambo la msingi sana hasa ikizingatiwa kuwa, wao ndio waajiriwa wa Kudumu na wanaobakia katika kuzisaidia Kamati kila siku, wakati Wajumbe wa Kamati ni wanasiasa wanaochaguliwa na wananchi kwa muda wa miaka mitano, hivyo ni vyema tukawaimarisha Makatibu hawa ili waweze kuzisaidia ipasavyo Kamati zetu za Baraza.

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba sasa kuwatambua Wajumbe wa Kamati na Makatibu Kamati wa Kamati ya *P.A.C* waliofanya kazi hii kama ifuatavyo:

1. Mhe. Omar Ali Shehe - Mwenyekiti
2. Mhe. Fatma Mbarouk Said - Makamo Mwenyekiti
3. Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando) - Mjumbe
4. Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi - Mjumbe
5. Mhe. Rufai Said Rufai - Mjumbe
6. Mhe. Salim Abdalla Hamad - Mjumbe
7. Mhe. Salma Mussa Bilal - Mjumbe
8. Mhe. Shamsi Vuai Nahodha - Mjumbe

Aidha, Makatibu Kamati ni hawa wafuatao:-

1. Ndg. Nasra Awadh Salmin - Katibu
2. Ndg. Othman Ali Haji - Katibu

Mhe. Naibu Spika, naomba kuwashukuru kwa upekee Wajumbe wa Baraza lako Tukufu, kwa usikivu wao na umakini wa kunisikiliza, nikitaraji kuwa, wataweza kabisa kuchangia bajeti ya Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu.

Aidha, niendelee kuwakumbusha kuwa, sisi Wajumbe ndio wenye dhamana ya kupitisha bajeti ya Serikali, ikiwa ni pamoja na Bajeti ya Afisi ya Mdhibiti na

Mkaguzi Mkuu, na sisi ndio wenye dhamana ya kuisimamia Serikali katika utekelezaji mzima wa bajeti ambayo tunaiidhinisha katika Baraza hili.

Mhe. Naibu Spika, hali hii inaendelea kunikumbusha dhamana yetu ya kuinua maendeleo ya kiuchumi ya wananchi wetu. Kwetu sisi wajibu wetu mkubwa ni kuhakikisha fedha ambazo Serikali imeazimia kuzikusanya, izikusanye kwa uadilifu, lakini matumizi ya fedha hizo yawe kwa mujibu wa Sheria za Fedha, Sheria za Manunuzi na Sheria nyengine zinazohusika.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Naibu Spika, kwanza nitoe shukurani za dhati kabisa kukushukuru wewe kuweza kunipa fursa hii. Lakini la pili na mimi nitoe mkono wa pole kwa Mhe. Rais kwa kufiwa na dada yake, Mwenyezi Mungu atampeleka salama safari yake na atampunguzia adhabu ya kaburi.

Mhe. Naibu Spika, mimi leo kwa kuwa ni Mjumbe mambo mengi sana humu yatakuwa ya ufanisi tu na ya kitaalamu hasa kwa mujibu wa sheria. Mambo mengine nitakuwa ninaelekeza kwa mujibu wa Kanuni zinavyonielekeza kama ni Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Naibu Spika, niseme kuwa nimpongeze Mhe. Waziri Dkt. Mwinyi mwenyewe na nimsifu sana sana kwa kazi zake nzuri, kwa usikivu wake na umahiri wake, ndio maana akafika kuitwa Dokta.

Mheshimiwa nimpongeze sana na nimshukuru sana Katibu wake na hapa ndio pa kuagana. Maana yake hawa nimecheza nao sana, Katibu ni mtu mmoja ambaye ni msikivu na ni mnyonge sana na anakubali kuonywa. Ukimuona mkimya na ukimuonya anakuwa kimya hawi mtu wa kukurupuka na akaonesha ukali kutokana na Ukatibu wake, hilo moja.

Mhe. Naibu Spika, katika Makatibu ambao nawasifu sana na yeye yumo. ni nambari *one*. Halkadhalika Naibu wake na yeye tulikwenda naye safari katuelekeza katika msafara huo, katuonesha ujasiri katika utendaji wake wa kazi na yeye nimpongeze sana sana. Na Wakurugenzi na wao *Alhamdulillah* ukiwapigia simu wanakuitikia, maana kuna Wakurugenzi wengine hawapokei simu lakini wao wanapokea simu.

Niwapongeze sana Wakurugenzi kuwa wapo *active* katika kupokea simu na hiyo ni moja katika Utawala Bora. Niwashukuru sana kwa hilo na niwapongeze sana kwa hilo. Wakurugenzi wengine wanajiona wameshafika hata simu za Wawakilishi hawazipokei. Lakini hawa hawajali hilo wanaona Mheshimiwa lazima atakuwa ana

jambo la kutaka kunielimisha mimi, wanapokea simu ikiwa imepigwa tena awe mwenyewe Waziri, akiwa Katibu, akiwa Naibu Katibu wote wanapokea simu. Niwapongeze kwa hilo na Mwenyezi Mungu awazidishie fani ya juu zaidi ili wazidi kuendelea katika Idara hii na kuweza kutufikisha pazuri.

Mhe. Naibu Spika, nimeona nitoe pongezi hizo kwa sababu sasa hivi Wawakilishi tupo *ICU*. Sasa hivi hatujijui, hiyo lazima tuseme Waheshimiwa, tunaweza tukarudi na tunaweza tusirudi. Sasa lazima nianze kuwapa shukurani sana kama nimewakwaza, nimewakosa, naomba radhi sana kwa hilo ili na mimi waniombee dua, wanipigie *fat-ha* ili niweze kurudi tena.

Mhe. Naibu Spika, sasa naanza kuchangia, ukurasa wa 26 katika hii Ofisi ya Usalama wa Serikali (*GSO*). Mheshimiwa tumetembea miji mingi, tumeona kitu kama hichi *GSO* ni kitu ambacho muhimu sana hata katika serikali. Kitu hichi niseme kama kuna mjiti mmoja ndani yake unakuwa una moyo, kwa hivyo na hichi niseme kwamba ni moyo wa Serikali.

Mhe. Naibu Spika, lakini nina sikitiko moja. Sikitiko langu Mheshimiwa bado hatujawawezesha vizuri sana hasa katika utendaji wa kisasa. Kwa sababu sasa hivi watu wanakwenda na sayansi na teknolojia, hichi ndicho kitu cha msingi katika dunia linatembea jambo kama hili.

Mheshimiwa bado hatujawafadhili vizuri, hilo tuseme ukweli. Kwa sababu kitengo hichi kwa kweli sidhani kama Mhe. Waziri utanambia wangapi umewapeleka nchi za nje, Marekani au sehemu nyengine yoyote, sijui utanambia wangapi maafisa wako au watendaji wako. Sijui kama utakuwa na namba hiyo ya kunambia. Kama unao ambao umewafikisha huko mimi nitakupongeza sana, hata kama huna nitakupongeza kwa sababu jitihada nyingi unazo.

Mhe. Naibu Spika, niseme ukweli ulivyo, kwa sababu hawa ni watu muhimu sana, ni watu ambao kazi zao ni nzito. Sasa watu kama hao wanapokuwa na kazi nzito basi ni lazima na wao tuwajengee vizuri. Kwanza Ofisi zao zinatakiwa ziende na wakati.

Mhe. Naibu Spika, kuna ofisi nyengine zinakutisha hata kuingia, lakini wao Ofisi yao ni *simple* tu. Pia wanatakiwa wawe kando ya mji lakini utashangaa *any time* tunawaona wapo chini ya ubavu.

Mhe. Naibu Spika, mimi niseme hili moja kama kutakuwa na uwezo tuweze kuwaingizia fedha ambazo zenye msingi. Halafu hapa nimeona matumizi yao haya fedha yao Mheshimiwa bado haijakidhi haja kweli, ninaomba sana Mheshimiwa turekebishe fedha zao, mishahara tena ndio usiseme hapo, hapo utajijibu

mwenyewe Mheshimiwa kwa sababu mshahara mtu yeyote hakuna anayetaka ajipunguzie. Lazima kuna watu mishahara wanatakiwa waweze kuongezewa ili kuweza kuwafikisha pahala pazuri.

Mhe. Naibu Spika, hii wizara kubwa, wizara hii ndio ya Rais, Rais ndiye Mtendaji Mkuu wa nchi, kwa hivyo lazima iende na mambo yake mazuri, watendaji wawe wazuri, watendaji wawe *faster* katika utekelezaji.

Niwashukuru sana Mheshimiwa mumejitahidi sana kiasi kikubwa sana kuin'garisha Ikulu. Mhe. Dkt. hongera sana, Ikulu ya jana si ya leo. Mimi nimekwenda Ikulu mara mbili nilikuwa natamani nisitoke, na sababu kubwa natamani nisitoke kutokana na ile asili hasa, kwa sababu ni kitu asili ndio ilikuwa Ikulu inanivutia Mheshimiwa.

Kuna mambo mimi siyaoni huko nje, asilia, lakini Ikulu asili ipo, kwa kweli imeniburudisha sana, hakuna isipokuwa Ikulu, lazima niyapongeze kwa sababu anavithamini vile vitu 24 *hours* viti vinang'ara, hivyo ndivyo inavyotakiwa Ikulu sio Ikulu iwe ovyo ovyo tu.

Mimi nimekaa Ikulu nimekaa na Rais naongea naye sijamuona hata nzi kupita, mama yangu nakwambia! Sijamuona Mhe. Naibu, na ndio sifa ya Ikulu, mara mbu, mara kakupitia mende lakini nimekaa muda mwingi na Mhe. Abdalla alikuwepo hakuna nzi mimi nimeshangaa sana. Nikaambiwa Mheshimiwa utapata uwakilishi umpate nzi Ikulu nasema nishasamehe uwakilishi, kwa sababu nzi simpati Ikulu. Nende kwa mganga anambie Mheshimiwa uwakilishi wako ukitaka kuupata kachukue nzi Ikulu ndio upate uwakilishi, aa nasema hapa nishakosa mimi kwa sababu siwezi kumpata. Na ile inavyotakiwa uzuri wa Ikulu lazima ioneshe umahiri wa Ikulu.

Mhe. Naibu Spika, nilipokuwa pale Washington DC Marekani nimekaa nje tu nimeona ile *White House* jinsi ambavyo ilivyokuwa, je ndani ningeingia ningepata kwenda kwa Obama lakini sikuwa na *appointment* ya kumuona, ilivyokuwa inan'gara, nje tu inan'gara na ndio maana ikaitwa Ikulu neno la Ikulu nyinyi msilifahamu dogo, neno la Ikulu neno kubwa.

Anaishi Rais wa Zanzibar anaendesha wananchi wa Zanzibar si kitu cha mchezo, na ndio maana mimi nikawa napiga kelele siku zote hata magari yaendane na Ikulu. Lakini hapa naomba sana Mhe. Naibu Spika, moja ninaliomba la masikitiko nakutuma hasa, kwa sababu *traffic* wetu Mheshimiwa hawajaendana na Ikulu kwa sababu hata ile inaitwa *radio call* sijui kama wanazo.

Naomba sana Mheshimiwa hili suala tusilifumbie macho. *Radio call* ni kitu muhimu sana ndio zinazoendesha misafara, lakini ikiwani kidogo naomba ziongezwe kwa sababu *radio calls* ni moja ambazo za kuzifikisha *messages* za *exchange* za wakubwa wetu *otherwise* sasa hivi Zanzibar, Zanzibar sasa hivi *half* London magari mengi, na ninashukuru sana sasa hivi tuna *stop lights*.

Zanzibar nani anajua kwamba kuna *stop lights*, unaona si maendeleo ya Rais hayo, ni maendeleo mazuri sana Mhe. Spika, hivi tukitaka tusitake lazima tuseme kuwa Zanzibar ina-*change* siku hadi siku, hilo tulikubali kwa sababu leo tuna *stop lights*, leo tuna taa tunatumia *solar* ndio maendeleo hayo. Sasa leo ikiwa *traffic* wetu hawana *radio calls*, kwa kweli naomba Mhe. Waziri utapokuja unambie tayari si chini *ya radio calls* 100 wamepata askari wetu wa *traffic*, naliombea sana ni muhimu.

Mhe. Naibu Spika, tunapokwenda askari wa wenzetu wanakuwa na *full* nondo; ana pingu ziko hapa, ana *pistol* iko hapa, ana kirungu kipo hapa, na hiyo *radio call* iko hapa, *wallahi* wanakwenda vizuri wanaringa, tutembee nje huko tuone, ukija Wamarekani ndio wenyewe ndio hao vitu vyote kaviweka hapa kwenye kiuno uone anavyokwenda na nini.

Lakini leo askari wetu wanakuwa hawana *radio calls* kwa kuwa hatuwezi kuwamiliki wote Polisi wawe na silaha hiyo haiwezekani kwa sababu tuna *special* mambo barabarani lakini *radio call* Mhe. Naibu Spika, ni wajibu wao lazima wawe nazo.

Nimeomba hilo Mheshimiwa lisimamie, lihakikishe hili suala kwa sababu si kitu cha mchezo wanatumia simu, simu mitandao utaambiwa sasa hivi simu hii imefungwa na kumbe iwazi lakini unaambiwa simu hii haipatikani, utawahi saa ngapi kum-*exchange* mtu na gari nyingi sasa hivi, tusiwasababishe ajali ambazo zinawezekana zikaepukika. Hilo nimeona nilizungumze sana kwa sababu liweze kutusaidia katika malengo ya kuwaenzi viongozi wetu; marais hawa watatu wa Zanzibar ili kuweza na wao Mwenyezi Mungu awape safari zenye salama na kheri na wao. Kwa sababu *radio calls* ni vitu ambavyo vinawezekana Mheshimiwa vikapatikana bila ya matatizo yoyote.

Mhe. Naibu Spika, nishukuru sana katika jitihada za wizara hii katika ujengaji wao wa Ikulu, lakini nisikitike sana bajeti yao inakuwa ndogo sana, Mhe. Waziri anajitahidi sana na mtaalamu wako yule injinia kaka yangu yule, jina lake nimelisahau lakini niseme ni injinia tu ambaye anayehusiana na yeye nimpongeze sana anajitahidi katika usimamizi, hana tabia kasoro kasoro kudokoa dokoa kwa sababu yeye anaona sifa nzuri kulikamilisha lile jambo na hivyo ndio inavyotakiwa.

Kwa sababu tulipokwenda kutembea tumeona majengo mazuri, tulimsifu sana na nitaendelea kumsifu sana tena asiliharibu tembo tena aendelee kuliweka vizuri tu, kwa sababu kila sifa zikiwa nzuri na wewe ujikuze katika utendaji wako wa kazi vizuri sana. Na hizo Ikulu zilizobakia ninamuomba sana Mheshimiwa wangu injinia zisimamie zimalize, kama ulivyotumia bajeti yako finyu, hivyo hivyo jifinye lakini ufikishe viongozi wetu wanapata nyumba zilizokuwa zinastahiki na jina lao.

Mhe. Naibu Spika, tukiendelea kwa Pemba kule nimesema kuwa haya mambo ya gari, gari hizi ninaomba sana kuwe na utaratibu wa kuweza kupelekwa *special* sio tena gari ya mtu binafsi ya raia inakodiwa fedha kutumia viongozi wetu.

Mhe. Naibu Spika, *security-wise* ni kitu muhimu sana. Naomba sana, ndio maana nikasema hiki kitengo kingekuwa kinakaa vizuri mkanielimisha vizuri mnawapa watu *training* nzuri basi wasingekubaliana na gari hizi za kuweza kwenda kukodiwa raia, Aisee ni kitu kigumu sana, Mheshimiwa ni kitu hatari, tusikubali sana tujihini lakini kule Pemba lazima tuwe na gari zetu hasa.

Ninashukuru sana Mheshimiwa kwa taarifa fupi fupi hapa nimeambiwa na Mhe. Waziri leo amenipa vitu vikubwa sana Mhe. Waziri wangu Mhe. Mohammed Aboud, jamadari wangu ananambia kuwa gari Mheshimiwa tayari zishakuja, mabenzi yapo sasa hivi lakini japo *left*, nikawaambia hakuna kidogo kisichoharibika lakini ndio hicho hicho *left* tunaweza kuendesha hapa Mheshimiwa.

Hilo moja ni pongezi kubwa sana, na hivyo visakina tumeambiwa zimekuja nazo lakini ziko *left* hakuna jambo lililokuwa baya na tunataka kitu kizuri. Sasa nazo hizo niseme niipongeze sana Ofisi ya Makamu wa Pili kusimamia Waziri wake kuweza kupatikana vitu hivyo. Nishukuru sana kwa jambo hilo, ninamshukuru balozi wa Oman kwa kuliona hilo na aendelee kutusaidia, hata hivyo si vibaya kasema na zile *radio calls* atatusaidia nalo sio mbaya kwa sababu ndio tunajenga udugu ambao udugu huo ni wa kudumu zaidi.

Mhe. Naibu Spika, niende hapa katika ukurasa 114 nimeona hapa inasema katika kuimarisha majengo ndio hayo niliyokwambieni, nimeona katika nyumba za walinzi Dodoma, nyumba za wafanyakazi Laibon hapo Dar es Salaam na ujenzi mwengine. Mhe. Naibu Spika, Laibon nimekwenda mwenyewe haki ya Mungu umetengeneza vizuri sana. Ndio maana nikasema kuwa wasisite katika utekelezaji wao ili tuone jinsi gani wanavyoendesha.

Mhe. Naibu Spika, twende katika mambo ya rushwa, Mheshimiwa Dkt. alituletea mswada huu tukaupitisha na nilizungumza sana, jamani tunapitisha miswada

ambayo ni mizito na migumu lakini tunajiandaa, kwa kweli mimi ninawashukuru sana wanajitahidi sana.

Kwanza nishukuru wamepata jengo lao pekee hawachanganywi na mtu mwengine yeyote, moja hilo ninalishukuru sana, sasa iliyobakia ni *moderlity* kulitengeneza likawa zuri likavutia likaendana na dhana ile ya ofisi yenyewe inavyotakiwa.

Mhe. Naibu Spika, nimeomba hivyo, naomba sana kuwa lile jengo litengenezwe liendane na ile dhamira ya ile Ofisi yenyewe, bado Mheshimiwa sijafurahi nayo kwa sababu haijaniridhisha kutokana na hali halisi hasa ilivyo.

Lakini masuala mengine kama magari ninafikiria labda yako au sijui wale watu magari yao wenyewe, kwa sababu siku nilokwenda hukuta gari zinajipanga tele hujiuliza mimi mara ile washaanza kuwa na gari zao wenyewe, lakini naamini na wao watakuwa hizo gari ushawapa. Naomba hilo Mheshimiwa, niwaombee nao wapatiwe *special training*.

Mheshimiwa kumkamata mtu *red handed* kumwambia kala rushwa si kitu rahisi, hamuwapati, na sheria inakubaliana nayo hiyo. Lakini tuwaelimishe jinsi gani ambao watautengeneza ushahidi wao tosha utakaokwenda kule katika haki katika chombo cha sheria na ukakubalika, mafunzo hayo Mheshimiwa bado madogo, hili suala tusilidharau Mheshimiwa, kwa sababu kutokana na chombo hiki umuhimu wake lazima wapate mafunzo makubwa sana.

Nilikwambieni mimi jamani tunaunda lakini tujiundie tujifahamu, Mheshimiwa lugha kubwa hiyo sio tuamue tu hiki kitengo hiki kina thamani. Kitengo hiki Serikali imewekeza hapa, maana yake niseme ukweli kwa sababu mambo mengi sasa watu wanapiga kelele mitaani rushwa, rushwa mpaka kwenye nywele, rushwa mpaka pua, hii ni hatari. Sasa kwa kweli naomba sana.

Mhe. Naibu Spika, unajua kuna ukakamavu, sisemi ukakamavu kuwa sharti uwe na mwili, wengi wa chombo hiki nimewakuta wengine wembamba, si sababu hiyo lakini awe *serious*, ukimpika huyu, ukimpa mafunzo huyu si kitu cha mchezo kama wale watu wengiune wale wa *CID*. Tizama wale *CID* Mheshimiwa uliyemzoea *CID* hasa unapomkuta sasa hivi si mas-hara, utatishika jamaa anavyokuwa yuko *serious*, sasa na hao wawe *active* hivyo hivyo, wawe hivyo hivyo Mheshimiwa.

Mimi naomba sana bado tuwaongezee mafunzo hivi sasa na tuwapatie *radio* maalum, unajua kuna *radio* maalum sina haja ya kusema kuwa na wao wapate *mobile*, lakini wawe na *radio* maalum ambao wataelewana *code* yao wenyewe. Kwa sababu hawa wanavyotakiwa wawe wana-*run* katika *street* sio wangojee wapewe taarifa.

Na taarifa ukingoja ofisini Mhe. Naibu Spika, hawazipati ng'o, kwa sababu utangojea upewe, tunajuana sote wazanzibari, ningeomba Mhe. Naibu Spika, wawe na taaluma hiyo *just* wawe wenyewe wawe wanaingiana na watu. Unajua mimi napataje vitu kama hivi, napata vitu ambavyo ninawajibika na watu ninakaa na watu. Sasa wale watu wanaopita na matani ndani yake na kumbe na ndani yake wananambia kitu cha ukweli. Sasa mimi ningeomba sana.

Lakini neno la *traning* kwenye shehia bado ziko adimu. Mheshimiwa mmejitahidi sana kupita kwenye mashehia kusomesha, kuwaelimisha watu, tatizo letu la masheha ukishamuelimisha hana *meeting*, hana uzoefu wa kusema niite *meeting* ya wanashehia niwaelimishe kile kitu wanachokipata Mhe. Naibu Spika, hili tatizo kubwa sana.

Masheha wetu hawana ubunifu, nitakuja kutoa taaluma wakati ikifika katika wizara yake lakini namega kidogo awe *attention* kabisa, Waziri afahamu nitakapokuja nalo hilo. Hawana ile kuwa leo tumepata semina aidha ya chanjo turudi kwa wananchi wetu tuite *meeting* ya shehia nzima, nianze kwenye *committee* yake ili akaweza kulifikisha, hiyo Mheshimiwa hamna, na ndio maana tunakuwa masuala haya watu wengi wanauliza.

Mheshimiwa ninasikia kuna kitengo cha rushwa kina madhumuni gani, sasa unaona matatizo hayo, badala ya wao waelimishwe na sheha mimi nirekebishe, hawaoni tabu Mheshimiwa watwite, na sisi kama wao halafu tatizo lenyewe masheha sasa wakishapata semina hawatwiti sisi wakatwambia, jamani ee tumepata semina Mhe. Mbunge au Mhe. Mwakilishi tunaomba hebu mtusaidie kuitisha muje kuelimisha na nyinyi ili tupate baraka, hafanyi hivyo Mheshimiwa hata siku moja.

Sasa hilo linakuwa ni tatizo, kwa hivyo mimi naomba sana Mheshimiwa jitahidi Dkt. Mwinyi shuka chini msione tabu, tena wanapotoa funzo lao wawe *serious*, wawaambie jamani sisi tutakuja kukagua hivi leo nendeni kakagueni lazima mtakuja kunambia hapa hapa, waende shehia yoyote wakakague wakaulize jamani ee tuitieni wananchi haraka sana, halafu watasemaje. Watasema sisi hatujapata mafunzo hata siyajui.

Sasa hayo inakuwa tatizo kubwa sana, na tatizo likiwa kubwa basi inakuwa hatari, kwa hivyo mimi naomba kuwa tuwapeleke katika *training out the country* ili waweze kufanya mafunzo zaidi ya ukakamavu na uweze kutumia neno ambalo litaweza mtu kumtia hatiani kutokana na *psychologist* ambayo atakwenda kusomeshwa kule. Hilo nimeona niwape na wao *chance* hiyo niwapigie debe hilo. Kwa maana hiyo hata bajeti yao tuiangalie kwa maradufu, tuiangalie tena uwezo wa kuweza kuongezwa bajeti yake haijawa nzuri sana.

Mhe. Naibu Spika, niingie katika ukurasa wa 50 katika mradi huu ambao wa *PPP*, kwanza nimshukuru sana Katibu Kiongozi wametupa semina nzuri sana kuhusu habari ya maelekezo madhumuni ya *PBB*.

Nimshukuru sana Mhe. Rais kukubali suala hilo. Na muundaji wa jambo kama hili huyu ni mtu ambaye ana historia ya Zanzibar, ataweka historia ya Zanzibar ikiwa Katibu, ikiwa Naibu Katibu, ikiwa Waziri mwenyewe hapa mumeweka historia ya Zanzibar. Kwa sababu unajua Mheshimiwa unapoleta kitu kikawatumikia wananchi, kikawaeleza madhumuni wa jambo hili *alhamdulillahi* sema wewe *minalfaidhina*, kama Waziri wangu wa Fedha alipotuletea *program* hii ya *PBB* na yeye amejiwekea historia, ataondoka hapa au atarudi tena Mwenyezi Mungu amrudishe tena, lakini historia kaleta kitu *program* mpya, bajeti mpya ndio maana tunashindwa kui-*judge* na yeye anazidi kutuelimisha.

Sasa hii Mhe. Naibu Spika, niseme kuwa Dkt. hapa ameona suala zuri sana, *PPP* ni nzuri sana lakini sitaki kuitoa kasoro nataka niongezee kasoro zisitokezee.

Mhe. Naibu Spika, sisi hapa tuna mtindo. Sisi hapa tuna miradi ambayo inakuwa hapa Zanzibar watu wengi wanajitokeza lakini hatimaye inakuwa tunakwenda *slow* sana. Sasa mimi ninaamini chombo hiki, kwa mtazamo huu wa Dkt. mwenye *PHD* sidhani kitakuwa kitu kama hiki hakitokuwa kina mshangao hakitokuwa kinarega rega.

Mimi ninaamini litafanyika jambo la *faster*, na maendeleo ya nchi yetu yatatokezea, uchumi uko hapa sasa, utajiri wa nchi uko hapa, wanapokuja wawekezaji tukapunguza urasimu, tukapunguza kuwadai rushwa, tukawaelekeza kwa mujibu wa sheria na sheria zetu zipungue makali.

Lakini mimi nikuombe Mheshimiwa wangu, *wallahi* nataka nikuombe kwa upole, tena nenda kwa Mhe. Rais, *wallahi* Mhe. Rais ni mtu mzuri sana Dkt. Shein. Nataka nitoe hadithi kidogo Mhe. Naibu Spika, naomba kwa ruhusa yako.

Mimi nina mwanangu alinipa mtihani sana karibuni kama wiki mbili nyuma, ananambia baba kwa nini mimi usinite Dkt. Shein, mimi nikamshangaa yule mwanangu yeye anaitwa Thani lakini anataka lazima nimgeuze jina nimwite Dkt. Shein, mimi nikamuuliza na mtoto wenyewe ni mdogo sio mkubwa sana kwa akili zake, akanambia nimempenda sana mimi Dkt. Shein Rais wa Zanzibar kwa sababu ana mambo mawili mpaka matatu mimi yameniridhisha, yamelingana na yeye ati anasema yamelingana na yeye yule mtoto mdogo tu kabisa, tizama hiyo hali halisi, malaika anavyompenda Rais wa Zanzibar alivyokuwa mzuri.

Ananambia kwanza msikivu, hilo jambo kubwa sana. La tatu akihamaki utajua kama kweli kahamaki. Sasa hizi *criteria* zote mwanangu anasema yeye anazo, na madhali anazo kwa hivyo nimwite Dkt. Shein. Nikamwambia sawa mwanangu sasa ongea na mama yako mimi nikugeuze jina hakuna tatizo nitakwita tu wewe Dkt. Shein, kwa sababu umempenda hata mimi nimempenda. Na hayo ndio anayo Rais wetu kweli ni msikivu, sasa kama ni msikivu naomba sana unipelekee salamu zangu.

Mhe. Naibu Spika, kuna Mradi huu wa *Sacrona* ningeomba sana pamoja na kwamba tuko katika *waiting list* ya kusubiri hiyo *study* ya *UN* basi *at least* angefanya kwa sababu fedha zimeshatengwa *special* Zanzibar, America wametuona Zanzibar tatizo letu.

America wenzetu wametuona kuwa Afrika kuna giza lakini giza zaidi liko ndani ya Zanzibar wametutengea fedha nyingi sana Mheshimiwa. Kwa hiyo, naomba sana kwa upole kabisa *at least* akukubalie isainiwe *MOU* tu, ikishasainiwa wale kule wawe na imani kabisa kwamba Zanzibar imeshafanyiwa *MOU* ya Mradi wa *Sacrona*. Ningeomba sana Mheshimiwa na yeye ni msikivu, na yeye anaipenda miradi, kwa sababu anajua miradi ikija na yeye ndio sifa inazidi kuwa kubwa na ushindi unakuwa mkubwa. Kwa hiyo, mimi ningekuomba Mheshimiwa wangu Dkt. Mwinyi mpelekee salamu hizi wala usimfiche, *wallahi* mtu huyu kama nilivyokwambia hana tatizo. Tatizo sisi tu tunamuogopa lakini hatishi, basi ningeomba sana Mheshimiwa hili *message* imefika hiyo pengine mwenyewe ananisikia anakungojea wewe sasa. Sasa tatizo la mwenyewe Rais kama hukumpelekea anaanza kukuuliza wewe itakuwa aibu, Dkt. itakuwa aibu kabisa akianza kukuuliza wewe.

Mhe. Mwenyekiti, nizungumzie suala la *Diaspora* sasa. Mhe. Naibu Spika, hapa nilikuwa nina mawazo *Diaspora* yetu hapa Zanzibar na kila mtu Mheshimiwa anakuwa na ufahamu wake na akili yake inavyomjenga katika hisia hasa katika kujenga nchi yako ilete maendeleo.

Hii *Diaspora* tuseme ushauri wangu katika mwaka atakayekuja tena atapoingia tena Mhe. Rais wa Zanzibar hebu afanye wigo au upanuzi zaidi aiunde wizara *special* inayohusiana na masuala ya mambo ya watu wa nje. Mhe. Naibu Spika, hapa itakuwa tumefanikiwa *hundred percent* katika kuwaenzi.

Mhe. Naibu Spika, *Diaspora* nchi za wenzetu Philippine, Ethiopia hawa sasa hivi wanatajirika kwa sababu hawa sera zao ni nzuri wameziweka. Kwanza tumuombe Mhe. Rais awapokee bila ya *visa* hawa watu, ni ndugu zetu Mheshimiwa, huko wamekwenda kutafuta maisha ili watuletee maisha tukubaliane nao Mhe. Naibu Spika. Kwa hivyo, nimuombe sana Mhe. Rais kwa hili hapa atapounda serikali

yake katika uchaguzi keshokutwa anaposhinda, basi na hili alitafutie nafasi ya kulipa wizara yake hili ni jambo ambalo zuri.

Mhe. Naibu Spika, unajua mimi namshukuru sana *wallahi* Mhe. Naibu Spika, juzi nilisema suala la Wakurugenzi watangazwe wa mazingira na nini. Mimi nimo ndani ya gari ile natoka Barazani hapa Mhe. Naibu Spika nasikia Rais anatangaza haki ya Mungu nakwambia. Nilisema suala la vikosi hapa vile vile yule pale Mheshimiwa wangu amekaa pale vizuri tu haikuchukua muda akatangaza, eeh kwa sababu yule ni binadamu anajua sisi waheshimiwa wake hapa ndio wawakilishi wake tunazungumza *point*.

Sasa mimi ningeomba sana Mheshimiwa mwaka kesho lazima hili suala tunaomba ili aweze kutusaidia kuweza kufanikisha. Sasa hii *Diaspora* Mheshimiwa iwe na nguvu ya kuweza hapa kwenda kutafuta kazi nje kuzileta ndani ya nchi, tuwe na *power* hiyo Mheshimiwa. Tuunganishwe makampuni ambayo yaliyokuwa yameshafanya *registration* Zanzibar waliokuwa wamefanya kwa hakika, kwa sababu kuna kampuni nyengine Mhe. Naibu Spika, zinafanya kwa hakika zimetambulikana na zinaitwa tu majina yako wazi ni *Zanzibar Life Opportunity*. Sasa hiyo ndio tunaweza hii *Diaspora* Zanzibar ikaanza ni kichocheo cha kuitumia, cha kuifanyia kazi vizuri, cha kukusanya vijana kuwatafutia kazi nje wakatuletea maendeleo Mheshimiwa.

Mhe. Naibu Spika, na ni kweli kwa sababu wakati ule *Danaus* ina watu wale wanafanya kazi nje lakini wametumia Benki ya PBZ, tizama dola wanavyozileta, tizama kazi inavyofanya vizuri na ndio tunavyotaka Mheshimiwa. Sasa mimi nafikiria Mhe. Naibu Spika si vibaya na hii kampuni mpya ya *Zanzibar Life Opportunity*, *Diaspora* hapa Zanzibar kwa kuwa na wao wamejitangaza basi ingeweza kuwachukua na kuwafanyia ziara.

Mhe. Naibu Spika, kweli ndio maana nikasema hapa fungu lao hili dogo, kwa sababu panatakiwa pesa za kuwatoa watu kama hao una Maafisa wazuri tu, mbona una Maafisa wazuri wako na wanajua kuzungumza, wakienda nje wana-*act*, wana-*organize* vizuri *Diaspora* za nje, wanawaitikia. Sasa Mheshimiwa nalo hili tusiwe wabahili la kutoa fedha kama hizi tukavitafuta vikundi ambavyo kama hicho cha uhakika si cha pembeni.

Mhe. Waziri Haroun alizungumza leo pale nataka nimsaidie. Mhe. Naibu Spika, kweli kuna kampuni ambazo za kiutapeli, hizo zipo hawataki kuji-*register* wanachukua watu kimagendo gendo wakifika kule wanapata matatizo. Nani muokozi hajulikani, watu wananyang'anywa mapesa chungu nzima hapa wakienda kudai hawapati haki yao. Sasa hayo mimi nimekubaliana na Mhe. Haroun futa kampuni kama hizo za udanganyifu hatuwezi kukaa nazo hapa.

Kwa hiyo, Mhe. Naibu Spika, mimi niombe sana kwa hii *Diaspora* tuitafutie wizara yake wakati Mhe. Rais Dkt. Shein anapokuja kushinda, *inshaallah* Mwenyezi Mungu atampa uwezo wa kushinda, basi aweze kuiunda hii *Diaspora* ili waweze kusaidia kuleta ufanisi mzuri na hasa kwa vijana wetu, kwa sababu sasa hivi serikali ina mzigo mkubwa sana.

Mheshimiwa serikali ina mzigo mkubwa sana, lakini wenzetu nchi za nje huko wanayatumia sana makampuni yaliyokuwa yamejiimarisha vizuri kwa kuyapa kazi, kuondoa kazi katika mzigo wa kuondolea serikali. Hata bajeti yake inakuwa inapungua katika wizara husika, tayari imepunguzwa jambo ambalo lilokuwa ni muhimu imepewa kampuni ya kutofanya kazi. Huo ndio utaratibu na ndio utakuta wenzetu sasa wanaendeshwa na makampuni, miradi mikubwa sana makampuni inaendesha kama mtindo ule ulokaa *PPP*, lakini na hii kwa kutafuta ajira Mheshimiwa unatupunguzia mzigo. Mhe. Naibu Spika, vijana wengi hawana kazi sasa hivi, kwa hiyo Mwenyezi Mungu atujaalie tuweze kufikisha malengo.

Mhe. Naibu Spika, nimalizie niingie katika hii dhana ya Utawala Bora. Mhe. Naibu Spika, nimpongeze sana Dkt. Mwinyi kuna kitabu hiki hapa sera ya utawala bora watu wengi hawajui nini maana ya utawala bora, hata humu viongozi wengine hawajui nini maana ya utawala bora. Sioni shida kuelimisha kwa sababu unapopata kidogo unaambiwa kitolee sadaka kwa mtu ili uweze kuimarika zaidi.

Naomba ninukuu sentensi moja Mheshimiwa “anakuuliza misingi ya utawala bora uwajibikaji na uwazi”. Sasa naingia ndani Mheshimiwa nistahamilie kidogo tu “uwajibikaji” maana yake ni madaraka yanayotumika ndani ya jamii na Taifa kwa jumla, na pia ni wajibu kwa wenye madaraka kutoa maelezo ya maamuzi yao.

Mhe. Naibu Spika, Waheshimiwa Mawaziri wengi tunashindwa kutoa maamuzi takriban mawaziri wadogo iko siku nitawataja hapa wanistahamilie kwa sababu kitabu hiki tumekitunga wenyewe kiko chini dhamana ya Dkt. mwenyewe. Dokta amesoma mambo mengi sana hakubuni tu hiki ovyo ovyo ameleta kina mantiki yake. Kwa hiyo, tunashindwa mawaziri kutoa maamuzi, tuna-*delay* kutoa maamuzi wakati wewe ni waziri ndiye mwenye mamlaka pale katika *department* zako, lakini tunashindwa Mheshimiwa, ikija karatasi au barua basi anaiweka pale imekwisha kazi, hatujawajibika. Mhe. Naibu Spika, tunapata matatizo sana hii dhana hii hatujaifuata.

Mhe. Naibu Spika, mimi husema siku zote tunatunga sheria hatuziangalii, tunaleta sheria lakini hatuziangalii zinatupiga wenyewe, kwa sababu tukija ya pili kama utawala wa sheria na haki za binadamu. Lakini ya tatu kuzuia rushwa, ufanisi, tija na ushirikishwaji, sasa hii ushirikishwaji tunashindwa kuwashirikisha jamii katika kuleta ufanisi wa mambo ya maendeleo na kila kitu.

Sasa mimi niombe tu jamani tufuate hizi sheria tunazoziunda hapa sera zetu wenyewe nzuri tu hizi Mheshimiwa. Kwa mfano, kama ile sheria sijui kama Rais keshaitia saini Sheria ya Maadili. Mhe. Naibu Spika, ningeomba sana ile sheria mpaka leo nadhani haijatiwa saini, kama imetiwa saini haijatiwa saini hapa ndipo pahali pake tumalizie tunaondoka na sheria iwepo, watu watakaoanza sheria ifuate mkondo wake.

Mhe. Naibu Spika, ninaomba sana Mhe. Rais atutilie saini ile sheria ifanye kazi, tulifanyia kwa sherehe kubwa sana hapa, tulipata taaluma kubwa sana hapa. Sasa mimi naomba sheria hiyo iweze kutiwa saini, maadili na hii haikutupana sana Mheshimiwa. Mhe. Naibu Spika, maadili na sheria hii ya utawala bora haikutupana sana. Kwa hiyo, naomba sana ili kwa kuweza kufanikisha vizuri sheria tuweze kuletewa.

Mhe. Naibu Spika, nikushukuru sana, nawashukuru viongozi wote walionisikiliza kwa makini na nimalizie kumpongeza sana Dkt. Ali Mohamed Shein azidi kuendeleza na jambo la bango kitita na hasa katika wizara hii, bango kitita nasema limepangiwa *hundred percent*. Kwa kweli limepangika Mheshimiwa si masihara, limepangiwa wizara hii humpati hata kwenye kitabu humu mimi kila nikitafuta wapi nitoe *comment* zake nashindwa kwa vile lilivyopangika.

Pia nimshukuru sana niseme kuwa *CAG* nimshukuru sana mama huyo, na yeye *Alhamdulillah* amefanya kazi zake kwa uadilifu tangu nilipokuwa na mimi ni Mjumbe wake na yeye nilikuwa sijapitia pitia nimshukuru sana kwa uadilifu wake mzuri wa kazi mpaka sasa hivi *Alhamdulillah* tunakwenda naye vizuri, na hivyo ndio inavyotakiwa, kwa sababu unafika pahali unastaafu kazi basi jina na huyu mama niseme anaacha jina katika nafasi yake ya u-*CAG*. Hilo nalo nimpongeze sana kabisa, tena nimpongeze sana, kwa sababu ningemsahau ningefanya makosa, kwani kina mama na wao wanataka kuwa mstari wa mbele, nashukuru leo Makatibu wako wawili hao wapo nao wamesoma wote, leo ripoti ni wanawake watupu, *fantastic* wamesoma vizuri sana na haki yao tuwape Mheshimiwa mimi sina uchoyo.

Tatizo uchoyo mimi sina lakini haki yao lazima Mheshimiwa tuwape, wameelimisha leo mama kule kasoma vizuri na hapa Mheshimiwa kasoma vizuri sana. Makatibu wako halikadhalika halafu huyu mama ambaye serikali nzima anayo yeye na mpaka leo hajatetereka, aah kwa kweli Mheshimiwa naye nimpe pongezi kubwa sana, na Mwenyezi Mungu azidi kumzidishia umri mrefu wenye salama na yeye, ili aendeleze kutudhibitia hesabu zetu asiogope pale anapoogopa. Asiogope pale anapoona nani kaiba pesa na aseme tu tutamlinda sisi, tutamsaidia hapa na mimi aniombee dua ili nirudi nizidi kumlinda katika utekelezaji wake.

Mhe. Naibu Spika, mimi naiunga mkono mia kwa mia wala sipunguzi theluthi moja. Kwa hayo, machache ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kunipa nafasi hii, na kwa kweli nina mchango mfupi sana na wala siingii kwenye mahesabu leo. Nilipoangalia mahesabu ya kitabu hiki naona yameandikwa zaidi kitaalamu, na kwa hivyo sitaki niyaguse kwa sababu nimeridhika nayo. Naomba nitoe mchango wangu kiasi ya kutoa tahadhari na wasia kwa waziri kaka yangu Dkt. Mwinyi ili iwe ni sehemu ya kumbukumbu ya Baraza hili kwa siku za mbele.

Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa nianze mchango wangu kwa kumpongeza sana Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete kwangu mimi Mhe. Kikwete nikiambiwa nimkumbuke kwa mema aliyoyafanya basi la kwanza nitasema kwamba Mhe. Rais Kikwete amewaunganisha Wazanzibari pale aliposimamia maridhiano ya kisiasa. Kwenye maisha yangu nikiambiwa tupe mchango wa Rais Kikwete kwa Zanzibar, nitasema kwamba la mwanzo amewaunganisha Wazanzibari pale alipowasaidia kufikia maelewano ya kisiasa mwaka 2010.

Mhe. Naibu Spika, jana Rais Kikwete alizungumza na Mabalozi na kama sikosei alisema maneno yafuatayo naomba ninukuu.

“Mhe. Rais alisema kwamba yeye amerithi nchi hii ikiwa na amani na ataondoka ikiwa na amani kamili”.

Mhe. Naibu Spika, hili ndio jambo ambalo ninaendelea kumshukuru sana Mhe. Rais, kwamba nchi hii ya Tanzania ameirithi ikiwa na amani na anatarajia kuondoka mwezi wa kumi *inshaallah* ikiwa na amani. Lakini amani hiyo ni pamoja na mchango mkubwa wa maelewano ya Wazanzibari chini ya *GNU*. Sasa Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu ningemuomba hilo alizingatie, kwamba nchi hii Rais wa Jamhuri ameirithi ikiwa na amani na anatarajia kuondoka ikiwa na amani. Je, Rais wa Zanzibar nini matarajio yake? Hili ni suala ambalo linahitaji tafakuri ya hali ya juu, ili amani ambayo Rais Kikwete anatarajia kuiacha basi iwe ni amani ambayo itaendelea hasa visiwani.

Mhe. Naibu Spika, nasema hayo kwa sababu tunategemea kuingia kwenye Uchaguzi Mkuu mwaka 2015 mwezi wa 10 huu, lakini kila ninavyoangalia kwa wale waganga wa kienyeji husema kwamba ninavyoangalia dalili za nyota naona zinaelekea kubaya. Sasa ni jambo ambalo wanadamu wenye akili timamu lazima watafakari sana, na waweke tahadhari ili siku moja watu waseme kwamba yule mtu wa Kiwani siku moja alisema kwamba tusipokuwa makini kwenye uchaguzi unaokuja, Ofisi ya Rais kama haikutusaidia kwenye uchaguzi unaokuja basi mema

yote haya ambayo Rais Kikwete leo anajivunia yanaweza yakawa machungu na watu wakajutia.

Nasaha zangu kwa Mhe. Waziri ili amsaidie Rais kutafakuri sana, ili nchi yetu iendelee kubaki na amani, Wazanzibari wabaki na maelewano, ili iwe nyenzo muhimu ya kufikia maendeleo ya Wazanzibari; Unguja na Pemba.

Mhe. Naibu Spika, hiyo ndio tafakuri yangu ya kwanza ambayo ningetoa wasia kwa Mhe. Waziri ili na wataalamu wake waitafakari sasa, nini mchango wa ofisi yake kwenye kufikia malengo ya amani hasa kwa viashiria ambavyo sasa hivi vipo. Viashiria vingi vipo vinaonesha kwamba kama hatukuwa makini kama serikali, kama mawaziri hamkumsaidia Rais basi amani hii iliyopo inaweza ikaharibika siku moja, kwa sababu viashiria vinaonesha kwamba watu wanaelekea kubaya.

Mhe. Naibu Spika, hoja yangu ya pili ni kupongeza Serikali ya Oman. Jana kumenukuliwa na vyombo vya habari kwamba Serikali ya Oman kupitia Ubalozi wake imekabidhi bilioni 12.5 kwa Zanzibar ambapo ni mchango kwa ajili ya matengenezo na ujenzi wa Kiwanda cha Upigaji Chapa. Kwa niaba yangu binafsi na kwa niaba ya wananchi wa Kiwani naomba niipongeze Serikali ya Oman kwa mchango huo mkubwa.

Tafakuri yangu ya pili kwa hili Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya Rais Ikulu ishirikiane na Ofisi ya Rais Fedha ilinde matumizi ya fedha hizi ili malengo ya fedha hizi zifikie kwa wananchi, na malengo ya fedha hizi zifikie kwa Ubalozi wa Oman ambao wametoa fedha hizi. Tukiwaachia fedha hizi zikielea elea tu, basi malengo ambayo Balozi na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wameyakusudia ya kujenga Kiwanda cha Uchapaji cha Zanzibar itakuwa hayafikii ufanisi uliokusudiwa.

Mhe. Naibu Spika, *page* ya 3, *paragraph* ya 9 waziri ameanza kupiga kampeni kwamba anawaomba Wazanzibari Katiba Mpya waipe kura ya ndiyo. Nadhani hakupaswa aseme hivyo, ilikuwa awaombe Wazanzibari tu kwamba ikifika kura ya maoni wakapige kura, kwa sababu wakati wa kampeni haujafika, leo anawalazimisha Wazanzibari wapige kura ya ndiyo, nadhani alipaswa tu awaambie Wazanzibari kwamba ikifika kura ya maoni wakapige kura, na ule muda wa kampeni miezi mitatu ukifika ndio yeye angepaswa sasa kuwaambia Wazanzibari wapige kura ya ndiyo au hapana. Nadhani hii sentensi ya kupiga ndiyo ilikuwa si pahala pake kwa leo, ilikuwa yeye awaombe Wazanzibari ikifika siku ya kura ya maoni wakapige kura. Kwa sababu kuna kipindi cha kampeni kuna kundi watasema ndiyo, kuna kundi watasema hapana, maana yake ukiandika hivi mimi nitasema Wazanzibari wapige kura ya hapana, itakuwa si lengo la hotuba yake ya bajeti. Nadhani ilikuwa haijafika muda wake, na hilo alitafakari ipasavyo.

Mhe. Naibu Spika, ukurasa wa saba Mhe. Waziri ametuelezea hapa kwamba, serikali imetekeleza misingi ya utawala bora, *paragraph* ya 16 imeeleza hayo na misingi hiyo Mhe. Naibu Spika, ni uwazi, uwajibikaji, ushirikishwaji, utawala wa sheria na ujumuishaji.

Mhe. Naibu Spika, mimi kwa kiasi kikubwa nasema kwamba haya yapo, lakini yapo kwa sababu, ili kuwe na uwazi na uwajibikaji na ili kuwe na utawala bora maana yake kuwe na sheria nzuri. Zanzibar tuna sheria nzuri, zipo sheria nzuri, sera nzuri ambazo tumezipitisha Baraza la Wawakilishi na Baraza la Mapinduzi zipo, na Katiba yetu inaashiria kwa kweli ni katiba moja nzuri sana. Lakini mapungufu yetu ambayo tunayo Zanzibar ni udhaifu, nidhamu ndogo ya kuheshimu ile misingi ya demokrasia. Sasa kuwepo ni jambo moja, lakini kusimamia misingi hiyo ni jambo la pili. Naungana na Mhe. Waziri kwamba misingi ya utawala bora Zanzibar hii minne; uwazi, uwajibikaji, ushikishwaji na utawala wa sheria ipo. Lakini je, nidhamu ya kulinda misingi hii ipo?

Mhe. Naibu Spika, kwa mtazamo wangu hapa ndipo ambapo Wazanzibari tumejikwaa, nidhamu ya kusimamia misingi hii ya utawala bora haipo, na kwa msingi huo unaweza kusema kwamba hapana misingi ya utawala bora. Kwa sababu kuwepo na kutosimamiwa ni udhaifu, sasa kuwepo misingi hii ni jambo moja na kusimamia misingi hii ni jambo la pili. Kwa mtazamo wangu hapana usimamizi mzuri wa misingi ya utawala bora.

Mhe. Waziri ofisi yake, Ofisi ya Rais nadhani ingezidisha bidii ya kusimamia misingi ya utawala bora, ili unapozungumza misingi hii basi iende sambamba na uhalisia wa mambo ulivyo.

Mhe. Naibu Spika, hoja yangu nyengine *paragraph* ya 17. Mhe. Waziri ametueleza hapa kwamba Rais ameanzisha utaratibu wa kujitathmini kwa kutumia utaratibu wa Bango Kitita. Mimi nasema kwamba ni utaratibu mzuri ambao Rais aliubuni, na kwa kweli ulikuwa na nia njema, lakini kwa mtazamo wangu Mhe. Naibu Spika, utaratibu huu kwa hivi ulivyo bado unaendelea kumdanganya Mhe. Rais.

Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania au (*SMT*) kwa upande wa wenzetu wana mradi wa *Big Results Now*. Ule mradi mtu mwenyewe anatathminiwa bila kujijua, lakini unapomwambia leo Hija Hassan njoo nikutathmini, maana yake niandike ninachokipenda kwa ajili ya kukinga kukosolewa. Ushauri wangu Mhe. Naibu Spika, kwamba Rais wa Zanzibar huu utaratibu ambao ameuandaa, nadhani aurekebishe vizuri zaidi, nisiseme auboreshe, niseme aurekebishe vizuri zaidi, ili sasa wanapotathmini wale watu wasijue kwamba mimi nimefanyiwa nini, lakini leo ukimwambia njoo utupe ripoti ya miezi

mitatu ataandika kujilinda. Kwa upande wangu Mhe. Naibu Spika, nadhani huu ni udhaifu.

Sasa Mhe. Waziri nakushauri kwamba kipindi kijacho cha serikali ijayo basi muige ule mfumo wa wenzetu Tanzania Bara ambapo mradi wa *Big Results Now* ndio mradi ambao unatathmini utendaji wa serikali bila ya mtu kujua vipi anahojiwa.

Mhe. Naibu Spika, hoja nyengine ambayo nataka nizungumze ni Ofisi ya *CAG*. Wawakilishi wengi hapa Zanzibar wamekuwa wakilalamika kwamba Ofisi hii ya *CAG* imekuwa na udhaifu wa wataalamu mara kadhaa. Lakini kwa mujibu wa ripoti ya Mhe. Waziri kwamba *value for money audit* kuna wafanyakazi 50, *risk base audit* kuna wafanyakazi 30, *IT audit* kuna wafanyakazi 25 na ukaguzi yakinifu kuna wafanyakazi 3 na jumla ya wafanyakazi wataalamu hawa ni 108. Mhe. Naibu Spika, binafsi yangu napongeza nguvu kazi hii ambayo kwa kweli imesaidiwa kujenga uwezo Ofisi ya *CAG*. Sasa kuwepo kwa wataalamu ni jambo moja, lakini ifuatiliwe na kuwepo kwa vitendea kazi vya kisasa na maslahi mazuri ya wafanyakazi hawa.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri nikuombe tu kwamba licha ya kwamba wataalamu hawa umewasomesha mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu, lakini yaende sambamba sasa na vitendea kazi vya kileo, sambamba na maslahi mazuri ya ofisi ya *CAG*. Hili ndio jambo ambalo Mhe. Waziri nitataka baadaye unipe ufafanuzi vipi umezingatia maslahi yao. Najua mpango ule wa *scheme of service* ya *CAG* umerekebishwa, lakini tuione basi imekwenda vipi, ilinganishwe na ofisi nyengine za *CAG* Tanzania na Kikanda ili iende sambamba na utendaji wa ofisi hii kitaalamu na kivifaa.

Mhe. Naibu Spika, mwisho kabisa niseme tu kwamba ukurasa wa 55 kifungu cha 151, Mhe. Waziri hapa ameeleza kwamba mpango wa *PBB* utazingatia mambo 15 ambayo yameelezwa. Mhe. Naibu Spika, nahisi binafsi kwamba mambo hayo 15 licha ya kwamba ni ofisi ya Rais ni ofisi kubwa, ni ofisi ya mkuu wa nchi, lakini kwa utaratibu wetu wa fedha unavyoingizwa, nadhani kwamba hayo mambo 15 ni mazito na ni mengi sana. Kwa hivyo, ningehisi kwamba ungechagua mambo angalau 10 wakayapa kipaumbele, hatimaye tukayapima yale 10 kuliko kuweka mambo mengi, baadaye wakasingizia uchache wa fedha hatimaye hatupati ufanisi wa hali ya juu.

Mhe. Naibu Spika, nilidhani kwamba mambo hayo 15 Mhe. Waziri na wataalamu wake wangekaa wakaangalia ni yapi mazito ambayo ni muhimu zaidi wakayapa kipaumbele na hatimaye wakayachagua hayo, ili mwakani 2016/2017 tukawapima vipi wametekeleza mambo haya ndani ya mfumo huu wa *PBB*.

Mhe. Naibu Spika, baada ya wasia wangu huo, hasa wasia wa kuilinda amani ya Zanzibar, naomba niunge mkono hoja hii na nikushukuru Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Naibu Spika, nashukuru na mimi kupata nafasi hii na leo nitazungumza kwa ufupi tu, katika kutoa mchango wangu katika hotuba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Ikulu na Utawala Bora, hotuba ambayo inahusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2015/2016 katika Baraza lako Tukufu, yaani Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Naibu Spika, kabla ya kuchangia chochote, kwanza nitoe pongezi za aina yake kwa Mhe. Mjumbe wa Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi (*PAC*), Mhe. Salma Mussa Bilal, kwa usomi wake uliofahamika na hasa katika yale maneno ambayo yaliandikwa kwa Kiingereza. Nampongeza alipowasilisha hotuba yake ya (*PAC*) tumeifahamu vizuri sana.

Pia Mhe. Naibu Spika, natoa mkono wa pole kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa kufiliwa na dada yake mpenzi kama wajumbe wengine waliotangulia kusema, pamoja na kuwa sisi ni viumbe na tutakwenda huko huko, lakini kama mwenzetu ametangulia mbele ya haki, basi sisi tuliopo katika uso huu wa dunia hakuna zawadi kubwa ya kumpa isipokuwa ni kumuombea dua. Kwa hivyo, dua yangu fupi ni kwamba namuomba Mwenyezi Mungu amsamehe makosa yake mwenzetu aliyetangulia mbele ya haki, amrehemu na amuweke mahapa pema peponi pamoja na wote waliotangulia amin.

Baada ya hayo Mhe. Naibu Spika, naomba kuchangia kwa kuanza ukurasa wa kwanza, katika kifungu namba 4 cha hotuba hii ya bajeti, ambapo Mhe. Waziri kwa ufasaha kabisa alieleza kuwa mafanikio yaliyopatikana chini ya uongozi wa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi yameiwezesha nchi hii kuendelea kuwa na amani, utulivu na mshikamano mkubwa.

Mhe. Naibu Spika, mimi binafsi nashukuru kuwa hivi sasa tumo katika amani, tumo katika utulivu na tumo katika mashirikiano, ndio hata bajeti zetu tunazipitisha kwa pamoja kwa asilimia kubwa. Lakini Mhe. Naibu Spika, mimi uzoefu nilionao tokea baada ya kuanza mfumo huu wa vyama vingi, na hasa inapofika siku kama hizi tunazokaribia uchaguzi pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo, mara nyingi huwapo nguvu zinatumika za serikali dhidi ya wananchi, lakini kwa sababu wananchi ndio wenye amani hukubali na hali ikatulia.

Mhe. Naibu Spika, ni haki ya kila chama cha siasa kufanya mikutano yake ya hadhara kwa kufuata utaratibu uliowekwa, na ni wajibu wa vyombo vyetu vya ulinzi vinavyohusika kuona kuwa mikutano hiyo inafanyika kwa amani na utulivu,

na ni Katiba yetu iliyotuelekeza kuwa, kati ya watu ambao hawastahiki kujiingiza katika chama chochote cha siasa moja ni walinzi wetu.

Mimi sikufarajika na ninasema wazi wala sikuwa wazi, ile siku tuliyokwenda kule Kitope kufanya mkutano ikawa hata magari kule Upenja yakakatishwa, ili yasiwe katika msafara uliokuwa ukiongozwa na Makamu wa Kwanza wa Rais. Vile vile sababu ya kuzuiwa pale, na kwa sababu tuliambiwa kuwa mkutano utakuwa katika sehemu, sijui Kilombero kama nimekosea jina naomba radhi kwa hilo, nilikwenda ndio kule hakukuendeka tena. Kwa bahati mbaya pale kwanza kulikuja gari moja ya askari, halafu zikaja gari tatu. Gari kwa lugha fupi tunasema zilikuwa *well up,* kulikuwa na majibwa matatu na wao kama walivyosema pale Upenja, ni kuwa wameelekezwa mkutano ule usifanyike, na pale palikuwa pameshajengwa shamiana, kiriri na pameshakusanyika watu wote. Nikajiona sasa Salim Abdalla ndio mwisho wake wa kuishi katika dunia hii, nikajikaza.

Mimi Mhe. Naibu Spika, niliwauliza nyinyi ilikuwaje mkaja hapa. Wakasema tumetumwa kuja kuvunja mkutano. Mimi nikawaambia mmetumwa na wakubwa wenu na hawa watu hapa wameitwa na wakubwa wao. Kama ni kuvunja mkutano tu, kaeni na silaha zenu, kaeni na majibwa yenu na mimi kwa bahati nzuri haikutimia muda mrefu nikapata *message* tukafanya kazi na mkutano ule tukauondoa. Mkutano ni wa Makamu wa Kwanza wa Rais, kuvunjwa kiasi kile sio vizuri hata kidogo, kama ilikuwa isifanyike, kwa sababu tunakwenda na sheria kungetolewa taarifa mapema kuliko kwenda kuadhirika kule.

Kwa hivyo, linaloombwa waheshimiwa, hivi sasa tumo katika utulivu hakuna fujo lolote, tunaendelea vizuri, lakini tumo katika mchakato. Kwa heshima zote tunaiomba serikali wawe na ustahamilivu wa kisiasa, watu wanaohusika na wizara hii ya ulinzi waone kuwa wote ni binadamu tuna haki, na kuanzia leo tuone kuwa demokrasia inachukua mkondo wake kwa maslahi ya Wazanzibari wote.

Mhe. Naibu Spika, jengine ni mara nyingi hapa isipokuwa awamu hii iliyomalizika na nitoe shukrani zangu za dhati kwa Mhe. Rais Mstaafu Mhe. Aman Abeid Karume na Mhe. Maalim Seif Sharif Hamad kwa kukaa na kuona umuhimu wa kuwaunganisha Wazanzibari kuwa kitu kimoja na tukaungana. Lakini mara zote yanayotukabili sisi tukawa na matatizo ni matokeo yanayotangazwa na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, tukiangalia kifungu cha 34(7) katika ukurasa wa 23 wa Katiba hii ya Zanzibar ya mwaka 1984, toleo la mwaka 2010 linasema hivi;

"iwapo mgombea ametangazwa na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar kwamba amechaguliwa kuwa Rais kwa mujibu wa Katiba hii au kwa mujibu wa

kifungu hiki, basi hakuna mahakama yoyote itakayokuwa na mamlaka ya kuchunguza kuchaguliwa kwake" yaani kwa mujibu wa kifungu cha Katiba Tume inapotangaza ndio hivyo hivyo.

Mhe. Naibu Spika, vile vile tukifungua kifungu cha 119(13)(12) na (14), ukurasa wa 85 ambapo pia inazungumzia kuhusu Tume ya Uchaguzi, ni kuwa katika kifungu cha 119(12) kinasema hivi;

Kifungu cha 119(12)

"katika kutekeleza madaraka yake kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii, Tume ya Uchaguzi haitalazimika kufuata amri au maagizo ya mtu yeyote au idara yoyote ya serikali au maoni ya chama chochote cha siasa", yaani inafanya kazi yake itakavyo haiingiliwi.

Mhe. Naibu Spika, tukifungua kifungu cha 119(13), Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kunukuu, kinasema kuwa;

Kifungu cha 119(13)

"hakuna mahakama yoyote itakayokuwa na mamlaka ya kuchunguza jambo lolote litakalotendwa na Tume ya Uchaguzi katika kutekeleza madaraka yake kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii".

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe yote hayo yamo ndani ya bajeti hayo.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Naibu Spika, nakuja kwenye amani na utulivu. Sasa Mheshimiwa,

Mhe. Naibu Spika: Nakuomba sana twende kwenye bajeti.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Ahsante. Sasa Mhe. Naibu Spika, ili tuwe na amani na utulivu naomba hii Tume inayopewa madaraka zaidi ya Katiba, kuanzia sasa irekebishe kufanya kazi kwa haki ili isije ikatokea mgogoro ambapo mgogoro huo huwa unatudhuru sote. Kwa hivyo, naomba ijue kuwa imepewa mamlaka juu ya Katiba, japo kuwa imo ndani ya katiba lakini watumie ilivyo hii amani na utulivu tulionao uzidi kuendelea kwa sababu tumo katika harakati za uchaguzi. Hicho Mhe. Naibu Spika, ndio kifungu nilichokizungumza kifungu namba 4 kilichokuwa katika ukurasa wa kwanza wa Hotuba hii ya Bajeti na Mhe. Naibu Spika, naomba univumilie.

Mhe. Naibu Spika, tukiendelea tukifungua ukurasa wa tatu wa hii Hotuba yetu ya Bajeti ambayo ndani yake mna vifungu namba 7, 8 na 9. Vifungu vyote hivi vinahusu Katiba Mpya inayopendekezwa ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambayo Katiba hiyo hapa tuna Katiba inayopendekezwa na Katiba hii ndiyo itakayopigiwa kura ya maoni na ikishinda katika kura ya maoni kwa hivyo ndio Katiba itakayotumika.

Mhe. Naibu Spika, hapa mimi namuomba Mhe. Waziri anisikilize vizuri sana, hapa ninalotafuta mimi kwa sababu nina mambo nataka nielekezwe, kwa hivyo naomba univumilie kwa haya nitakayoyazungumza ili anipe maelekezo, na akishanipa maelekezo niweze kujua ni kwa namna gani vifungu hivi nilivyovitaja hapo vitalenga hali halisi iliyokusudiwa kwa sababu Mhe. Naibu Spika, tukifungua hii Hotuba yetu ya Bajeti kifungu cha 9 kinasema:-

"Sambamba na hilo naomba kuitumia fursa hii kutoa wito kwa Wazanzibari na Watanzania wote kwa jumla kujitokeza kwa wingi katika kura ya maoni ya kuipigia kura ya ndiyo Katiba inayopendekezwa inayolenga kupata ufumbuzi wa kudumu ya hoja za Muungano".

Mhe. Naibu Spika, kulikuwa na Tume ya Kukusanya Maoni, Tume ya Rais ambayo ilikuwa ikiongozwa na Mhe. Jaji Joseph Sinde Warioba wakati huo na mpaka sasa tunaendelea inafanya Tume ya maoni hiyo kuhusu Katiba mpya tunayo Katiba yetu ya Muungano.

Mhe. Naibu Spika, Katiba hii ya Muungano sehemu ya kwanza inaeleza kuwa Tanzania ni nchi moja na ni Jamhuri ya Muungano.Mheshimiwa wewe uko katika Baraza kwa muda mrefu, kuna wenzetu walisema kuwa Zanzibar si nchi kwa kifungu hichi, na kabla ya kuwa na Katiba hii kulikuwa na Katiba ya Zanzibar ambayo inaeleza kuwa Zanzibar ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano na huku Katiba ya Muungano inasema kuwa Tanzania ni nchi moja na ni Jamhuri ya Muungano.

Sasa tulipozungumza hili na kupiga kelele Mwenyezi Mungu amrehemu Mwanasheria wetu Mkuu tuliyekuwa nae Mhe. Iddi Pandu Hassan alitwambia subiri na mtaona. Namshukuru Mwenyezi Mungu ikafanywa hiyo kazi na mwisho tukapata Katiba hii. Katiba hii inapingana na ile kwa sababu inavyoeleza Katiba hii mpya tuliyonayo ambayo nashukuru imetungwa kitaalamu na ina sehemu nyingi haziwezi kurekebishwa isipokuwa kwa kura ya maoni.

Katiba hii ilisema Zanzibar ni nchi ambayo eneo la mipaka yake ni eneo lote la Visiwa vya Unguja na Pemba pamoja na visiwa vidogo vidogo vilivyozungukwa

na bahari yake ambayo kabla ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ikiitwa Jamhuri ya watu wa Zanzibar.

Tumetoka kule kuwa Zanzibar ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano tukakileta kifungu hichi kwa makusudi kikaongezwa kifungu cha pili kuwa Zanzibar ni miongoni mwa nchi mbili zinazounda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, naviruka vifungu vyote tukaja kifungu cha 4 ambacho kinasema Katiba hii ni Katiba ya Zanzibar, na itakuwa na nguvu za kisheria nchini kote na isipokuwa kutokana na kifungu cha 80 ambacho kina vifungu ambavyo haviwezi kubadilishwa na Baraza la Wawakilishi isipokuwa kwa kura ya maoni.

Vifungu ambavyo Baraza la Wawakilishi ikipatikana theluthi mbili wanaweza kurekebisha haya mambo ambayo hayaharibu maudhui yaliyokusudiwa katika vifungu mama. Ikiwa sheria yoyote inayotafautikana na Katiba hii basi Katiba hii ndiyo itakayokuwa na nguvu, na sheria hiyo itakuwa batili kwa kiwango kile ambacho kitahitalifiana.

Mhe. Naibu Spika, ilipokuja Tume kwa kuangalia Katiba ya Zanzibar na wale ni wataalamu wakaangalia Katiba ya Muungano na utaalamu wao walipendekeza kuwa baada ya kuwa na neno kuwa ni Tanzania ni nchi moja na ni Jamhuri ya Muungano tuwe na Muungano kama ifuatavyo:-

Kama tunafahamu sote ile Rasimu ilipendekeza kuwa kuwepo na Serikali ya Zanzibar yenye mamlaka kamili, kuwepo na Serikali ya Tanganyika yenye mamlaka kamili na kuweko na shirikisho la mambo 7 yaliyopendekezwa. Tumefanya marekebisho tumekwenda lakini sasa *point* yangu iko hapa Mhe. Naibu Spika.

Kwa vile tumeondoka kuwa Tanzania ni nchi moja na Jamhuri ya Muungano ikafatiwa na Katiba hii ikaleta utata sasa hivi kuleta kifungu hichi kinachosema kuwa :-

"Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni nchi yenye Mamlaka kamili ambayo inatokana na Muungano wa nchi mbili za Jamhuri ya Tanganyika na Jamhuri ya Watu wa Zanzibar ambazo kabla ya hati ya Muungano ya tarehe 22 Aprili 1964 zilikuwa nchi huru".

Hivi kusema Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni moja yenye mamlaka kamili mimi naona inatuziba zaidi na Zanzibar inakwenda na maji kuliko ile inayosema Jamhuri ya Tanzania ni nchi moja. Sasa mkitwambia kuwa Katiba hii inaondoa mambo yote ya Muungano na ikiwa hivi ndivyo inavyoeleza na hivi ndio tunavyokwenda kuipigia kura ya maoni naomba Mhe. Naibu Spika, kwa umakini

au kwa yeyote anayehusika atueleze ni kwa misingi gani Katiba hii imeweka uhuru wa Zanzibar kama ni nchi huru, uhuru wa Tanganyika kama ni nchi huru na kwa Muungano wetu wa nchi mbili zilizo huru. Sio Muungano wa nchi moja yenye mamlaka kamili.

Mhe. Naibu Spika, naendelea na naomba univumilie kwa mujibu wa Katiba hii tunayokwenda kuipigia kura ya maoni...

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa na mimi naomba unisikilize kidogo naona umetoka nje ya bajeti kabisa. Umeshasoma Katiba zote mbili toa mawazo yako songa mbele, lakini unarudia hapo kwa hapo. Toa mawazo yako.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Naibu Spika, wenzangu wamezungumza saa nzina. Mimi nilosema nataka ufahamu wa kunifahamisha wapo hapa Katiba hii tusisahau kuwa alikuwepo Mwanasheria Mkuu akatoa ushauri wake na akafukuzwa kazi. Sisi ndio Wawakilishi wa wananchi tunataka tukawaelekeze sasa kama sikueleza ninavyojua mwenyewe ukanifamu mkanielekeza, na nilisema nataka nipewe maelekezo. Kwa hivyo, maelekezo yangu nitapewa wapi. Ndio nikasema naomba univumilie.

Mhe. Naibu Spika: Sasa nimekuvumilia muda mrefu.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Sasa basi kwa hivyo, kwa sababu naomba tu nizungumzie kifungu cha mwisho na vyengine vyote naviacha hapa.

Kwa hivyo cha mwisho kitakuwa ni kifungu cha 294 ukurasa wa 258 ambayo ukurasa huu wa 258 nasikitika Mhe. Naibu Spika, kwa kunikata lakini basi, nasikitika sana. Ukurasa wa 258 kifungu 294 kinasema hivi:-

"Mambo yafuatayo yatafanyika na kukamilika katika muda wa mpito"

Ninalokusudia kusema moja kubwa ni kuwa kurekebisha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 ambayo ndiyo hii ili kuwiana na masharti ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 2014.

Suala langu kwa sababu nilikuwa nasema mengi umenikatiza, kwa sababu huku inasema Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni nchi moja yenye mamlaka kamili, na sisi tunasema kuwa Zanzibar ni nchi kama ilivyo katika Katiba yetu.

Katiba ya Zanzibar itabidi ifanyiwe marekebisho kifungu hichi tu cha uhai wa Zanzibar kitabadilishwa kiwe vipi, kwa sababu hakiwezi kukaa kikapingana na Katiba ya Muungano, mengine nayaacha kwa heshima yako tuendelee.

Mhe. Naibu Spika, sasa ninalipenda kuzungumza ni jambo dogo tu ambalo limetajwa katika kitabu hichi ni kuhusu Ikulu ndogo ya Micheweni, na taarifa hii imo katika kifungu cha 115 tena ukurasa wa 43 na nikifungua ukurasa huu wa 43 kwa ruhusa yako Mheshimiwa unasema hivi naeleza pale nilipokusudia tu sio kusoma kifungu chote kwa ruhusa yako.

"Katika azma ya kujenga Ikulu ndogo ya Micheweni michoro ya Ikulu hiyo imeshafanyiwa mapitio na utoaji wa zabuni na utaratibu wa kumpata mjenzi unaendelea".

Mhe. Naibu Spika, mimi pamoja na Kamati ya Viongozi Wakuu ilikuwa tukifatilia sana ujenzi wa Ikulu hii ndogo na matatizo yake ya kutowalipa wakandarasi au tuseme mjenzi Kampuni ya Ahly, na bahati nzuri hata juzi nilijibiwa, na majibu niliyopewa na Mhe. Waziri ni kuwa Ikulu hii wale watu waliohusiana na ujenzi tayari walikwishapewa haki yao, na kwamba hakuna mgogoro wowote unaoendelea. Nilieleza kuwa walikwishakaa pamoja, walikwishakubadilishana mawazo na walikwishalipana.

Sasa mimi Mhe. Naibu Spika, linalosikitisha ni kuwa majibu niliyoyapata yalikuwa hayaendi na uhalisia. Mhe. Naibu Spika, *contractor* huyo Ahly alikwenda Mahakamani na uamuzi ukatoka wa Mahakama tarehe 5/9/2008 na uamuzi huu ulikuwa kama ifuatavyo naomba kunukuu.

"Kwa kuwa mdai amefungua kesi dhidi ya wadaiwa na kulipwa fidia kwa kukatishwa kwa mkataba wake wa ujenzi alioingia tarehe 1/7/2004 na 13/6/2006 baina yao kwa kujenga nyumba ya mapumziko nyumba ya walinzi, uzio, jiko na kibanda cha mlinzi huko Micheweni Pemba"

Kwa kuwa mdai aliendelea na ujenzi kama walivyokubaliana lakini wadaiwa walishindwa kutekeleza majukumu yao ya kugharamia ujenzi huo ipasavyo. Na kwa kuwa mdai aliendelea na ujenzi kwa gharama zake mwenyewe bila ya kupata msaada kwa wadaiwa isipokuwa gharama za awali za ujenzi huo, na kwa kuwa wadaiwa wamekatisha mkataba huo bila ya kulipwa gharama alizotumia katika kipindi chote cha mkataba, hivyo basi, mdai na wadaiwa wamekubaliana yafuatayo:-

(a) Wadaiwa watamlipa mdai jumla ya shilingi milioni mia moja na nane na laki tatu (108,300,000), ikiwa ni gharama za ujenzi alizotumia pamoja na usumbufu;

(b) Fedha hizo zitalipwa kwa awamu tano ambazo zitakuwa jumla ya shilingi milioni ishirini laki nane na sitini (20,860,000) kwa awamu kuanzia mwezi wa kusaini makubaliano hayo;

(c) Fedha hizi zitalipwa moja kwa moja kutoka katika Bajeti ya Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba kwa mujibu wa muundo wa wizara ilivyokuwa wakati huo; na

(d) Makubaliano haya yamechukuliwa kama ni hukumu katika Mahakama hii, na kwamba iwapo wadaiwa wameshindwa kukamilisha masharti ya mkataba huu mdai anaweza kukaza hukumu. Kukaza hukumu mimi sijui maana yake imetiwa saini na mwenyewe Ahly shahidi wake na vile vile shahidi wa Mahakama.

Mhe. Naibu Spika, kwa sababu walichelewa kulipa walikuja Baraza hili Tukufu, na Baraza likatoa maelekezo kwamba kwa sababu kesi imeshafika mahakamani wao hawawezi kumsaidia vyovyote na barua hii hapa.

Halafu tena kuna agizo na agizo hili alipelekewa Katibu Mkuu Afisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora Zanzibar barua ya tarehe 23/12/ 2013 na kichwa chake cha maneno kinasema:-

"Ujenzi wa *Rest House* Micheweni Pemba,barua inaeleza hivi. Kwa heshima kubwa naomba uhusike na mada iliyoko hapo juu".

Kufuatia maamuzi ya serikali kukamilisha ujenzi wa *Rest House* Micheweni Pemba unatakiwa umtake Injinia wetu awasiliane na *contractor Ahly Construction Company* ili ampatie maelekezo katika maeneo yafuatayo; eneo kwa ujenzi wa jiko, eneo kwa ajili kwa ujenzi wa kibanda cha mapokezi, eneo kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ya walinzi, *design* ya fensi, maelekezo ya mabadiliko yoyote yatakayohitajika katika nyumba ikiwemo kuongezwa urefu wa nyumba kwa juu. Hii barua inatoka kwa Katibu Mkuu Wizara ya Fedha.

Lakini Mhe.Waziri alinijibu kuwa ameshalipwa huyu mtu, binafsi mimi kaniona kwa sababu suala lake nalifuatilia na akanambia hajalipwa na ushahidi ni kuwa jana tarehe 26/5/2015 kuna barua hii imeandikwa ndugu Ali Salim Ali, *Ahly Construction Limited.* Asalam Alaykum suala hili aliachiwa Mhe. Omar Yussuf Mzee ni waziri wetu wa fedha kulimaliza na wewe tafadhali muone muyazungumze ahsante Dkt. Mwinyihaji Makame.

Sasa mimi naomba kupata ufafanuzi, huyu kuna mtu mwengine alikuwa akilipwa badala yake, maana naona huyu tunayesema akilipwa haya ni maelezo yake. Mhe. Waziri kwa ruhusa yako naomba ufafanuzi wa kina, kwa sababu hii serikali ni serikali inayotenda haki haimdhulumu mtu, na mtu asionewe kutokana na udhaifu wake.

Jengine nimalizie sasa kwa kamati ya *PAC* na Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali. Mhe. Naibu Spika, hii nasoma kwa pamoja kifungu 88,89 na 90 katika ukurasa wa 34 naomba ruhusa yako na hii itakuwa ndio mada yangu ya mwisho.

Mhe. Naibu Spika, Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imeimarisha uwezo wa wafanyakazi wake kitaaluma katika fani mbali mbali za ukaguzi, na fani hizo ikiwemo ukaguzi wa kimazingira, ukaguzi wa Kompyuta, uchambuzi wa taarifa za ukaguzi, ukaguzi yakinifu, muongozo wa ukaguzi na vile tumeleezewa kuwa kuna wafanyakazi 50 wamepatiwa mafunzo ya ukaguzi, na hayo mafunzo waliyopatiwa yamo, lakini kwa kuyasoma naona kama wakati umekuwa mkubwa.

Na si hivyo tu katika kifungu cha 90 ni kuwa wafanyakazi, hayo wamepatiwa mafunzo juu ya ukaguzi wa hesabu unaozingatia viwango vilivyowekwa kitaifa na kimataifa katika ufungaji wa hesabu na uwekaji wa kumbukumbu za hesabu, nifike hapo.

Hii naipongeza Afisi ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kutoa taaluma kwa wafanyazi wake ili wamudu kuifanya kazi yao vilivyo ya ukaguzi kwa maslahi ya Taifa.

Mimi Mheshimiwa jambo ninalosikitika sana ni kuwa ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ikishatengenezwa, ikishapitisha na baada ya kupewa Mhe. Rais inakuja katika Baraza la Wawakilishi, kila Mjumbe anapewa kopi ili ifanyiwe kazi kwa ufanisi na wanaofanya kazi ni Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ambalo Mhe. Spika kwa mujibu wa Kanuni ndiye mwenye mamlaka ya kuunda Kamati za Kudumu, na moja ni Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali inayokwenda moja kwa moja na Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Hawa ni wanasiasa tu, wanatoka katika majimbo yao na wanapangwa katika Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, isipokuwa Mawaziri, Manaibu Mawaziri na Mwanasheria Mkuu pamoja na Spika mwenyewe.

Jambo la kusikitisha ni kuwa, kwa sababu Kamati ya *PAC* na ikiwa itafanya kazi ipasavyo, ndivyo wataweza kuichambua ipasavyo ile ripoti ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali na ni ya kitaalamu. Kwa hivyo, watendaji wa Ofisi hii ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali tayari wameshapatiwa mafunzo wanafanya kazi yao kitaalamu. Lakini Kamati ya *PAC* inayopitia ripoti ile wanakwenda tu kutokana na Mwenyezi Mungu anavyowajaalia.

Matokeo yake wanajitahidi, wao ni wakaidi sana wanatafuta misaada na kila mbinu waweze kuingia katika *system* lakini si rahisi. Kwa hivyo tuna lazima kipindi cha miaka mitano na *inshaallah* Mwenyezi Mungu atujaalie tuingie katika uchaguzi salama na usalimini, na Baraza letu la Wawakilishi liendelee liwe imara na nchi ya Zanzibar iwe huru, lakini tunahitaji watendaji wake.

Kwa hivyo, kwa huko usoni tunakokwenda ninaomba tena kwa heshima zote Serikali ione umuhimu wa kuwapa taaluma Wajumbe wa Kamati ya *PAC,* ili waweze kufanya kazi yao kwa ufanisi kutokana na mabadiliko ya mambo yanavyokwenda tokea kwenye ukaguzi na mazingira yake ya kidunia. (*Makofi*).

Kwa hayo machache Mhe. Naibu Spika, naunga mkono. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika: Tunakushukuru Mhe. Salim Abdalla Hamad. Sasa tunamalizia na Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana na mimi kunipa fursa ya kuweza kuchangia mawili matatu katika bajeti hii muhimu iliyowasilishwa hapa na Mzee wangu Mhe. Mwinyihaji Makame Mwadini - Waziri wa Nchi (OR), Ikulu na Utawala Bora.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo vile vile niwapongeze Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote wakiongozwa na Katibu Mkuu katika taasisi hiyo kwa kazi kubwa na nzuri ambayo hatimaye leo imeweza kusababisha hichi kitabu kuja hapa.

Mhe. Naibu Spika, katika Wizara hii kuna mengi yamefanywa. Kama tungelifanya kazi ya kuja kukusanya yote ambayo Mhe. Rais amefanya, kutoka kipindi chake kama tunavyokiona hichi kitabu, maeneo mengi yalikuwa yanagonga kuanzia kumi na moja hadi kumi na tano. Tungekuwa na vitabu kama sita hivi, lakini kwa muhtasari wa kukusanya baadhi yake na kuweza kuyaleta haya ambayo wameyaleta, hii ni sehemu tu ya yale ambayo yamefanywa chini ya usimamizi wa kiongozi wetu shupavu, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, Waarabu wana maneno huwa wanasema na aya hii imo katika aya za *Qur-an* na Dkt. Salmini Amour Juma, Rais wa Awamu ya Tano alikuwa akilipenda sana. Na aya zenyewe Mhe. Naibu Spika, zinasema "*Khuliqal-insaana halua, idhaa massahuu sharru jazua, waidhaa massahul khayru manua, illal muswalliin".*

Mhe. Naibu Spika, maana yake ni kwamba nimemuumba mwanadamu kwamba awe ni kiumbe asiyefahamika, asiyetabirika, asiyeeleweka. Ukimpatia shari

utamuona namna anavyohangaika, lakini ukimpa kheri huwa anaing'ang'ania, hataki imtoke. (*Makofi*).

Hii ndiyo maana ya tafsiri ya maneno ambayo nilikuwa ninayazungumza. Wale Maulamaa ambao wapo kama itakuwa nimekosea naomba radhi na *inshaallah* wanirekebishe katika utaratibu huo.

Mhe. Naibu Spika, ninazungumza maneno haya kwa sababu tokea tumeanza bajeti zetu hapa tunahubiri amani na utulivu katika nchi yetu. Lakini kinachonishangaza mimi Mhe. Naibu Spika, ninahisi haya maneno ya amani hayatoki kwenye vifua vyetu, yanatoka kwenye ndimi zetu. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, ningeomba sana wale ambao wana udhati wa neno amani katika nyoyo zao wazungumze neno hili kwa ajili ya kulizungumza kwamba linatoka katika sakafu za nyoyo zao, siyo katika ndimi zao. Tumesikia hapa wengi wanazungumzia suala kwamba kuna wenzetu wanaonekana wapiga bao hapa, wanafikia hadi kudiriki kusema kwamba tayari kunaonekana kutakuwa na matatizo katika uchaguzi unaokuja mbele. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, mimi silioni hilo. Ninachokifahamu mimi na tena si hayo tu, kuna wengine kuna maneno mazito wanazungumza, tutang'ang'aa, aah! jamani. Chama kinachoendelea kutawala, kwanza kina asili ya kutawala chama hichi. Chama kinachoendelea kutawala kinashinda kwa sababu ya uzuri wa ilani yake. Ilani ambayo kwa vipindi lukuki tumekuwa tukienda tukiinadi kwa wananchi, na wananchi badala yake wanaikubali, wanaipitisha kwa kura nyingi kabisa. (*Makofi*).

Ni imani yangu baada ya marekebisho ambayo yamesimamiwa na kutengenezwa ilani mpya na Mzee wangu; Mzee Wassira pamoja na mjumbe wake swahibu wangu hapa Mahmoud Thabit Kombo na wengine na wengine, ilani itakayoletwa kwetu itakuwa ni nzuri zaidi, na wananchi hawatakuwa na sababu ya kuikataa ilani hiyo na watakipa ridhaa Chama cha Mapinduzi kiendelee kuongoza. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, nilisema nianze na hayo kwa sababu ya kuangalia lile neno linaloashiriwa kila mara. Unajua chombo hichi cha Baraza la Wawakilishi ni chombo kikubwa sana Mhe. Naibu Spika. Tunapokaa kila mara kuwatisha wananchi wetu si jambo jema wala siyo jambo linalotarajiwa viongozi wa nchi kwenye nafasi za Uwakilishi katika nchi yetu kila mara kuhubiri machafuko katika nchi yetu, si jambo zuri. (*Makofi*).

Sote kama tunakuwa tunajiamini, sote kama tunafahamu kufuata utawala bora, sote kama tunasema kwamba tuna uwezo wa kushinda, twendeni kwa wananchi. Wananchi watatupima, wakiona ipo haja ya kuendelea kuwapa Chama cha

Mapinduzi kuendelea kuongoza, watatupa ridhaa hiyo, wakati ndiyo kawaida yao na wakiona kwamba ipo sababu ya kusema vyenginevyo, watasema. Kwa nini tunatishana kila mara humu ndani. Kila anayekuja hapa amani, lakini uchaguzi huu utakuwa huru na wa haki na wa salama. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, ninavyofahamu mimi chini ya uongozi wa Dkt. Ali Mohamed Shein katika kampeni zake zote alizokuwa amepiga, tulikuwa sisi sote ni washirika wake, tulitembea naye Kusi, Kaskazi, Mashariki na Magharibi. Hatukuona pahala ambapo alikuwa anatuamrisha au kutuhamasisha kufanya fujo au kutoa matusi. Maisha yake yote katika kampeni zake mwaka 2010, alikuwa akituhamasisha tufanye uzuri uchaguzi na kampeni za kistaarabu, na ndicho kilichokuwa kimefanyika. (*Makofi*).

Sasa leo tukikaa hapa kila mara, kila anayekuja hapa uchaguzi utakuwa hivi, jamani hebu tusiwasemee watu kuwapangia watu mambo ambayo hayapo. Tuingie katika uchaguzi huu tukiwa tunajiamini na *inshaallah* Mwenyezi Mungu ndiye wa kuombwa na tuombe amani na salama katika nchi yetu. Hilo ndilo la kusimamia na kuliomba, siyo kila mara tunakaa kuzungumza vitu ambavyo havipo. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, nikimaliza ninaelekea katika Kifungu cha 45 cha kitabu hichi.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi.

MUONGOZO

Mhe. Mwanajum Faki Mdachi: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana, naomba unipe muongozo wako kwa sababu tunachangia lakini hatujui kama huku kuchangia kwetu tunaojibu ni sisi au anayejibu ni Waziri. Naomba unipe muongozo Mhe. Naibu Spika. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika: Mimi ninadhani Mheshimiwa apewe nafasi ya kuchangia, kila mtu kachangia hapa kwa uwezo wake, aliyesoma Katiba amesoma, aliyekuwa hakusoma.

Sasa na yeye anahubiri amani na utulivu wa nchi yetu, na kishamaliza anakuja kwenye kitabu, lete hoja kwenye bajeti. (*Makofi*).

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Mhe. Naibu Spika, pale mwanzo nilikuwa ninazungumzia suala la amani pamoja na utawala bora.

Lakini sasa ninaingia Kifungu cha 45. Ninachukua fursa hii kumshukuru sana Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa namna ambavyo Ofisi

yake ya Faragha iliweza kuratibu ziara 31 za ndani na vile vile kufanikisha shughuli za kiserikali katika ziara hizo kwa upande wa Unguja, Pemba, Dar Es Salaam, Dodoma, Arusha na Lindi.

Aidha, ninapenda kuchukua fursa hii vile vile kumshukuru sana Rais wa Zanzibar na shukurani hizi ninazitoa kwa niaba yangu na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kikwajuni, kutokana na ahadi yake ambayo aliitoa ya kutengenezwa barabara kutoka Darnaus pale mpaka Skuli ya Kisiwandui, na hilo likawa limetimizwa. Ninatoa shukurani za dhati kabisa kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Wawakilishi kutoa kauli na baadae ikawa imetimizwa katika Jimbo la Kikwajuni. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, nikiondoka hapo ninakwenda katika Kifungu cha 149. Mhe. Naibu Spika, kifungu hicho kilikuwa kinazungumzia hotuba ya bajeti ambayo ilikuwa imewasilishwa hapa na suala zima la utawala bora pamoja na kujenga uchumi madhubuti ambao ni endelevu.

Mhe. Naibu Spika, siyo siri kabla ya kuingia madarakani Dkt. Shein ilikuwa hakuna utaratibu wa kuweza kufanya kazi ya kuzichunguza Wizara kwa yale mambo na bajeti ambazo tulikuwa tunazipitisha hapa katika Wizara katika viongozi wakuu kule. Lakini tokea kuingia uongozi wa Dkt. Ali Mohamed Shein ametengeneza utaratibu wa bango kitita. Sasa matokezeo yake imekuwa Wizara zote zinafanya kazi zake kwa umakini, kwa kujua kwamba kila baada ya miezi mitatu wana pahala wanakwenda kuhojiwa, na hatimaye wanakwenda kupeleka taarifa ya mambo ambayo walikuwa wameyafanya, lakini yakiwa na malengo ya utekelezaji wa bajeti ambayo ilikuwa tumeipitisha hapa kama Wawakilishi wa wananchi wa Zanzibar ambao tulikuwa tumechaguliwa na wananchi hao. Mhe. Naibu Spika, ninaipongeza sana hatua hiyo ya Dkt. Shein kwa kazi hiyo ambayo alikuwa anaifanya. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, nikiondoka hapo ninakwenda Kifungu cha 188. Mhe. Naibu Spika, hebu nimuombe Mhe. Waziri atakapokuja hapa, katika Kifungu hichi cha 168 kuna suala zima la programu hii inayotekelezwa sambamba na miradi, kuna Kifungu (a), (b) na (c). Mimi ninamuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa anisaidie programu (b) ambayo ina mpango wa kurasimisha raslimali na biashara za wanyonge (MKURABITA).

Mhe. Naibu Spika, ninamuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa anielezee kwa faida ya Baraza lako hili Tukufu ni namna gani Wazanzibari wananeemeka na programu hii ya (MKURABITA). Namuomba Mhe. Waziri anisaidie hasa tuone na maeneo yepi ambayo yananeemeka katika mradi huu.

Nikiondoka hapo Mhe.Naibu Spika, ilikuwa ninakuja katika eneo la Kifungu Nam. 169 ambacho hichi kilikuwa kinazungumzia programu ya usimamizi wa uchumi mkuu. Naomba ninukuu baadhi ya maneno ya hapa Mhe. Naibu Spika,

"Programu hii lengo lake ni kuandaa sera madhubuti za kiuchumi na sera za kodi na kufanya tafiti za kiuchumi na kijamii kutokana na vipaumbele vya Taifa. Programu hii ni Zanzibar kuimarika kwa viwanda vidogo vidogo na vya kati. Aidha, kuwa na huduma bora za miundombinu ya kiuchumi na kijamii kwa kupitia idadi ya miradi iliyoratibiwa katika mfumo wa mashirikiano baina ya sekta ya umma na sekta binafsi. Programu hii ina programu ndogo mbili".

Bado tuna tatizo katika suala zima la viwanda, kwa sababu ili tuweze kukuza uchumi wetu Mhe. Naibu Spika, tunahitaji kuwa na viwanda ili viweze kutusaidia. Ni jambo la faraja, juzi tu nilisikia kwamba Kiwanda chetu cha Mahonda kinatiwa mashine mpya na kinafanyiwa ukarabati ili kiweze kuwa *modern* zaidi. Lakini ningeomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa anisaidie hasa kuna mkakati gani wa kuweza kuvishamirisha hivi viwanda ndani ya nchi yetu ili viweze kunyanyua uchumi wetu kama ambavyo maeneo mengine yanavyonyanyuka. Mhe. Naibu Spika, ninamuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa anisaidie namna walivyojipanga kwa ajili ya hiyo. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, lakini nikiondoka hapo ninakwenda katika Kifungu cha 180. Hapa nimeona makusanyo, na makusanyo haya mimi nilitishika kidogo, kwa sababu nilipoambiwa kwamba Ikulu inakusanya, niliona hee! huku Ikulu kwani kunafanywa biashara siku hizi. Kumbe haya makusanyo yanatokana na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Lakini nikiangalia makusanyo yenyewe sasa ni ya shilingi milioni ishirini na nane, nukta mbili (28.2). Sasa nikiangalia ukubwa wa hii taasisi yenyewe na makusanyo haya ya taasisi hii, mimi ninaona kwamba siyo vitu ambavyo vinalingana sana. Ningemuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa anisaidie, hii *twenty eight point two millions* ambayo wameiweka hapa kwamba ni makisio ya makusanyo *basis on what?*

Baada ya maelezo hayo sasa. Kwa mara nyengine tena nichukue fursa hii kuwashukuru sana wenzangu hususan katika Wizara hii pamoja na wale wasaidizi wa Dkt. Ali Mohamed Shein, ninakusudia Makamu wa Kwanza wa Rais pamoja na Makamu wa Pili wa Rais kwa namna ambavyo wanasaidiana na kushauriana na Rais wa Zanzibar na watendaji wote kwa ujumla wakiongozwa na Katibu Mkuu wao pamoja na Waziri katika kukamilisha yale mambo ambayo wameifanya kwa umakini wa hali ya juu ndani ya Wizara hii, na *inshaallah* Mwenyezi Mungu amjaalie uwezo zaidi katika kipindi cha mbele kinachokuja baada ya uchaguzi wa

2015 mwezi wa Oktoba, Rais Shein atakapoapishwa tena ili waje na mipango mizuri zaidi na tuweze kuendelea kula matunda na manufaa ya uongozi wa Dkt. Ali Mohamed Shein kwa ujumla wake.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo kwa niaba yangu na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kikwajuni naunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia kwa mia.

Mhe. Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe ninawashukuru lakini kabla sijaahirisha naomba niseme mambo mawili.

Jambo la kwanza hivi sasa tunachangia bajeti ya Serikali. Si uzuri kutoka kwenye bajeti ukaenda kwenye mambo mengine, mambo mengine muda utafika mwenye hoja zake atasema, mwenye sera zake na wananchi wataaamua. Sasa hivi tuchangie bajeti, maana yake wananchi wanatusikiliza. *(Makofi).*

Suala la pili ni kwamba majadiliano yanaendelea lakini majina yamekwisha kwa leo. Naomba Waheshimiwa kesho asubuhi tukijaaliwa baada ya maswali tuchangie ili jioni tuimalize bajeti hii. (*Makofi*).

Baada ya haya niwashukuru kwa kushirikiana na mimi tangu jioni hii mpaka sasa hivi. Ninaahirisha kikao chetu hichi hadi kesho siku ya Alhamis tarehe 28/05/2015, saa tatu barabara za asubuhi.

(Saa 1:42 usiku Baraza liliahirishwa hadi
tarehe 28/05/2015 saa 3:00 asubuhi)